ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Tatu - Tarehe 16 Juni, 2015

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika**,** naomba kuweka hati mezani kuhusiana na Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2015/2016. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 56

Matayarisho ya Soka la Ufukweni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza**:**

Soka la ufukweni (*beach football*) ni mchezo unaoinukia na kuanza kupendwa na hivyo kupata washabiki wengi katika Mataifa mbali mbali ya Ulaya, Ghuba ya Uajemi, *UAE* pamoja na Afrika. Kwa kuwa timu ya Taifa ya Tanzania, kuna taarifa kwamba inajitayarisha kwa ajili ya Kombe la Dunia la mchezo huo.

(a) Je, Zanzibar zipo timu za soka la ufukweni.

(b) Timu ya Taifa ya Tanzania itashiriki kwenye mashindano ya soka la ufukweni ni ya Jamhuri nzima au ni ya upande mmoja wa Muungano.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli mchezo wa Soka la Ufukweni ni mchezo unaoinukia na kuanza kupendwa, na hivyo kupata mashabiki wengi katika Mataifa mbali mbali duniani.

Mhe. Spika, aidha ni kweli Tanzania inatayarisha Timu ya Taifa kwa ajili ya Kombe la Dunia. Baada ya kueleza hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, Zanzibar ndio ya mwanzo Tanzania kuanzisha timu ya soka la ufukweni. Hivi sasa zipo timu 12 za soka la ufukweni zinazoshiriki katika ligi ya Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba Zanzibar ndio ya kwanza kuanzisha timu hizo, ninachoweza kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi ni kwamba kila inapoundwa timu ya Taifa ya Tanzania, Zanzibar inashirikishwa ambapo hutoa wachezaji saba na Tanzania Bara saba kuingia kambini na baadaye kuchaguliwa wachezaji 10 kushiriki katika mashindano ya Kimataifa.

Mhe. Spika, katika mchezo na Kenya Zanzibar ilitoa wachezaji wanne na watatu tulipocheza na Misri.

Katika mashindao ya Kombe la Dunia, Afrika huwakilishwa na timu mbili, lakini kwa kuwa Tanzania ilikwishatolewa na Misri, hivyo haiko tena katika mashindano hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali la msingi ni kuhusu soka la Ufukweni, na kwa vile soka hili linatokana na *FIFA* linachangia dola laki mbili na nusu kwa Tanzania, na Tanzania inatokana na jina Zanzibar. *CAF* inatoa dola laki moja na Ufukweni inasaidia pesa na inaandaa miradi inapelekwa kule *FIFA*.

Ninachojua mimi tu tokea kupata bahati hii kwa mchango kutoka *FIFA* Zanzibar imefaidika na Uwanja wa Gombani tu kwa nyasi za bandia.

(a) Mhe. Naibu Waziri unaweza kutwambia kipi tulichofaidika tokea kuungana kwenye *FIFA* kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara.

(b) Katika Uteuzi wa Timu ya Taifa mara nyingi tumekuwa tukishuhudia kocha kutoka Tanzania Bara, madaktari kutoka Tanzania Bara ndio wanaoshirikishwa, hata safari wanazokwenda ni tabu kushirikishwa kiongozi kutoka Zanzibar. Je, unatoa kauli gani Mhe. Naibu Waziri kuhusu hili.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Mjumbe hili swali la mgao naona kama liko nje ya swali hili. Kwa sababu hapa ni suala la Mchezo wa Soka la Ufukweni na kutaka kujua kama Zanzibar ipo timu na Timu ya Taifa ya Tanzania.

Kwa hiyo, hili la mgao naona ulitafutie utaratibu wa kuliuliza kwenye swali la msingi. Hivi la pili lilikuwaje?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali linahusu Soka la Ufukweni lakini kutokana na Kanuni zetu za mpira linasimamiwa na *FIFA*.

Mhe. Spika: Swali la pili lilikuwa vipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Katika uteuzi wa Timu ya Taifa tumeshuhudia mara nyingi kocha akitoka Tanzania Bara na Madaktari kutoka Tanzania Bara. Msafara wote au benchi la ufundi linaongozwa na ndugu zetu wa Tanzania Bara, si rahisi kumkuta mtu kutoka Zanzibar. Je, analitolea kauli gani suala hili.

Mhe. Spika: Kwa hiyo, hiyo timu ya Soka la Ufukweni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa sawa Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, uhusiano wetu na wenzetu wa Bara katika suala la *FIFA* linajulikana ni suala la muda mrefu. Zanzibar sio mwanachama wa *FIFA*, tumejaribu kujiunga hatukufanikiwa kwa sababu hatuna *sovereignty* huo ndio ukweli wenyewe. Sasa wenzetu ndio walionao, na kwa sababu wanao ndio ambao wanasimamia masuala haya.

Sasa katika kuchagua timu kama mwenzetu Mhe. Naibu Waziri amezungumza hapa tunapeleka wachezaji wanafanyiwa mazoezi, ambao wame- *prove best* ndio ambao wanachaguliwa kujiunga. Sasa hayo ndio ambayo ya msingi ambayo tunayashughulikia.

Sasa kusema kwamba madaktari na watu wengine ni suala ambalo wenyewe ndio wanasimamia Afisi ya *FIFA* ambayo ni Dar es Salaam, ndio ambao wanasimamia kazi hii. Bado hatujaweza kulitatua hili, nilidhani kupitia Katiba ile iliyopendekezwa tungelipata hili, bahati mbaya sote tulikuweko Dodoma hakuna ambaye alilizungumza hili. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ulikuwepo na ulikuwa na nafasi nzuri ya kulitoa, lakini hakuna hata mmoja aliyelizungumza kama *FIFA* na michezo wanatusumbua.

Mhe. Spika sasa litaendelea kutusumbua mpaka ambapo tutaamua uhusiano wa kimichezo katika Jamhuri ya Muungono wa Tanzania katika Katiba ambayo inapendekezwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri pamoja na Waziri kwa majibu yao mazuri.

Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba Zanzibar kwa Tanzania ni wa mwanzo kuanzisha mchezo huu wa mpira wa miguu wa Ufukweni, na timu 12 tayari zinashiriki katika mashindano ya Zanzibar.

(a) Hizo timu 12 ni zipi.

(b) Amesema kwamba katika jibu lake (b) wachezaji 7 kutoka kila Upande; yaani Zanzibar na Tanzania Bara kuunda timu ya Taifa na baadae huchaguliwa wachezaji 10 hushiriki mashindano mbali mbali ya kimataifa.

Je, kwa vile Zanzibar ni waanzilishi wa mwazo kwa Tanzania kwa mchezo huo wa mpira wa miguu wa Ufukweni, je, katika hao viongozi yaani makocha, madaktari, na viongozi wengine wa timu, Zanzibar tunatoa viongozi wangapi au makocha wangapi ambao wanaunda timu hii ya Taifa ya Tanzania.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, timu hizi 12 nyingi zipo katika Wilaya ya Mjini na nyengine zipo katika Wilaya ya Kaskazini na Kusini.

Wito wangu ni kwamba mchezo huu kwa Zanzibar tuna nafasi pana zaidi kwa vile kuna fukwe nyingi na vijiji vingi vya Zanzibar vina nafasi ya kucheza.

Ombi langu kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi washajihishe wachezaji wa mchezo huu katika majimbo yao ili tuhakikishe kwamba tuna nafasi nzuri sana ya kushinda.

Katika suala la sisi katika uongozi mzima wa timu hii ambayo inashirikisha kikosi kile cha Muungano, naomba swali hili nimjibu kwa maandishi.

Mhe. Spika: Hiyo pamoja na timu zenyewe ni zipi kwa sababu nalo pia aliuliza.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ndiyo.

Mhe. Spika: Haya, Mhe. Waziri na Naibu Waziri tunawashukuru.

Nam. 57

Taarifa ya Habari kusomwa kwa Lugha ya Kiingereza

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC)* kupitia Redio yake pamoja na mpangilio wake wa vipindi huwa lina kawaida ya kusoma taarifa ya Habari kwa lugha ya Kiingereza kwa wakati wa saa 3:00 usiku.

(a) Je, nini madhumuni makuu na sababu ya msingi ya kutumia lugha ya Kiingereza kwa taarifa hiyo ya Habari.

(b) Kwa nini matangazo hayo kwa lugha ya Kiingereza yasiwe kwa vipindi au matangazo mengine zaidi ya hiyo taarifa ya Habari.

(c) Kwa nini hata hiyo taarifa ya habari ya saa 3:00 siku nyengine huwa haisomwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye kifungu (a), (b) na (c), lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) Redio kupitia vipindi vyake wakati wa 3:00 usiku huwa na kawaida ya kusoma taarifa ya Habari kwa lugha ya Kiingereza.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya *ZBC* kutoa taarifa hiyo kwa lugha ya Kiingereza ni kuwapatia fursa wasikilizaji wa Redio hiyo wasiofahamu vizuri lugha ya Kiswahili kusikia taarifa muhimu za ulimwenguni.

(b) Mhe. Spika, vipindi na matangazo mengi ya lugha ya Kiingereza yasiyokuwa taarifa ya Habari hutolewa na *ZBC* Televisheni inapoungana na Sauti ya Ujerumani (*DW)* nyakati za usiku na asubuhi.

(c) Mhe Spika, inavyotakiwa kila siku saa 3:00 usiku *ZBC* Redio itoe taarifa ya Habari ya Kiingereza. Inapokosekana kusikika taarifa hiyo ya Habari huwa kuna sababu maalum zisizoweza kuepukika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, katika uchunguzi wangu nilioufanya taarifa ya habari ya Kiingereza haipatikani kutokana na ukosefu wa *internet* katika chombo chenu hichi, na *internet* hiyo kwa mwezi ina-*cost* shilingi elfu arubaini. Sijui mnachukua hatua gani kufuatilia majukumu yenu, kuna kitu *internet* katika kufuatilia kwangu inakosekana kusoma taarifa ya habari ya kizungu, na kufuatilia *internet* hiyo kwa mwezi ina-*cost* elfu arubaini. Hamuoni wajibu wenu umekushindeni na lini mtafuatilia matatizo hayo.

Ulipokuwa unajibu swali la msingi Mhe. Naibu Waziri ulisema *ZBC* inapoungana na Sauti ya Ujerumani *DW* wakati wa usiku. Hivi sasa kwa taarifa niliyonayo naona hapa watangazaji wetu hawa wana kifaa kinaitwa *link* wakitaka kuungana kutoka Barazani na studio unachukuwa dakika tano.

Mna mpango gani kabla ya bajeti kuja kuipitisha kukitafuta kifaa hicho kabla ya kupitisha bajeti hii kuna kifaa kinaitwa *link*, watanganzaji wetu hawa wanapoungana na studio wanachukua dakika tano kuungana. Kabla ya kupitisha bajeti hapa mnatoa kauli gani kuhusu suala hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, mimi sina taarifa kwamba ili taarifa ya habari isomwe pale *ZBC* lazima iwepo *internet*. Kwa hivyo, taarifa ya habari iwe ya Kiswahili, iwe ya Kiingereza iwe ya lugha nyengine yoyote, taarifa ya habari kama ya kawaida mtangazaji anatakiwa awepo *studio* asome.

Sasa kwamba iwepo *internet* ndio taarifa ya habari ya Kiingereza isikike hili mimi sina habari lakini nitalifuatilia pengine sijaarifiwa vizuri.

Kuhusu *link* iliyopo Barazani ambayo inaungana na *Microwave link* iliyopo *ZBC*. Taarifa niliyonayo inafanya kazi vizuri na haina tatizo, na kama vijana wana tatizo la kiufundi basi wakubwa wao hawajui. Haiwezekani kwamba tumenunua *link* karibuni mpya tu kwa shilingi milioni karibu sabini.

Sasa ukisema kwamba kuna tatizo sisi hatuna taarifa hiyo, baada ya kumaliza hili suala labda nitoke nipate ufafanuzi zaidi, mambo madogo madogo haya tutarekebisha Mhe. Spika, kama tumeweza kuinunua kwa shilingi milioni sabini, kama kuna jambo dogo dogo tu la kiufundi ambalo labda ni *relay* au jambo jengine linaloweza kugharimu shilingi milioni moja, hili tunaweza kulifanyia kazi bila ya tatizo.

Mhe. Spika: Tunawashukuru Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri. Katibu tunaendelea!

(*Majadiliano yanaendelea*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Asubuhi ya leo nafasi ya kwanza inakwenda kwa Mheshimiwa Nassor Salim Ali na atafuata baadae Mhe. Mgeni Hassan Juma, na wengine watafuata huko baadae.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mhe. Said Ali Mbarouk.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hapa katika Baraza lako Tukufu kutekeleza yale ambayo tumetumwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, pili nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri, mwanana na yenye malengo mazuri katika sekta hii ya Habari, Utadamuni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuleta maendeleo kwenye Wizara hii, hususan sekta hii ya michezo, habari, utalii na utamaduni.

Mhe. Spika, nianze na Baraza la Sanaa ambalo lipo kwenye ukurasa wa 48 mpaka wa 50.
Mhe. Spika, Baraza la Sanaa lina kazi kubwa ya kusimamia kazi za sanaa nchini, kwani sanaa ndiyo kioo cha jamii.

Mhe. Spika, wasanii wengi Zanzibar wamepoteza malengo kwa sababu ya kutopata ushirikiano mkubwa kutoka katika Baraza la Sanaa. Vipaji vingi imebidi viishie kati kati katika mpango mzima wa kuendeleza sanaa Zanzibar.

Mhe. Spika, Zanzibar tumejaaliwa kuwa na vipaji vya aina mbali mbali vikiwemo hivi vya sanaa. Wasanii wetu wanaposhiriki katika maonesho mbali mbali ya kisanaa, basi huwa kivutio kikubwa ndani ya Tanzania yetu na nje ya Tanzania. Lakini yale matarajio yao au malengo yao yamekuwa yakifika mahali wanavunjika moyo kutokana na kutopata msaada mkubwa kutoka kwa Baraza la Sanaa. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba anafanya kazi ya ziada kuweza kuwasaidia wasanii wetu ili kufikia malengo na kuinua sekta hii ya sanaa kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, nije katika Baraza la Taifa la Michezo ambalo linaanzia ukurasa wa 51 hadi 53.

Mhe. Spika, kuna msemo unaosema wa Kiswahili hata waimbaji hawa wa sanaa ya kizazi kipya, ya muziki wa taarabu na munamkumbuka msanii Ngurumo alipoimba wimbo ule, akaimba nyimbo moja inayosema kwamba:-

"Ukiona mtu mzima analia, ujue kuna jambo".

Mhe. Spika, mtu mzima halii tu. Sasa toka jana Mhe. Spika, Wajumbe walipoanza kuchangia wameanza kulia na kilio cha Baraza la Michezo Zanzibar, ikiwa na sekta nzima hususan mchezo wa mpira wa miguu na michezo mengine.

Mhe. Spika, tuseme ukweli soka la Zanzibar lipo kaburini na sijui nani atakuja kulifufua.

Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ana malengo makubwa sana, na ana mipango mikubwa sana ya kuinua sekta ya michezo hususan *football*, lakini anakatishwa tamaa na Wazanzibari wamekatishwa tamaa na usimamizi na uendeshaji wa soka la Zanzibar.

Sasa mimi nimuulize Mhe. Waziri, tatizo lipo wapi. Tatizo lipo Wizarani, tatizo lipo kwenye Baraza la Michezo au tatizo lipo kwenye chama chenyewe. Nina imani kwamba yeye anajua jibu sahihi, kwa sababu ndiye aliyepewa dhamana ya kuendesha masuala ya michezo Zanzibar.
Mhe. Spika, tuseme ukweli tatizo ambalo linafanya michezo yetu kudorora ni kutokana na uongozi mbovu. Vipaji vipo, walimu tunao wazuri tu.

Mhe. Spika, Zanzibar imekuwa ikitoa vipaji mbali mbali vingi tu, na kuna wachezaji wengi ambao wamepata sifa kubwa hapa Zanzibar. Kuna wachezaji ambao wewe mwenyewe unawajua. Kuna Mzee Mkweche, kuna Nassor Mashoto, kuna Mzee Haroub (Baba yake Nadir Haroub Cannavaro), kuna Abdalla Maulid, akina Bausi hao; Salum Bausi na Seif Bausi, Mzee Majaham na Shaaban Ramadhan Kichwa.

Mhe. Spika, kule Pemba kulikuwa kuna wachezaji wenye vipaji kweli kweli, wako akina Eddy Abdalla walitoka kule, kuna Apali Othman, kuna Khamis Mafua, Ali Koresheni na Ridhaa Khamis.
Kwa hivyo ni kuonesha wazi kwamba Zanzibar tuna vipaji na wameleta sifa sana Zanzibar. Lakini katika miaka ya karibuni, sijui sifa hii imepotolea wapi. Tumebakia kuwa na migogoro, mara Mahakamani na hata Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kasema jana.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri mimi ninadhani ipo haja ya kuwakusanya angalau hawa wanamichezo walioleta sifa, na wapo wazee ambao wanajua suala hili, walianzia akina Marehemu Hija Saleh, vipo vizazi vya Hija Saleh hapa. Yupo Mzee Shamuhuna ndiyo, hivyo vipaji ambavyo viliandaliwa na Hija Saleh. Sasa sioni tatizo kuwa limefika wakati mpaka inakuwa ni aibu.

Mhe. Spika, ukiangalia kwenye kiambatanisho, nimeangalia hapa imetajwa vyama ambavyo vimefanya vizuri na vile vyama ambavyo vimekuwa haya tunakwenda tu. Nichukue fursa hii kukipongeza sana Chama cha Mchezo wa *Netball. Netball* ndiyo chama ambacho kinafanya vizuri katika mashindano mbali mbali, yakiwemo ya ndani na nje. Halikadhalika mchezo wa kuogelea, wanafanya vizuri. Wavu wanafanya vizuri.

Mhe. Spika, vipo viambatanisho hapa, riadha wanajitahidi lakini tatizo lipo kwenye Chama cha Mpira wa Miguu, tumebakia wasindikizaji tu. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri, na mimi nina imani kuna viongozi wazuri wa *ZFA*, siyo kama hakuna, wapo, na wapo wanamichezo pia, kwa sababu wote wengine wanatoka katika uongozi wa vilabu. Hata huyo Rais anatokea katika uongozi wa vilabu. Mimi nilikuwa nina imani naye sana huyu Rais wa *ZFA*. Sijui tatizo ni nini.
Kuna akina Hashim Salum ni kiongozi ambaye anayetoka katika michezo, ni kiongozi mzuri tu, alikuwa ni mchezaji mzuri tu, kiongozi mzuri. Lakini Mhe. Spika, tuangalie tatizo ni nini, "*Yaliyopita si ndwele tugange yajajo*". (*Makofi*).

Mhe. Spika, tumuunge mkono Mhe. Rais, ametujengea uwanja wa Amaan, uwanja unapendeza tunausifu, uwanja wa Pemba Gombani umejengwa uwanja mzuri tunausifu. Sasa hivi tunasifu uwanja wa Mao Tse Tung. Haya yote ni mambo mazuri yamefanywa kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa Mhe. Spika, tusifanye mambo ya kuua michezo hii kwa sababu zetu wenyewe ndani kwa ndani, kama kuna tatizo tuwasaidie. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nimepata taarifa kwamba hata wadhamini hatuna mara hii kutokana na matatizo yetu ya ndani, tuondoe tofauti zetu. Mheshimiwa ndiyo mwenye dhamana, likiharibika hili tutalia na wewe. Kama ni Baraza twambie, aah! tatizo lipo Baraza lakini tukiliacha hivi hatimaye vipaji vyetu vinapotea. Zanzibar tuna vipaji vingi sana.

Mhe. Spika, Zanzibar tumeshaleta makombe mengi huko wakati wa nyuma hapo. Timu yetu ya vijana imeshachukua kombe la *Copa Coca Cola* na Mhe. Ali Juma Shamuhuna shahidi, tumemkabidhi akiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, tulikukabidhi wewe kombe lile, mimi nikiwa ni Katibu wa *ZFA* na tulipata sifa kubwa mpaka Mhe. Rais wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete alisema hawa watoto wa Brazil ndogo, kutokana na vipaji ambavyo vimeoneshwa katika Uwanja wa Taifa, yale yote yamepotea. Kwa hivyo tuondoe matatizo. Nadhani kuungana kwa pamoja tuwaite wale wachezaji wa zamani ambao walileta sifa ili kuondoa matatizo yaliyopo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nije katika sekta ya habari. Mhe.Spika, wenzangu wamezungumza sana kuhusu sekta ya habari.

Mhe. Spika, kwa kweli ni aibu. Ulimwengu wa leo wa sayansi na teknolojia, taarifa ambazo zinazotokea ulimwenguni huko, leo sasa hivi likitokea tatizo tunaliona kutokana na wenzetu wanavyojipanga kununua vifaa vya kisasa, maandalizi mazuri, waandishi wazuri. Lakini leo ukienda *ZBC* utakuta kompyuta moja, ukienda chumba cha habari kompyuta moja. Hili ni tatizo.

Mhe. Spika, tusilaumu tu chombo cha *ZBC* kwa sababu sijui nini, hawana vifaa. Saa nyengine Mhe. Spika, kunakuwa na kazi hapa *camera* moja inachukuliwa inakwenda kwenye shughuli nyengine, humu ndani inatolewa kutokana na upungufu wa vifaa. Hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri tuiwezeshe *ZBC*.

Mhe. Spika, *ZBC* kuna tatizo hata la usafiri. Kuna wafanyakazi pale wanatoka saa sita za usiku, mara nyengine usafiri hamna. Tunapewa malalamiko na ni kweli. Sasa haya matatizo madogo madogo tuondoshe, tuwawezeshe *ZBC. (Makofi).*

Mhe. Spika, jengine wafanyakazi wapewe haki zao ikiwemo pesa zao za likizo, posho la kazi ya ziada ili waweze kufanya kazi kwa uzuri. Waandishi wa habari ni watu muhimu Mhe. Spika. Jamii inataka kupata habari, waliopo Pemba, waliopo Kengeja, waliopo Mwambe, waliopo Shamiani, waliopo Mtambwe Daya, wote wanataka habari. Kwa hivyo ni sekta muhimu hii.

Mhe. Spika,...

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri kuwa msikivu, yale ambayo Wajumbe wako wamezungumza ayafanyie kazi, ili kuinua suala zima la michezo, habari na mambo mengine.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi siungi mkono mpaka baada ya kupata maelezo kwa Waziri.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana. Ninaomba sasa nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma afuatie Mhe. Hija Hassan Hija wakati Mhe. Abdallah Mohammed Ali anajitayarisha.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii adhimu kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ambayo itaweza kunisaidia katika kuchangia Hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma ambaye ametuwezesha kufika hapa leo tukiwa na afya njema, kuweza kutimiza majukumu yetu ambayo wananchi wametutuma kuja kuyafanya.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wao wote, kwa kazi nzuri ambayo kwa kipindi chote cha mwaka 2014/2015 walizokuwa wakizifanya pamoja na hatimaye kutuwasilishia bajeti hii ya mwaka 2015/2016 katika kutupa mwanga na mwelekeo wa shughuli ambazo watazifanya kwa kipindi cha mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, mimi nianze kwenye kitabu kikubwa katika ukurasa wa 3 ambao umeelezea kwa ufupi mafanikio ya Wizara katika vipindi tofauti, kuanzia 2010 mpaka 2015.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 3 kwanza wamezungumzia suala zima la kuweza kuhamasisha uanzishwaji wa redio mbali mbali ambazo ni redio za binafsi zilizomo ndani ya jamii yetu.

Mhe. Spika, napenda sana kuipongeza Wizara kwa kuweza kuhamasisha redio saba ikiwemo redio mbali mbali za *FM* na nyengine nyingi, ambazo kwa kweli zimekuwa zikiwafikia wananchi kwa hali nzuri sana.

Mhe. Spika, nazipongeza redio hizi kwa sababu katika redio ambazo zinawafikia wananchi au jamii moja kwa moja ni hizi redio ambazo zimo ndani ya jamii zao. Pia redio hizi mara nyingi sana huwa zinazungumzia masuala mtambuka, kwa maana kwamba yale yote ambayo yanawagusa moja kwa moja wananchi redio hizi zimekuwa zikifanya kazi hizo, na kuzi-*adress* na ndio lengo la kuwa na redio hizi,

kwamba kuwafundisha, kuwaelimisha pamoja na kuburudisha, lakini kuburudisha na kuelimisha jamii ambayo inahusika katika maeneo yale.

Mhe. Spika, mimi nazipongeza sana redio hizi, kwa sababu ni redio ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kuzungumzia suala la udhalilishaji wa kijinsia na watoto.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu nimeshakutana na waandishi mbali mbali wanaotokana na redio hizi, wakija kutuuliza maswali mbali mbali yanayohusiana na suala la udhalilishaji wa wanawake pamoja na watoto. Vile vile kutuhamasisha kinamama katika masuala mbali mbali yakiwemo masuala ya kisiasa na kiuchumi. Nawapongeza sana tena sana kwa kuielimisha jamii.

Mhe. Spika, pia ningeiomba wizara, kwa sababu redio hizi zinahitaji motisha na redio hizi ni moja katika msaidizi mkuu wa kuelimisha jamii. Hivyo basi ili kuzipa motisha redio hizi za jamii, sasa tuanzishe utaratibu maalum ambao utawawezesha na utawapa hamu ya kufanya kazi katika masuala mtambuka mbali mbali, kwa kuwapa tunzo maalum inayohusiana na masuala ya kuwafikia jamii katika masuala mtambuka, likiwemo suala zima la kulizungumzia suala la udhalilishaji wa wanawake na watoto. Hiyo itatoa ari na itatoa motisha ya kufanya redio hizi za jamii ziendelee kuzungumzia masuala hayo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba sana kwamba redio hizi za jamii muzione katika hali hiyo, ili na sisi wananchi tuweze kufaidika na masuala mbali mbali, yakiwemo masuala ya haki za mwananchi, pamoja na fursa ambazo zinaweza kutolewa ndani ya Serikali.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulipongeza sana Shirika la Utangazaji ambalo wameona muelekeo sasa wa kuanza kutanua wigo wa kuonekana katika mataifa ya Afrika ya Mashariki, pamoja na nchi nyengine za Kiafrika.

Mhe. Spika, mimi sina wasi wasi na hilo, na nikiliona hili linafanyika kwamba sasa *channel* za Zanzibar zinaonekana katika mataifa mengine. Lakini ni fursa ya pekee kwa sababu kwanza Zanzibar utamaduni wake ni tajiri mno. Lakini jengine ni kwamba tuna fursa, kwa sababu Zanzibar ndio kituo kikubwa cha lugha ya Kiswahili.

Mhe. Spika, nasema maneno haya kwa sababu nina kumbukumbu nzuri ingawa sijui hatua gani tumefikia.

Mhe. Spika, Zanzibar hata katika Afrika ya Mashariki ilichaguliwa kuwa ndio kituo kikubwa cha lugha ya Kiswahili na wengine wote waje kusoma hapa

Zanzibar. Kwa hivyo, ni mfano mzuri kabisa ikiwa tutaanzisha huu utaratibu wa kuweza kuonekana nje ili basi tueleweke Zanzibar, kama Zanzibar kimataifa. Utajiri wa lugha ya Kiswahili uonekane uko hapa. Kwa sababu wenzetu wengine hili wanalionea choyo, hii wanaona ni fursa kubwa ya Zanzibar, kwamba Kiswahili sisi ndio lugha yetu peke yetu ambayo tunaitumia na ni tajiri kwenye lugha hii.

Kwa hivyo, mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri kwanza tufanye utafiti wa kutosha wa kuweza kufikisha basi hizo *channels* katika mataifa mengine, kwa maana kwanza tuwe na ubora wa vipindi vyetu vya Kiswahili, lakini tuwe na ubora wa matukio mbali mbali ambayo yanatokea ambayo tunataka kuyarusha katika mataifa mengine.

Mhe. Waziri ningekuomba sana tujitayarishe vizuri. Pia tunapojitayarisha basi tujue kwamba watu wengi nje wanajifunza Kiswahili kutoka kwetu. Hivyo, nakuomba sana kama ulivyoahidi mwenyewe katika kitabu cha bajeti, kwamba kutakuwa katika mfumo wa *satellite* kutaiwezesha Zanzibar kuonekana katika nchi zote za Afrika ya Mashariki na Kati, lakini ni njia pekee nzuri vile vile ambayo itasaidia katika kukuza utalii wetu.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba Zanzibar ni moja katika kituo cha utalii kwa Afrika ya Mashariki, na watalii wengi hutembelea kuanza katika nchi nyengine, kwa mfano Kenya wakapita Tanzania Bara kisha wakaja Zanzibar. Hivyo itakuwa na nafasi nzuri ya kuweza kujitangaza ndani ya televisheni zetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningeomba tujipange vizuri ili kuhakikisha kwamba matangazo hayo au vipindi hivyo vya televisheni vitaleta tija katika Taifa letu.

Mhe. Spika, pia niipongeze sana wizara kwa kuweza kufanya utafiti wa uchimbaji wa Ngome ya Mazrui.

Mhe. Waziri kwa mujibu wa kitabu chako ukurasa wa 5 unasema kwamba kwa udhamini wa "*African Archaeology Network"* imeweza kuvumbua na kuchimbua vifaa mbali mbali vya ufinyanzi zilivyofinyangwa ambavyo vinatoka katika karne ya kwanza na vinatokana na watu waliokuwa wanaishi katika wakati huo.

Mhe. Waziri mimi nipongeze sana kwamba tumepata historia ndani ya utafitu huo. Historia Mhe. Spika, ndio inayotujenga wanadamu. Ndani ya maisha yetu ya kila siku Mhe. Spika, yanaonesha au yanatoa mwanga wa kumuona huyu mtu ametoka katika mazingira gani. Kwa hivyo, historia ina umuhimu sana, na kama hatutoitafuta historia yetu basi hatutoweza kuipata. Lakini kama hatutoweza kuithamini hatutoweza kuendelea. Vile vile kama hatutoifanya tukarithisha vizazi

vyetu vijavyo tutakwamisha maendeleo ya vizazi vinavyokuja. Kwa hivyo, mimi niipongeze sana wizara kwa kuweza kufanya utafiti huu na kuweza kugundua.

Mhe. Spika, ningeiomba sana wizara, na ningemuomba waziri kwa uwezo wao, kuna uwezekano mkubwa baada ya kuvipata vitu kama hivyo, sasa tukaanza kutengeneza maumbo ambayo yatalingana na vile vitu vyenyewe. Kwa sababu tunaweza kusema kwamba vile vitu vimepatikana vipande vipande, lakini bado vikiunganishwa au bado vikifanyiwa kazi ikiwa katika picha au katika muundo kama ule, lakini bado vile vitakuwa vinatoa picha ya watu ambao wameishi katika karne hiyo.

Mhe. Spika, hiyo ni kazi kubwa na wengine wenzetu wanaifanya katika mataifa mengine. Tutafute historia na kuweza kuibua yale mambo ambayo watu wa zamani waliishi katika mfumo huo.

Mhe. Spika, kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri baada ya utafiti waweze kujua vipi wataweza kuiweka hiyo historia, hilo ni muhimu sana.

Mhe. Spika, mimi nataka kwenda kwenye kitabu hiki kidogo ambacho kina taarifa ya utekelezaji wa programu ya Maabara ya Utalii katika mwaka 2014 na 2015.

Kwanza niipongeze sana serikali kwa hatua ambayo imechukua ya kuanzisha programu hii ambayo itaweza kusaidia katika kuendeleza utalii.

Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba programu hii ya kufanya utafiti inalenga katika kuhakikisha kwamba utalii itakuwa ni sekta ya kwanza katika kuleta mapato ndani ya nchi. Lakini sio sekta ambayo itakuwa inadhalilisha utu wetu, lakini itakuwa ni sekta ambayo itatuletea manufaa katika Taifa letu hasa ya kiuchumi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa kwanza inazungumzia suala la bidhaa za utalii na huduma.

Mhe. Spika, mimi nipongeze sana kwamba katika utafiti wake wameweza kujipanga na kutoa kipaumbele katika masuala mbali mbali, lakini la mwanzo kabisa wameweka bidhaa za utalii na huduma.

Mhe. Spika, jambo moja ambalo mimi nalifahamu ni kwamba bidhaa nyingi za utalii ambazo zinauzwa katika maeneo mbali mbali zinatengenezwa na akinamama. Wanawake ndio wasarifu wakubwa wa kutengeneza bidhaa za kitalii na wengi wao wanaishi kwa pato hilo la utalii.

Mhe. Spika, katika lengo hili la mwanzo kabisa tuhakikishe tunawasaidia akinamama kwa ajili ya kuongeza ubora wa bidhaa zao. Kwa kuwa tumebahatika kwenda katika mataifa mbali mbali na tumeona ubora wa kazi za wenzetu, ambapo ni jambo muhimu sana. Hakuna mtalii ambaye anataka kuja kununua kitu ambacho hakina ubora, kwa sababu pengine atakuja hapa mara moja akiondoka anataka bidhaa ya Zanzibar idumu katika nyumba yake au katika roho yake kwa muda mrefu, lakini bidhaa ile iwe nzuri.

Mimi naomba sana kwamba katika kitu ambacho kimefikiriwa na ni cha muhimu sana ni suala zima la bidhaa za kitalii, litiliwe mkazo wa kuwawezesha hasa akinamama katika kutengeneza ubora wa bidhaa hizo.

Mhe. Spika, kinamama wamekuwa wakitengeneza sabuni nzuri sana, sabuni zinazotumia viungo vya Zanzibar, tunakiita kisiwa cha Zanzibar "*Spice Island"* ni moja katika *brand* ya kutangaza utalii kwamba Zanzibar ni "*Spice Island"*.

Sabuni zile kwa bahati mbaya sana bado hazijaingia katika soko la mahoteli yetu, na hakuna kitu kikubwa sana ambacho kinahitajika, zaidi ya kuwawezesha wale wajasiriamali wadogo wadogo wanaotengeneza zile sabuni, kutengeneza kwa wingi ambao unatakiwa katika mahoteli yetu. La pili lakini ni kujua kama soko lipo, hilo ni muhimu sana.

Mhe. Spika, unatizama saa, lakini bado sijafika mbali. Lakini lazima tuhakikishe katika utafiti wetu kwamba wananchi wanafaidika. Na tunajua kwamba tunapomuwezesha mama ina maana tumeiwezesha jamii, na hilo nashukuru sana kwamba kina baba pia wanafahamu. Kwa sababu mara nyingi mama akitoka huko anakotoka kutafuta baba yuko mlangoni anamuuliza umepata ngapi, hakai mbali na mama hata kidogo. Ndio kwa sababu tunasaidiana.

Mhe. Spika, tunasaidiana siku hizi, maisha siku hizi ni kusaidiana na kinamama wako tayari kabisa. Kwa hivyo, ningeiomba sana wizara kusimamia hili, ili kuhakikisha kwamba nao kinamama wanafaidika katika suala zima la kukuza uchumi wake hasa katika sekta ya utalii.
Mhe. Spika, moja ambalo nimeliona ni changamoto katika programu hii ya Maabara ya Utalii ni fedha.

Mhe. Spika, fedha wanazotiliwa ni ndogo, tunapanga makubwa lakini utekelezaji unakuwa mgumu kwa sababu ya fedha. Katika sehemu nyengine unaona fedha wametiliwa kwa mfano ukurasa wa 2 fedha zilizoingia ni asilimia 8.52.

Mhe. Spika: Unazo dakika 5.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, vile vile katika maeneo mengine kuna asilimia 25 tu. Sasa sisi tunaweza tukawakaba hawa wenzetu watendaji, lakini ukweli ndio huo.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuwaambia kwamba katika nchi zote wenzetu suala la kutafuta masoko na kuitangaza nchi ni muhimu sana. Kwa sababu huwezi ku-*invest* kama hujatumia fedha zako mwenyewe.Sasa tu-*invest* kwenye utalii, tuhakikishe tunatoa huduma bora ndani ya utalii, tumejipanga vizuri kabisa.

Mimi sitaki kutoa dosari ya aina yoyote ndani ya vitabu hivi kabisa, kwa sababu hakuna dosari hapa, isipokuwa tunachokitaka ni suala zima la kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana, na kwa sababu uchumi wetu, fedha zetu zinatokana na utalii basi tuwekeze huko huko kwa uwezo wetu.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ambalo nataka kulizungumza, hili naomba sana wizara yako Mhe. Waziri na hasa katika *ZBC* Televisheni.

Mhe. Waziri nimepata malalamiko mengi sana, kuhusiana na *ZBC* hasa katika kuendeshwa katika vipindi mbali mbali, hasa taasisi zisizo za kiserikali, ambapo wengi wanapata fedha zao kutoka katika mashirika ya kimaendeleo. Tunapotaka kupeleka vipindi pale, pesa ni nyingi mno, wanataka kwenda kuzungumzia masuala ya udhalilishaji wa mwanamke na mtoto, lakini wanaambiwa watoe pesa nyingi. Kwa hivyo, haya ni masuala mtambuka, haya ni masuala ambayo sasa hivi yanatuathiri sana, tutayapeleka wapi na wadau wa maendeleo hawataki kutoa pesa nyingi, kwa sababu haya mambo ni ya kwetu sisi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri tusaidie, kwa sababu saa nyengine mimi hujiuliza, na wengi wanajiuliza hasa hizi asasi za kiraia, inapowekwa picha au mchezo ambao kwa kweli hauna tija yoyote, lakini tupeleke mambo ambayo yanahusu jamii, sasa huyu hapewi. Inawekwa filamu tu ambayo haina maana. Hii Televisheni na Redio tumeambiwa ni kwa ajili ya kuelimisha na kutoa taarifa na kustarehesha, lakini starehe isizidi zaidi ya elimu. Kwa sababu yako mashirika mengine *private* yanatustarehesha sana, yanatuburudisha sana, sasa tunataka sisi hii iwe inaelimisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri mimi kwa kipindi kirefu sana sijaona kipindi kinachofundisha mapishi katika Televisheni ya Zanzibar, na kwa sababu pengine labda hakuna mtu ambaye atakwenda kufundisha mapishi pale akatoa pesa, lakini hii ni kazi yenu. Tunasema maadili, utamaduni mapishi ni utamaduni pia wa Mzanzibari.

Sisi tuna mapishi maalum ambayo sehemu nyengine hayapo, tutangaze mambo yetu. Mhe. Waziri hilo ni muhimu. Hebu tutafakari ni vitu gani ambavyo tunataka

kuvionesha kwenye Televisheni sio ngoma tu, ngoma tuwaachie wengine huku twende kwenye masuala ya kuelimisha Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nafikiria hilo ni muhimu, lakini nikupongeze kwenye masuala ya michezo Mhe. Waziri umejipanga vizuri. Kwenye masuala ya sanaa nimeona kwamba kazi ni nzuri lakini tuboreshe vikundi vyetu, vikundi vyetu vimekuwa havina nguo nzuri ambazo kwa kweli zinaonesha asili yetu, bado tunajifananisha Mhe. Waziri, kwa bahati tunapata nafasi ya kutembea tembea na tunaona wenzetu ngoma zao za kitamaduni zinavyokuwa, tuwe na ngoma zetu zile zile za asili, lakini tu- *modernize* vitu vingine ndio raha ya hizo burudani.

Aidha tuwape motisha wale wanaofanya ile kazi ya kucheza ile ngoma, saa nyengine kwa sababu ya ule utashi wao na mapenzi yao tuwaenzi wale ambao wanashiriki katika masuala ya sanaa.

Mhe. Spika, ni mengi sana ambayo nilikuwa nafikiria kuyazungumza vile vile lakini ningemalizia hapa isipokuwa namtakia kila la kheri Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote.

Naipongeza sana Serikali kwa hatua ambazo tumefikia na tuko pazuri lakini tunataka usimamizi mzuri, usimamizi Mhe. Waziri ni kwako pamoja na Naibu wako na Watendaji wako wengine wakuu, kwa sababu tunapoacha kusimamia ndio mambo yanaharibika, lakini vile vile fedha zinatakiwa zipitishwe katika maeneo mbali mbali hiyo ni changamoto, lakini Mungu atasaidia tutatoka huko.

Basi niwaombe wenzangu tuipitishe bajeti hii kwa sababu ni bajeti ambayo ina muelekeo mzuri, na tumpe basi nafasi Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake waweze sasa kufanya yale ambayo wamependekeza.

Baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana Mhe. Spika, naunga mkono bajeti kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na kwanza niseme kwamba kidogo hali yangu si nzuri nitakaposhindwa kuendelea nitaondoka bila ya kukuaga univumilie.

Mimi nianze kwa kusema kwamba siungi mkono hotuba hii, na siungi mkono kwa sababu moja tu haiwezekani watu wenye akili timamu miaka mitano wanazungumzia maslahi ya wafanyakazi wasiozidi saba ikiwa hatuna majibu ya Serikali.

Baraza hili miaka mitano tunazungumzia maslahi ya watu wa *camera* humu ndani miaka mitano, na Serikali imekuwa ikitujibu kwamba tutawafanyia hadi hii leo mwaka wa tano bado siku sita saba kuvunja Baraza hakuna majibu, baadae mtu anakuja hapa anasema Wizara hii nzuri inafanya kazi, si kweli, na mimi siungi mkono hii hotuba.

Haiwezekani kwamba watu wazima wanakaa miaka mitano hapa kuzungumzia maslahi ya wafanyakazi wasiozidi saba, na wala sio mamilioni ni shilingi elfu tano tano tu, Wizara inashindwa kuwatekelezea wenzetu hawa badala yake hapa mtu akiapa hapa anasema bajeti nzuri hii nzuri maana yake inafanya vizuri si kweli. Mhe. Spika, huo ndio utangulizi wangu wa mwanzo siungi mkono na nina sababu hizo za msingi kabisa.

Mhe. Spika, jambo la pili niende kwenye jadweli namba mbili, jinsi Wizara ambavyo imesomesha wafanyakazi wake, kwa jinsi ambavyo wameandika Mhe. Spika, Wizara imesomesha wafanyakazi 61 lakini ukihesabu ni 58 kuna *printing error* pale sio 61. Kwa hivyo ukiangalia viwango walivyosomesha wenzetu hawa ngazi ya cheti wamesomesha watu 6 kwa asilimia 10.34%, ngazi ya Stashahada (*Diploma)* imesomesha wafanyakazi 25 kwa asilimia 45.01%. Shahada ya kwanza ni watu 17 asilimia 29.3%, Shahada ya Pili ni watu 10 asilimia 17%.

Kwa hivyo ukiangalia Mawizara mbali mbali, Wizara ya Habari na Utamaduni imesomesha wafanyakazi wengi. Lakini kusomesha ni hatua moja na maslahi ni hatua ya pili. Kwa hivyo kwa msingi wa kusomesha wafanyakazi wake Wizara hii Mhe. Spika, imesomesha wafanyakazi wengi ukilinganisha na Wizara nyengine, lakini Je, waliosomeshwa wamelipiwa, wamekopwa, kwa hivyo hiyo ni hoja ambayo nataka Mhe. Waziri atueleze, hadi hii leo malalamiko ya wafanyakazi mbali mbali wa wizara yake yapo, na ndio nimesema pale kwamba miaka mitano Baraza hili limeshindwa kuwajibisha Wizara kutoa mafao ya wafanyakazi ambao wametumikia chombo hiki naona tumetumia Serikali.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hoja yangu hapa kwa Mhe. Waziri naomba unisaidie malimbikizo au *arrears* ya miezi sita ya wafanyakazi wa *ZBC TV* na Redio ambayo walichukua zaidi ya miaka mitatu nyuma hakuna hatua. Hilo Mhe. Waziri, ingelikuwa wewe na mimi mtu anakufanyia hivyo ungeridhika, mtu ajiulize kama mimi ningelikuwa nafanyiwa mimi ningeridhika.

Kwa hivyo malimbikizo haya ya wafanyakazi wetu ya miezi sita naomba yalipwe, na kwa sababu bajeti ndio inamalizika mwezi huu, na kwa tabia yenu ya kutudanganya Mhe. Spika, maana yake hiyo ndio imekwenda, kwa hivyo kabla ya kuja hapa leo kupitisha vifungu jioni ulipe hizi pesa za *arrears* za wafanyakazi hawa, kwa sababu tukitoka hapo Mhe. Spika, niwaambieni hawa hawalipwi tena.

Hii ilivyokuwa miaka minne imeshindikana, sidhani na siku moja ya leo kwa ahadi zenu mutawalipa watu, kwa hivyo nikuombe Mhe. Waziri umwambie Katibu Mkuu wako ahangaike huko nje atafute fedha za wafanyakazi wetu hawa *arrears* naamini sio nyingi mnazo, mna uwezo lakini dharau ya wafanyakazi wetu. Mhe. Spika, nikuombe sana kwamba hawa watu walipwe.

Mhe. Spika, ukienda kwenye msingi wa fedha jadweli namba moja.

Mhe. Spika, nianze kutoa mifano ya baadhi ya Idara Shirika la *ZBC* fedha ya mishahara iliyotengwa ni bilioni 1.24 lakini *O/C* iliyotengwa ni Milioni 313. Maana yake unalipa mishahara bilioni 1.3 lakini unawapa theluthi ya fedha ndio wafanyie kazi, maana yake umealika harusi ya watu elfu kumi lakini una polo ya mchele, haiwezekani kwamba unatoa mshahara mara sita ya fedha za *O/C.* Kwa tafsiri nyengine *ZBC* ni chaka la kulipana mishahara, kwa maana kwamba kuna fedha za mishahara kubwa bilioni 1.3 lakini fedha ya kazi hiyo ya mshahara haipo.

Sasa hivi tutafikia wapi maendeleo? Ikiwa watu wanalipana mshahara mkubwa kwa maana ya 1.3 bilioni lakini *O/C* ni milioni 300, ni theluthi moja ya ile fedha bado mtwambie kuna kazi hapa, na ndio maana mafao ya hawa wafanyakazi wetu hamuwalipi kwa kuwa hamna fedha ya *O/C* ya kuwalipa wafanyakazi wetu.

Mhe. Spika, Idara ya Habari Maelezo mishahara ya Shilingi milioni 235.9 lakini *OC* ni milioni 85 iliyopatikana ni milioni 28, eti Idara hii ndio ifanye kazi, kwa hiyo ni Idara ya kulipana mishahara tu.
Mhe. Spika, Idara nyengine ni Chuo cha Uandishi wa Habari chuo muhimu sana, mishahara ni 202 milioni lakini *OC* ya kuendesha Chuo ni milioni 35, hii mliona wapi? Mliona wapi mambo haya kila siku mko China, Uholanzi, Uturuki, muliona wapi mambo haya kwamba ulipe mshahara milioni 500 lakini hiyo kazi yenyewe milioni 30 mliona wapi?
Mhe. Spika, Idara nyengine ni Tume ya Utangazaji. Mishahara 146,400,000/= *OC* ni milioni 50 lakini hapa nashukuru mliwapa milioni 44, kazi haifanyiki, mishahara sio kazi mshahara ni malipo, kazi ni *O/C.*

Mhe. Spika, Chuo cha Maendeleo ya Utalii mshahara ni Shs. 370,000,000/= lakini *O/C* ya kufanyia kazi Chuoni ni 44,000,000/= muliona wapi? Mhe. Spika, Serikali ielewe mishahara ni haki ya wafanyakazi *O/C* ndio kazi yenyewe.

Mhe. Spika, jengine Shirika la Utangazaji Pemba ni 144,000,000/= mshahara lakini kazi yenyewe ya Pemba nzima 41,000,000/= na iliyopatikana 34,000,000/= lakini jambo la ajabu Mhe. Spika, ni Idara moja tu, na hii niipongeze sana Kamisheni ya Utalii hii mshahara 554,000,000/= *O/C* 834,000,000/= hapa unaona kwamba kuna

kazi inafanywa, kwa maana fedha ya kazi kubwa kuliko mshahara 834,000,000/= ndio *O/C* 442,000,000/= ndio mishahara, unaona kwamba hapa kuna kazi zinafanywa lakini sehemu nyengine zote zinalipwa mishahara tu.

Mhe. Spika, mwaka jana niliwaambia hapa kwamba nyinyi mnatufanyia mzaha mmeandaa Maabara ya Utalii (*Tourism Lab)* angalieni fedha ambayo ilikusudiwa na fedha iliyopatikana.

Mhe. Spika, mambo yenye utalii Mhe. Spika, uhifadhi wa maeneo ya historia na maeneo ya kale Serikali ilitenga milioni 150 iliyopatikana milioni 41, asilimia 28% ndio mnahifadhi maeneo ya kale yote Unguja na Pemba.

Mradi wa Maabara ya Utalii ambao huu ndio unaongeza pato la nchi. Utalii una sehemu kubwa ya pato la nchi, Serikali ilitenga na wakaja hapa tukapitisha fedha bilioni 5.6 maabara ya utalii yaongeze fedha za utalii Serikali imetoa milioni 476, asilimia tisa (9%), ni aibu kubwa! Bilioni 5.6 Serikali imetoa 476 asilimia 9 mkatembea Unguja na Pemba munawaambia utalii kwa wote mukala fedha za umma kwa sababu ya utalii kwa wote. Wanatudanganya kiasi hichi, bilioni tano mnatoa milioni mia nne, asilimia tisa, (9%), mna hakika fedha mliotembelea Pemba na Unguja ilikuwa kubwa kuliko hiyo *O/C,* ni aibu.

Mhe. Spika, ujenzi wa Vituo vya Kutoa Taarifa za Usalama wa Watalii. Watalii wanahitaji kupata taarifa muhimu kwa usalama wao, Serikali ilitenga milioni 250 mukatoa milioni 80 (asilimia 32).

Mwisho Mhe. Spika, bilioni 5.6 za mradi mzima Serikali itoe milioni 528, asilimia kumi ya fedha za maendeleo. Hivi ukiangalia fedha ya maendeleo na mishahara na *O/C* hii Wizara ni ya kulipa mishahara tu, hakuna kazi, huwezi kutoa bilioni 4 za mishahara lakini kazi za maendeleo ni asilimia 10, milioni 500 ni hesabu gani jamani hiyo Mhe. Spika, hii hesabu si ya kurudi nyuma.

Mhe. Spika, nadhani niseme tu kwamba bajeti wanaopitisha na wapitishe, lakini ni bajeti ya kutoa mishahara hakuna maendeleo yanayoendelea.

Lakini sishangai Mhe. Spika, na hapa ndio inakuja hoja yangu *ZBC* ni chaka tu la kufanya mambo yanayofanywa. Na Mhe. Waziri unajua kuna orodha hapa ya wafanyakazi ambao mmewahamisha, *ZBC* ni Shirika, chini ya Bodi huwezi kuchukua maamuzi bila ya idhini ya Bodi. Kuna orodha mmewahamisha watu bila ya Bodi kujua, na kama Bodi inajua leo Mheshimiwa Waziri sema hapa kama Bodi inajua. Wewe unahamisha wafanyakazi 22 kwa utashi tu bila ya Bodi kujua ni kuvunja kanuni, kuvunja sheria na mnafanya haya yanajulikana halafu mnatwambia maana yake *ZBC* nzuri, maana yake ving'amuzi vizuri, si kweli!

Mhe. Spika, kuna wafanyakazi mliowafukuza kazi Bwawani 2011 wafanyakazi 11 ninayo orodha yao hapa. Bahati mbaya mmewafukuza kwa sababu wameghushi vyeti vya elimu, ni *right* lakini wengine mnawachukua kwa mlango wa nyuma wakati mnajua kwamba sifa ilikuwa ni moja, baadae mnawapa majukumu *ZBC*, baadae Mhe. Bhaa atwambie *ZBC* nzuri kuliko *Channel Ten*, si kweli watu wana viwango!

Mhe. Spika, Mhe. Waziri anijibu kwa nini *ZBC* ikatoa barua ya kuondosha wafanyakazi. Tena wanakiri Mhe. Spika, wanakiri hoja yangu, wanakiri kabisa. Kuwasilisha orodha ya majina ya wafanyakazi wa sehemu ya utawala ambao hawana kazi maalum, maana yake mnaweka watu tu wanalipwa mshahara, haya maandishi yenu Mhe. Spika, haya maandishi yenu, mnakiri kwamba kumbe kuna watu hawana kazi maalum wapo tu mnapewa hidaya kwa fedha ya umma, huku Wizara nyengine hawana fedha nyinyi mnatoa hidaya. Mna watu 22 kwenye Idara moja hawana kazi maalum wamekaa tu.

Mhe. Spika, nikwambie leo sitaji jina lakini mnatoa watu kwamba hawana viwango vya elimu vya kutosha ni *right* kabisa, lakini kuna watu mmewabakisha na wameghushi vyeti, kwa hivyo unapotoa *treatment* kwa mtu A na mtu B basi utoe *treatment* kama hiyo, kuna watu wameghushi vyeti mumewaachia wengine mumewaondosha kwa nini? *Why?*

Mhe. Waziri nitakuletea kopi hizi lakini unipe majibu leo, kwa nini mtu A unamuondosha kazini; watu kumi na moja wameondoshwa kazini wameghushi vyeti, lakini mtu B unamlinda halafu utwambie kwamba unafanya vizuri *ZBC* itakuwa haiwezekani!

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mimi ambaye *form four* nimeghushi namsimamia mtu mwenye *degree* nyinyi mliona wapi? Mimi nimeghushi cheti cha *Form IV* lakini nakusimamia wewe mwenye *Masters* mliona wapi mambo hayo au ndio mafunzo ya China hayo?

Mhe. Spika, nipate jibu na hizi ndio hoja zangu ambazo hotuba hii haina haja ya kupitishwa, tuwaachie mfanye mtakalo lakini mimi sitotoa mchango wa kupitisha mambo ambayo wafanyakazi wenyewe mnawadhalilisha, unawafanyia *harassment* wafanyakazi 22 bila ya hoja, bila ya sababu, halafu unakuja hapa unaomba tukupe bilioni kumi ukaendeleze mambo yako, hatuwezi kufanya hilo kosa, lazima fedha yetu itolewe kwa maslahi ya wafanyakazi wetu na Serikali yetu, hatuwezi kutoa fedha kwa ajili ya watu kuhujumiana.

Mhe. Spika, aliye-*forge* cheti lazima aangaliwe, ashughulikiwe, ili *ZBC* iende vizuri na msipochukua hatua sidhani kama miezi mitatu mingi uchaguzi mwezi wa Oktoba tutakuja hapa mwakani tukijaaliwa, lakini lazima mchukue hatua kwa misingi ya utawala bora.

Mhe. Spika, baada ya hoja zangu hizo nitahitaji majibu ya Malipo ya wafanyakazi wetu, na kwa nini mnaruhusu watu wanaghushhi vyeti wengine mnawaadhibu hatimaye mnawapa vyeo. Nasikia hivi karibuni mmekwenda China huku mmeghushi vyeti, mnakwenda China nendeni tu, China nendeni tu si mnafukuza wafanyakazi!

Mhe. Spika, nakushukuru siungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kupata fursa asubuhi hii kusema machache. Sitaki niseme sana, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, kusema kweli tumeshaongoza Wizara, tumeshaomba, imeshakosoa lakini kama alivyosema Mjumbe mwenzangu aliyepita sijui tulikuwa na masikio gani maana kusikia hatusikiani, isipokuwa tu kuna baadhi ya mambo kidogo nataka niyaweke wazi.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kuhusu hii *Tourism Lab;* Maabara ya Utalii. Na nina imani kwamba Serikali ilikuwa na nia nzuri sana ya kuja na chumba sasa cha kufanyia uchunguzi wa maradhi yetu. Lakini nasikitika kwamba chumba hichi kama tulikihesabu ni hospitali ya kuweza kupima maradhi yetu na kujua tuko vipi hakikupatiwa vifaa vya kufanyia kazi. Kwa hiyo kazi itakuwa ni pale pale tu.

Mhe. Spika, wizara hii imebeba moja kati ya nguzo kuu za uchumi, nayo ni utalii. Kitengo hichi kilitengenezwa hasa kwa kuangalia huu utalii iko vipi, na tufanye nini ili kuona kwamba utalii wetu unadumu na unaongezeka na unatuletea faida. Ili iendelee kuwa ni nguzo ya uchumi wetu. Serikali ikaamua kwamba *okay*, tuweke kitengo hichi, lakini nahisi hatukuamua kwamba sasa kama tunaunda hapa *priority* iwe ni nini.

Mheshimiwa kwa masikitiko wameidhinishiwa hawa bilioni 500 na *something*, lakini matokeo yake ripoti inasema kwamba wamepata asilimia 8.5. Na hapa ndio tunaposema ndio nguzo ya uchumi. Hivyo kweli Serikali ilikuwa ina nia ya kuunda chombo hichi ili kiweze kufanya kazi na huo utalii uwe ni wenye tija kwetu. Ukiangalia hizo fedha zilizopatikana utakuta zimekwenda kununua kompyuta, kutafuta mshauri muelekezi na kutafuta wataalamu. Hakuna fedha iliyotumika hasa kwa kuona jambo hili lifanywe ili kuongeza hiyo tija ya utalii. Ukiangalia unaambiwa kwamba moja katika kazi zake kuibua vivutio katika visiwa vidogo vidogo.

Mimi ninavyofahamu mtalii atakapokuja hapa kwanza anahitaji huduma, na huduma zinazohitajika ni pale ambapo keshagundulika kwamba hicho kivutio, kama huko kuna pango Kiwengwa. Kama kuna mto huko, kama kuna mbuyu basi huo mbuyu uwe huyo mtalii aufike. Sasa leo utakutia kuna mapango ambayo wameshayaona sawa, lakini yanafikika?

Sasa mawazo yangu mimi ilikuwa hii *Tourism Lab*, kipaumbele cha kwanza basi waangalie miundombinu ya kufika huko ili huyu atakayekuja kuangalia apate fursa ya kufika. Lakini leo ukienda yote yapo msituni.

Mimi mawazo yangu kwamba *Tourism Lab* ingetumika kuona vipaumbele vya mwanzo ni kupeleka huduma katika hizo sehemu ambazo mtalii akishakufika tunataka akaone.

Leo ukienda huko Pangawatoro unakuta hata mtalii akifika kama kaja na mtoto wake basi atamuweka mjini yeye hawezi kufika, kwa sababu barabara hakuna, maji hakuna, umeme hakuna, sasa mtalii huyo tutamu-*encourage* namna gani ili yeye aweze kufika hapa.

Mhe. Spika nafikiri hatupo *serious*. Kwa sababu hizi fedha sijui milioni 400 zilizopatikana zote Semina elekezi, sijui mafunzo gani, mzungu yanamuhusu na nini au mtalii yanamuhusu na nini yeye, ufuatiliaji sijui tufuatilie nini. Hamna, hatukuangalia *priority* tunahitaji miundombinu ya kufanya mtalii aje. Lakini leo unakwenda kijijini huko, unakwenda huko kwenye visiwa hupati maji, hupati umeme, sijui utakwenda vipi. Kweli atakuja akiona kwamba kuna upepo wa Kaskazi pale hawezi kuingia katika kiboti kilichokuwepo pale.
Sasa hizi fedha mimi nashauri mara nyengine Mhe. Waziri basi zipelekwe katika zile huduma muhimu sio kwenda kununua karatasi za *photocopy*. Hivi wazungu watabakia huko huko watatafuta sehemu nyengine watakwenda, lakini kwa kusema wanakuja hapa hawaji, hilo moja.

Lakini la pili Mheshimiwa kama tulivyosema *"duka lililofungwa mteja haji,"* ataona pale pamefungwa. Leo Kamisheni ya Utalii ndiyo tuliyoipa jukumu la kuutangaza Utalii wetu, lakini nashangaa kwamba inapofika wakati kwamba kuna maonesho ya Utalii ulimwenguni ili na wao waende wakajulikane kwamba kuna kijisiwa kinaitwa Zanzibar basi kwanza watafutane, wamtafute Katibu Mkuu kuna fungu huko? Ah! hakuna kitu. Sasa tutakwenda vipi, basi tukopeshane. Sasa huo utalii unafanywa hivyo Mheshimiwa. Twende tunajifunza, waliokwenda China wameona hao, mimi sijafika. Mhe. Spika sijui kama kuna safari na mimi nipate japo moja nikaone, lakini nimekwenda nchi nyengine *Alhamdulillah* nimetembea nimeona jinsi gani wanavyoutangaza.

Nimewahi kushiriki maonesho Ufaransa, nimewahi kushiriki maonesho Uingereza, Ujerumani, yote nimeona, lakini ukienda unauliza banda la Tanzania liko wapi? Hamna kitu. Sisi tunamsubiri bahati mbaya tu mtalii akae huko aone ah! Mara hii nataka kuelekea *East Africa* kuna kisehemu kinaitwa Zanzibar ndio aje, lakini bado fungu ambalo wanatiliwa hawa wenzetu kwa ajili ya kuutangaza utalii Mhe. Spika, ni dogo.

Kwa hivyo naomba serikali ione kama kweli tunaweka kwamba utalii sasa ndio nguzo, huko zamani tulikuwa tunasema karafuu *is a backbone,* sasa hivi tunasema utalii ndio *backbone* ya uchumi wetu, basi tufanye kweli. Lakini hii kudanganyana danganyana hatutofika mbali.

Leo kama tuko *serious* kwa nini hatu-*allocate* pesa tukasema *period* hii tunaweka programu kweli ya uhakika ya matangazo na miundombinu kwa ajili ya kufanya watalii waje katika nchi hii. Si hivyo tunadanganyana danganyana tu.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulisema wengi wamezungumzia *ZBC*. Mimi nasema hivyo serikali imeweka kiwango cha kusema kwamba Shirika letu hili litakapofika mwaka fulani basi tulifanyie *analysis*, tulifanyie *review* na tufanye na mengine. Kwa sababu nahisi kwamba kama serikali wamebeba mzigo, ukiangalia hicho wanachotumia na hicho kinachotoka ni *big difference*, sasa kuna haja gani ya kuweka Shirika hebu rudi nyuma. Sasa sijui serikalini kuna mpango maalum uliowekwa wa kusema kwamba tutakapofika mwaka fulani kama hatujafikia lengo fulani basi hili Shirika tunalivunja.

Mhe. Spika, ni aibu, kwa sababu hii *ZBC* hivi sasa kama wanavyosema wengine ndio mdomo huo mdomo meno yanapungua humu. Atakuwa anasema kibogoyo, unajua meno yakipungua unasema maneno mengine hayapatikani vizuri ndiyo ilivyo *ZBC*.

Kama leo unaipata Kusini Pemba basi kesho Kaskazini Pemba haipo, sijui mpaka lini mambo haya na wengine wameisifia sana, sijui inaonekana wapi. Haya matokeo sawa yanatokea, tunajilazimisha. Lakini mimi siku nyengine nampigia mwenzangu aliyekuwepo Kaskazini namwambia angalia hapo, kuna jambo fulani *ZBC*. Ananambia wapi, *ZBC* mimi nimeshasahau kama ipo hewani hasa. Sasa mzigo huu mimi nafikiri serikali ifike wakati ione kwamba hapa bwana tumebeba gunia la misumari. Hii bwana tuutafute utaratibu mwengine lakini *ZBC* kwa mwendo huu hatwendi.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kusema, wengi wamezungumzia hapa *ZFA*. Mimi nashukuru nilikuwa ni mchezaji mpira mashuhuri sana, na pia nikafanyia kazi *ZFA* Taifa kwa muda karibu wa miaka mitano. Nayajua mengi katika Chama Chetu

hichi cha Mpira wa Miguu. Mimi huwa nashangaa sana hivi karibuni lilitokea sakata kubwa sana kuhusu *ZFA*, na ikafikia wakati vijana wetu huko wakawa hawana la kufanya, mpira hauchezwi.

Kuna mmoja kiongozi yeye ni Makamo Mwenyekiti wa *ZFA* ndiye aliyeipeleka *ZFA* Mahakamani akaenda kuishtaki. Sasa tuko *serious* kweli. Ikiwa wewe ndiyo kiongozi wa michezo, leo unafika wakati wewe ndio unakwenda kushtaki unaizuia michezo isiendelee. Vijana wetu hawa wakasimama kwa muda wa miezi sita mpaka wakapoteza lengo kabisa kwa sababu yako wewe. Eti yeye ndio kiongozi.

Mhe. Waziri hebu tupe kidogo, mtu kama huyu sijui Wizara inamuonaje hivi sasa, na itamchukulia hatua gani. Mtu kama huyu aliyefika hatua ya kupeleka chombo chetu akijua anavunja sheria za *FIFA* kwamba vyama vya michezo hazitakiwi kupelekwa Mahakamani moja kwa moja.

Sasa je, mtu huyu sijui tunamuonaje na keshaandaa utaratibu wowote wa kuona labda huyu alifanya kosa, kwa hivyo labda tuitishe *fresh election* ili hawa wadau wa michezo wamuone kama anafaa au hafai kuendesha michezo aondoke. Mhe. Spika, naomba hili ulifuatilie.

Jengine kuna wakuu wetu wa vitengo kule Pemba ambao wanaongoza vitengo mbali mbali, kwa mfano *ZBC* na vyenginevyo, si hawa katika utaratibu wa maposho wao huwa wamo katika kada gani na labda wanapata chochote, kwa vile wao wanaongoza Idara katika kisiwa cha Pemba au ofisi yetu iliyopo Pemba.

Mhe. Spika, mimi nilisema sitaki kusema sana kwa sababu nimo katika Kamati hii, isipokuwa kuna machache tu nilitaka niyaweke sawa na wananchi wayasikie. Kwa hayo machache mimi nakushukuru.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa na uzima na akatuwezesha kuwepo kwetu hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Spika, nisiwe mwizi wa fadhila nikushukuru na wewe kunipa nami fursa hii ya kuweza kusema machache katika mada iliyokuwepo mezani wakati huu. Nichukue tena fursa hii pia kumpongeza Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri.

Mhe. Spika, wizara iliyo mezani ni ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Wizara hii imebeba mambo muhimu, imebeba sauti ya serikali. Imekuwa ndiyo mdomo na sauti na kufikisha nini serikali inataka na ni dira ya kuonesha Taifa liko wapi na linataka lielekee wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii ambayo umenipa ruhusa niseme kwamba Wizara hii ina mambo muhimu katika wakati huu tunaoelekea katika uchaguzi mkuu wa serikali.

Nalisema hilo kwamba wananchi wengi wa Zanzibar wametulia shwari, na huwa hawasikii mambo wanayoyasikia mengi yao ni kupitia sauti ya chombo chao cha Serikali. Sasa Mheshimiwa hapa nataka niguse hili Shirika lenyewe haswa ndiyo malengo yangu makubwa kabisa.
Kwanza kabisa nami nataka nianze kwa kusema naungana na Kamati na mimi nasikitishwa na Mwenyekiti wa Kamati wakati akisoma ripoti yake naye mpaka anasema tarehe 10 bado vijana wetu hawa waliomo humu hawakupewa posho zao.

Nasema jamani wao walikuwa wana wajibu wa kufanya hili lakini walikuwa wana haki zao. Niiombe sana Wizara ifanye inavyowezekana na ijenge moyo wa kuwathamini badala ya kujenga moyo wa kutusikiliza sisi kama Wawakilishi, tumesema tu inafaa tuwapende tuwatendee haki zao. Hivi kulikoni mpaka Sh. 5000/= ya watoto wetu hawa iwe inasumbua na inatajwa kila wakati.

Mhe. Waziri nakuomba nisingependa kabisa kuweka lolote ambalo lingeweza kufunga maelezo yaliyokuwemo katika kitabu hichi, lakini kwanza naona kwamba nitakuwa sikutenda haki endapo sikudai haki za wafanyakazi hao. Wengine ni wanawake tunawaona wanavyosimama kwa muda wote. Jamani tunasema kwamba mnasema kwamba mmesaini mikataba ya kimataifa.

Mheshimiwa Waziri naomba utakapokuja haja utueleze au utwambie kabisa kwamba tayari umeshawalipa halafu wewe unasema tukupitishie bajeti.

Mhe. Waziri niwambie sasa nataka kujua kwa nini tuambiane kwamba Shirika linaendeshwa kwa misingi ya hasara bado halijasimama. Nataka nikwambie kwamba utaratibu unaokwenda hapo inaelekea sio mzuri.

Tulitoka huko nyuma tukasema kwamba tutakapotengeneza Shirika basi tutapiga hatua nzuri. Tumeona kwamba hata uingizwaji wa hizo fedha zenyewe unasuasua, lakini pia usimamizi inaonesha ni mbovu na haya ndiyo maradhi ya taasisi zetu nyingi, tunaweka azma na malengo madhubuti lakini usimamizi wetu ni wa kusuasua na hatimaye tunakuja hapa ikifika mwaka tunaelezwa tu ilikuwa ilikuwa ilikuwa.

Jambo ambalo haliturudhishi sisi kwa sababu tumekuja humu kutetea haki za wananchi wetu wanyonge. Hii ndiyo sauti yao tukaseme wapi na mnaomba fedha kwamba mtafanya hayo.

Mhe. Waziri nikiacha hapo niseme kwamba kule Pemba kumepelekwa mitambo, lakini hali haiko shwari, maana hayo mambo kama nilivyosema ni sauti. *ZBC* pamoja na *TV* yake na redio ndio vyombo vya serikali ambapo serikali inapotaka kufikisha mambo yake kwa wananchi hichi ndio chombo chake. Kule Pemba vyombo na mitambo iko iweje hawawezi kusikia, kulikoni? Tueleze Mhe. Waziri umeganda wapi? Nini hasa tatizo tuweze kuelewa. Tunashangazwa na kusikitishwa kwamba watu wa aina moja, Taifa moja, wengine wanapata taarifa wengine wanakosa.

Ndiyo maana haya mambo yakafikia pahala, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, kasema pale utasikia hotuba ile ya Umoja wa Kitaifa kwamba Rais kakubali, akasikia jengine kwamba huku limetolewa kwamba mwengine atachukua. Kama taarifa hizi zingetolewa kwa ukamilifu wake mimi naamini kila mmoja angeweza kupima. Tatizo limejitokeza kwamba mnatoa mambo nusu nusu, mambo mnayabinya hayaendi, vipindi mnavisokota sokota, hebu toeni hizo hotuba za viongozi wetu tusikie tuweze kupambanua.

Mhe. Waziri Pemba nao tunatarajia kwamba waweze kusikia tunakwenda kwenye uchaguzi.

Mhe. Waziri ukurasa wako wa 25 unasema kwamba kuna Shirika la Magazeti ya Serikali. Mhe. Waziri nataka nikwambie kwamba kabla ya Mapinduzi kulikuwa na magazeti 60 Zanzibar. Hebu twambie tuna maradhi gani sisi kutoka kwenye 60 tukaja kwenye moja, nalo tukashindwa kulichapisha Zanzibar hii ni aibu.
Haya mambo haya hayaendani na Zanzibar iliyokuwa na heshima yake na hadhi yake, tunautangazaje utalii uliokuwa hauna historia, maana gazeti ni historia watakuja watasoma.

Magazeti 60 yalikuwa, leo moja linakwenda kuchapishwa Tanzania Bara Mhe. Waziri nina masikitiko makubwa sana kabisa kabisa, sikupenda kusikia lugha hii ya mitambo na ofisi pia haipo, hakuna mitambo tukilitaka likachapishwe liletwe tena kwa ndege ndio tuje tupokee gazeti ni aibu.

Tuna umri mrefu Mhe. naomba sana taasisi yako hii iangalie, Serikali iangalie kwamba hivi jamani bado tunakwenda kuchapisha huko, tulipotaka kweli Baraza hili lilikubali kuidhinisha fedha ya meli na tukanunua meli na nasikia karibuni tu kwamba itawasili hapa. Tuna nini mambo ya msingi kama haya tuweze kushindwa au ndio aliyoyasema Mhe. Hija, tunapanga mishahara tu sisi *O/C* nyengine sijui, maana yake alimradi watu wapate mwisho wa mwezi mshahara wao.

Hili linasikikitisha na linatia aibu, nasema kwamba *In shaa Allah* akipenda Mwenyezi Mungu tunataka kusikia bajeti ya mwakani basi mtambo huu

unapatikana na shughuli hizi zinafanyika kwetu Zanzibar, tunaomba sana Serikali ifanye hivyo.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye ukurasa wa 33 ambao unagusa Sekta hii ya Utalii, sekta kiongozi ambayo kwa sasa inatumika kuweza kuongeza pato la Taifa letu na tukajisifia sana kwamba tumeongeza nguvu.

Sasa hivi jamani fedha ndogo kama hii ambayo inatengwa katika taasisi hii kweli tunaweza tukafikia malengo? Unajua kama laiti ingelikuwa Mhe. Spika, sikuwa nimeleta jina langu kuomba nisingeomba Mhe. Hija alinimalizia maneno, na kwa nini amalize ni ile fedha ndogo ambayo tunasema tunataka kwenda kwenye huo utalii wa kweli ili tuweze kufika na tuweze kufaidika, lakini fedha iliyotengwa ukiangalia unakuta hasa kwenye hiyo dhana ya utalii kwa wote. Unakuta fedha ya kuitangaza yenyewe Zanzibar ili watu watuunge mkono watukubali na waje kutembea, waje kuwekeza, waje kufanya mambo mbali mbali. Wengine waje kutembea na wengine wawekeze ili tuweze kupata kuongeza pato la Taifa na kuinua uchumi wetu.

Nchi yetu imeingiwa na mambo mengi, mabadiliko tabia nchi sasa ule ukulima pia nao umepoteza uwezo na mambo mbali mbali. Utalii tulitarajia kwamba uwe ndio taasisi ambayo itaongeza pato la Taifa letu na wanyonge waweze kuneemeka.

Mhe. Waziri nakuomba utakapokuja hapa uniambie ile dhana ya *utalii kwa wote*, uniambie namna na utaratibu ambapo wanafaidika wale wananchi ambao ni wakulima wanapeleka mazao yao kwa ajili ya huduma za kihoteli wakiwemo wavuvi na wafugaji. Kwa sababu dhana hii ya kwa wote inakwenda mpaka watu wetu kwenye taasisi za kilimo, ili wote nao katika biashara zao hizo badala ya kuhangaikia masoko na mambo mengine tuone wewe umewabebaje katika dhana hii ya utalii kwa wote.

Tukiwaacha wale wachache ambao ni mapapasi na wachache ambao wameajiriwa katika mahoteli mbali mbali. Mhe. Waziri hili uje unipatie kidogo niweze kuelewa kulikoni. Lakini kuna kitu chengine kuna wale wenyewe wananchi ambao wameamua kutoa hizo bidhaa kwenda kwenye mahoteli kupeleka kutoa huduma, hawa mara nyingi Mhe. Waziri wale watu wanaohusika na mahoteli haya wale wasimamizi wanawanyima fursa ya fedha zao wakati mwengine wanafunga inakuwa ni tatizo kwao kudai haki zao hizo Mhe. Waziri.

Hebu tusaidie watu hawa maskini wanyonge, wengine wanapeleka tungule, wengine wanapeleka mabilingani, wengine wanapeleka mambo mbali mbali. Lakini inapofika muda wa kwenda kuchukua fedha zao inakuwa ni tatizo. Wanafunga mikataba unawashughulikia kwenye mambo ya mikataba. Mimi

nakushauri maana kuna virisiti vidogo huwa wanapewa vile nimeona mimi, hebu niambie wewe Mheshimiwa ili ile dhana ya utalii kwa wote nao wafaidike wewe katika utaratibu huu hebu wafungishe basi hata mikataba, washauri jumuiya yao nayo ikuwe; iwe kubwa wawe na jumuiya maalum ambayo itasajiliwa, na hatimaye utaweza kuisimamia mikataba yao katika haya mahoteli ili haki zao na ile dhana ya utalii kwa wote na wao ile faida iwafikie.

Jengine ambalo Mhe. Panya na yeye alilizungumza ni kwamba taasisi hii wanawake wengi inakuwa wanafanya kazi katika sehemu ile, lakini kwa kweli mbali ya mikoba vifaa vile vyengine lakini hata wale waliomo katika yale mahoteli mara nyingi sana imekuwa kazi zao ni kufanya, na hatimaye kufukuzwa maskini wanakosa kiinua mgongo na haki zao zinapotea, hali imekuwa ngumu kwao wanawake hawa.

Mhe. Waziri dhana ni kwa wote hebu tuambie wanawake hawa wewe wanaofanya kazi katika mahoteli haya hali ikoje, wewe unawasimamia vipi.

Mhe. Waziri nataka kujua tena jambo jengine vile vivutio vya wageni hapa Zanzibar tunavyo vingi, kwetu kuna Mangapwani kuna kisima cha chini kwa chini kuna na nyumba ya chini kwa chini.

Hebu twambie hasa hivi vivutio tayari umeshaweza kuvifanyia tafiti, na tafiti hizo umevijumlisha viko vingapi haswa, maana umesema umefanya humu lakini ni vingapi na vipi vipo katika daraja la kwanza ambavyo vinaweza vikawa ni vivutio vya mwanzo kabisa, kuona kwamba wageni wetu wale wa daraja la kwanza wanavipenda zaidi, vitatupatia fedha na watu wetu wanavutika na hili na vyengine vyote vingi vyao.

Mhe. Spika, sasa nije hapa kwenye Chuo cha Utalii hapa nitakupongeza kwamba umekiboresha, umejenga kidogo na sehemu nzuri ambazo vijana wanapata taaluma pale nje wanapata hali nzuri, tunafurahi kwa hili nasema hongereni kwa hili. Lakini lengo letu pale la kutengeneza kile chuo halikuwa ni kujenga Chuo tu cha Utalii, kwamba tuje tufanye tu iwe basi.

Moja katika lengo ni kuongeza au kuzaa ajira kwa ajili ya vijana wetu, kwa sababu tulisema kwamba vijana wetu wanashindwa taaluma na wanashindwa kuajiriwa, kwa hivyo dhana hii ikaja tujenge chuo hiki na tusomeshe ili vijana wetu waweze kuhimili sio ushindani wa soko la utalii.

Nakuomba Mhe. Waziri hebu unipatie kwamba wahitimu wa kile chuo kwanza ni wangapi, na wangapi wameweza kuajiriwa, sasa tuchukue hizo nafasi ambazo tunataka wazichukue hawa vijana wetu ni wangapi.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Waziri tumepata tetesi kwamba vijana wetu pale wanapotoka kwenda *field* huko, mahoteli mengine wanakataa eti kuwachukua, na tuulize hivi kwa nini waweze kuwakataa labda kuwachukua hawa vijana kwenda kufanya hayo mafunzo ya vitendo kama ni kweli hili. Kama ni kweli labda utupe na sababu, kuna sababu gani ambazo zinawafanya labda wasiwapokee, wanasema kwamba wanapata tabu sana hawa vijana, kama ni hivyo basi utwambie kwamba labda ni hivi.

Mhe. Spika, sasa nije hapa kwenye makusanyo kidogo. Hivi katika Hoteli ya Bwawani nini kimekwaza mpaka wawe na asilimia 24 tu ya makusanyo, nyengine ziweze kumudu mpaka asilimia 83 na 92 lakini hii Hoteli ya Bwawani katika makusanyo iwe imeshindwa kulikoni?

Nataka niwaambie Serikali ile ni hoteli yetu ya Serikali hamjaiamulia kwenda katika ushindani wa kukubalika, hebu ijengeeni mazingira yanayoendana na wakati wa leo ihimili ule uwezo kama yalivyo mahoteli mengine.

Mimi ninaamini kwamba hata nyinyi Serikali hamko tayari kufanya mambo yenu mengi pale, mkipata mambo yenu mnakimbia mnakwenda zenu huko mahoteli mengine nje mnatoka. Lakini kama mngekuwa Serikali mambo yenu yote mnatumia hoteli ile, mimi ninaamini ingekuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha, lakini Mhe. Spika, ninagusa tena hapo wale wafanyakazi ambao wamefukuzwa, na kuna wengine bado wana mashaka, hebu twambie wafanyakazi hawa kulikoni na wenye haki zao nao walipwe.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye Sekta hii ya Utamaduni. Nataka niseme taswira ya Taifa utamaduni wake ndio unaoonesha. Utamaduni wa Taifa ndio nembo ya Taifa, wageni mnaowaona wanatoka huko na kuja hapa kwetu hawatamani kuona mambo yale ambayo wanayaona Ulaya na kwengineko, lakini wanachokipenda ni kile kuona kwamba yale mambo ya mila na tamaduni zetu za Kizanzibari ndio kivutio chao. Kulikoni leo Mheshimiwa wewe umeiboresha vipi, maana hata yale mavazi yetu ya kanzu na kofia mkawa mnapendeza hapa haionekani taswira hiyo ndio wazanzibari, lakini na wanawake wanavaa kanzu na majalbibi yao, na vitu vyao ndio utamaduni wetu, tuna mambo yetu ya mitungi na kujitwika kata leo hakuna, kuna mambo ya kili na mambo mengine na mikopa.

Leo kuna mifuko ile ya lambo tunapiga kelele kwa mifuko mibovu. Wewe kama wewe utamaduni wetu ni mikoba, mikeka na mambo mengine. Leo mabusati imekuwa ni dili ambayo hayapo katika asili ya Wazanzibari; Watumbatu na Wamakunduchi na Wahadimu wa hapa, hivyo vitu si vya kwetu, sisi tuna ya kwetu hasa.

Tuna mavazi, tuna mapishi, tuna mambo mbali mbali ambayo ndio mila na tamaduni ya kizanzibari, tuna nini wakati hicho ni moja katika kivutio cha watalii, watalii hawataki kuona *jeans* na tai si mambo yetu. Nguo zimebana zimekuwa *tight,* na wao wamevaa suruali wanawake wa Zanzibar si kweli, si utamaduni wetu.

Ninaamini kwamba, kama watakuja wageni na wakaona hasa huu utamaduni wetu wa Kizanzibari, nina imani kubwa kwamba watakuwa wanapeana wenyewe taarifa na kuona na kurusha kama Bi Mgeni alivyosema katika mitandao mbali mbali, watapata na watafaidika na hayo, na hayo ndiyo watakayoyafuata, halafu tukiwapikia vile vyakula vya kwao walizoea, tuwapikie vyetu hasa vya mila na tamaduni zetu.

Mimi ninaamini kama wataona hivyo kuna ugali wa muhogo kwa pweza Mheshimiwa ananifahamu sana ndio mambo yetu na chwale na mambo mengine, jamani si ndio vyakula vyetu. Maana yake hiyo ni utamaduni, na ikioneshwa tamasha kama hilo na wakaona hapa kwetu Zanzibar kama wanakuja, maana yake wanavutika kuona kwamba kweli Zanzibar hicho ni kisiwa na kiko hivi na tamaduni yake tunapata hiyo fursa.

Lakini nikwambie jengine kwamba mambo haya ya utamaduni na kujisahau sisi wazanzibari jamii yetu sasa imepotoka na hali imekuwa ngumu, zile mila na tamaduni zetu tumeondosha kila kitu tumesema tunakwenda na teknolojia; *digital*, Mheshimiwa utamaduni hauendi na *digital*. Turudi tuna mambo ambayo kwa kweli mafunzo haya yakipatikana na yakifanyiwa taratibu huko vijijini kwetu, na hata mijini basi inaonesha hasa ile heshima na hadhi ya Zanzibar na hata utamaduni.

Mhe. Spika, na haya yanaendana sambamba sana kabisa na ile Baraza letu la Kiswahili. Mambo poa, mpango, shughuli yaani vitu vya ajabu ambavyo sisi kwa mila na tamaduni za wazanzibari hazipo. Ushefa sijui nini, hebu tuulizane jamani hii ndio tamaduni ya Zanzibar, ndio ukweli tunaizungumzia hii taasisi yetu sisi kama wazanzibari hiki ndio Kiswahili chetu hiki?

Siku moja nilimsikia Mwalim Haroun hapa akikataa neno wadau akisema hasa mimi lugha hii ya wadau siipendi, lakini tujiulize inaandikwa mara ngapi katika taratibu zetu sisi kama waswahili na sisi ndio chimbuko la Kiswahili fasaha. Kiswahili cha mwambao ukikitaka hasa njoo Zanzibar, ndio kwao, wengine wote wanaiga tu Kiswahili kitamu chenye ladha ya kuzungumzika ni hapa.

Hebu tujiulizeni mambo, mshefa, imekuwaje, gonga, imekuwaje mshua ndio ya kwetu? Ndio sayansi na teknolojia hii tunayoitaka ambayo inaendana na wakati. Wenzetu wanathamini mambo yao mengi ambayo wanayajua na utamaduni wetu sisi tukifika na hapa *asalaam aleykum*, ukimaliza hapo shikamoo baba ndio

tamaduni zetu, shikamoo mama, shikamoo bimkubwa, dada shikamoo, ndio utamaduni wetu. *Wallahi* leo mtu baba yake anamuuliza mambo mzee bwana, mzee si unamjua lugha nyengine wanaita dingi. Hivi mnadhani maadili haya tunaweza tukafikia na hicho ndio Kiswahili kilivyo Mhe. Spika. Nasema kwamba ninapata mshtuko mkubwa kwamba inawezakana Kiswahili fasaha kikapotea Zanzibar, na sisi ikafika muda twende tukasome Kiswahili pahala pengine ambapo asili yake na chimbuko lake ni hapa kwetu Zanzibar kwa hivi tunavyokwenda kwa wakati huu inawezekana sana. Kwani tulikuwa na mangapi na yamepotea, sasa hivi tunakwenda kuyatafuta kwengine, tujiulize tulikuwa na mangapi na sasa tunakwenda kuyatafuta kama vile kwetu hayakuwepo.

Kwani hilo gazeti nililosema mimi likichapishwa wapi, si hapa, tena sasa hivi kwa nini tunakwenda huko Tanganyika kuchapisha? Nasema hivi kwa ushahidi huo, umefika wakati wa kusimamia, tusiende tu kama tunavyotaka ili utamaduni wetu ubaki na uheshimike, na hayo mahoteli yafanye kazi vizuri. Na kweli tupate fedha ya kiutalii basi hayo ni ya kuzingatia.

Kwa nini tuwaruhusu wageni wavae viguo vifupi wakati sisi utamaduni ni kuvaa nguo ndefu, Hayati Mzee Abeid Amani Karume alikuwa wakati huo nasoma darasa la tatu wanakuja wageni wamewekewa vile vitenge jamani, wakifika wanavalishwa pale bandarini wakati huo nimekwenda pale tunacheza ngoma mtoto mdogo kabisa tunawapokea wageni. Wamevalishwa nguo ambazo ndio tamaduni za Kizanzibari, sisi hofu yetu nini, tuna hofu wageni, eti watapotea wageni maana yake ndio tumewaambia. Tamaduni yetu ni hiyo tuvae nguo, na kama tunawafanya hivyo maana yake na wao watajenga hasa tamaduni ya Kizanzibari kumbe ukifika ni hivi watatufuata sisi.

Wangapi wamekuja tumewaona wamevaa kanzu na kofia wazungu hapa, tujiulize tumeona, lakini sisi tunaona kwamba wakitupita uchi mbele ya wazee wetu na watoto basi wakiondoka maana yake ndio wageni hao.

Utamaduni wetu ndio silaha na ndio uchumi wetu, tukisimamia kweli nina imani kwamba tutaongeza pato la Taifa nina hakika. Kwa sababu wakituona tumevaa wakienda shughuli za maulidi utawaona walivyoshughulika na kuhamanika roho zao. Hii inaonesha kwamba wanapenda na wanavutiwa mno na hilo, lakini sisi sasa tumekuwa ndio wazungu wenyewe wakija hilo wanalotaka kuona hawaoni.

Mhe. Spika, hali hii ninaitahadharisha sana Serikali,tuna majanga yamelikabili Taifa, kuna madawa ya kulevya ukiuliza sana kama utakwenda mno utaona hasa tamaduni ile yetu ile ambayo ilikuwa inalelewa baada ya saa mbili na nusu kula ugali wazee wakikaa na watoto wao kuwaeleza mambo, kulikuwa na baraza maalum kina Mzee Shamuhuna wanajua hayo leo tamaduni hizo zote zimepotea.

Tunasema mambo mengi lakini utekelezaji wake umekuwa mfupi sana, Serikali msidhani kwamba kuna mtu mwengine atakuwa *mas-ul* sisi ndio *mas-ul*, nyinyi ndio *mas-ul* tutakwenda kuuliza huko.

Balaa leo tumekuwa tunatumia *a lot of money* kwa ajili ya UKIMWI, madawa ya kulevya fedha ambazo pengine tungekuwa wakakamavu zaidi tungezitumia kwa shughuli za maendeleo, shughuli nyengine kabisa ndio ukweli, lakini tunalazimika kufanya hili kwa sababu sisi wenyewe kuna mambo tumeyazembea, kuna mambo tuliona kwamba tukifanya hivi tukibana hivi itakuwa hivi, si kweli nikwambieni, si kweli. Mambo yapo, shughuli ipo na utamaduni upo na vijana walikuwepo hata enzi hizo, lakini hakuna kijana aliyekwenda uchi, hakuna kijana aliyekwenda uchi, hakuna kijana aliyevuka miiko. Leo jamani hivi tunavyokwenda wakati mwengine ukiwa na mtu ambaye unamstahi huwezi kuangalia macho, mtu anavyokupita ndio ukweli, ndio utamaduni wa Zanzibar huo tunaoutarajia? Hayo tuyafikirie, lakini pia tujue kwamba sisi sote ni waumbwa na tutaondoka, na kwa Mungu ni *Mas-uul.*

Mhe. Spika, hee! Nimezoea sana Mwenyekiti, Mheshimiwa nisamehe sana unajua muda kidogo sijakuona.

Haya mambo ya kale haya nije na historia. Nilianza hivyo Mheshimiwa wananionea choyo choyo hawa, naomba uniachie maana yake hii kidogo inawajenga nini. Lakini niseme kwamba mambo ya kale kwa kweli kwa Zanzibar ni muhimu nayo kuweza kujulikana, kwa sababu yatajenga historia pamoja na uelewa wetu wa uwepo wetu kama tulivyokuwa tulisema kwamba uwekaji ule wa kumbukumbu zetu, tukasema kwamba *archives* za mambo yetu yale ndio historia yetu, kwa hivyo kuna mambo mengi ambayo yatapatikana humo. Kwa hivyo, haya mambo ni muhimu kweli mambo ya kale kuwepo, watasoma vijana wetu wenyewe historia yao na wataielewa. Mtu aliyekuwa hajui historia yake anakuwa mtumwa jamani, kujua historia yako ni uungwana.

Kwa hivyo, ni muhimu sana mambo haya, na hata walimu nao waichukue hiyo fursa kuona kwamba vijana wetu wanakwenda kwenye zile sehemu mbali mbali ili kuweza kujifunza mambo yetu ya kale, na kuona hasa watakuwa wana historia, wazuri watakaoweza kuielewa na kuieleza tukiepuka yale mambo ya kuja mtu haijui historia ya Zanzibar naye akapata fursa ya kuchukua wageni kwenda kuwatembeza. Kwa hivyo, utakuta pia mbele huko unazalisha ajira.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunivumilia kunipa fursa hii nami nasema Mhe. Waziri anisaidie majibu hayo sina nia ya kuzuia fungu, lakini nina nia kwamba wale wenye haki waweze kupewa, haki na wajibu ni vitu vinavyofuatana, kwa hivyo hayo yakitendeka sina mashaka Mheshimiwa naweza nikakubali kupitisha fungu hilo, lakini napunguza kumi kwanza nipate majibu yake.

Ahsante nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nafikiri sitokuwa na mchango mkubwa sana kwa wizara hii, *hardly* nitatumia dakika saba mpaka kumi pengine.

Mhe. Spika, asubuhi hii niliuliza swali hapa na nikataka kuinuka kidogo kutoa muongozo lakini nikaona haina haja najua wizara ipo na nitachangia.

Mhe. Waziri naomba unisikilize kwa makini kabisa sasa hivi kuhusu suala la asubuhi, juu ya taarifa ya habari ya Kiingereza katika *order paper* yetu ya asubuhi.

Mhe. Waziri mimi siwezi kuleta kitu kama nikakurupuka tu usingizini saa tisa ya usiku, unakuwa ni usingizi mzito.

Taarifa ya habari Mhe. Spika, *internet* ni kitu muhimu, wewe nafikiri Mhe. Waziri ulivyofahamu pale mimi sikutaka mabishano makubwa, nafikiri taarifa ya saa sita tunataka itangazwe vile vile Kiingereza kwa Kiswahili nilivyokufahamu ulipojibu swali.

Mhe. Spika, *internet* ni kitu muhimu Mhe. Waziri ndio inayoleta ripoti na mambo yalivyo, pia ndio unapata habari za dunia zikoje. Lakini taarifa ya saa tisa inaletwa kwa Kiswahili, unataka itangazwe tena kwa Kiingereza vile vile si kitu kizuri.

Taarifa ya habari ile ya saa tisa ni ripoti zetu hapa hapa za Unguja na Pemba labda na Dar es Salaam tunasikia. *Internet* inahitajika Mhe. Waziri nakuomba ufanye ziara hiyo na watendaji wako, na niko tayari kama nimekosea mimi mwenyewe nikosoe mimi sio mkamilifu. Mkamilifu ni mmoja tu, yeye ndiye anayetushughulikia, mimi si lolote si chochote, lakini hiki kitu kipo Mhe. Waziri ki-*note* na sikutaka kubishana pale asubuhi, nikaona ah leo wizara ipo nitapata kuzungumza kwa ufasaha kabisa.

Mhe. Spika, na suala la *link* Mhe. Waziri lipo sikutaka kubishana. Naomba liandike nalo ulifuatilie, waulize watendaji mimi siwezi kuja kukurupuka nikazungumza kitu nisichokijua. Naomba liandike na ulifuatilie suala la *link* watendaji wetu hawa wana kazi nzito, waulize kutoka pale *studio* na hapa kuungana karibu dakika au nne sawa sawa nakwenda kwa baiskeli au kwa gari utafika ofisini. Huo ndio ufafanuzi, nilitaka kuweka sawa katika hapo.

Mhe. Spika, sasa kwanza nichukue fursa hii kuwapa pole waandishi wa habari wa dunia nzima ikiwemo Zanzibar kwa kazi wanayoifanya ya kuelimisha jamii, kazi ambayo nzito, kazi ambayo malipo yake wategemee kwa Mungu. Katika watu

wanaoelimisha jamii ni waandishi wa habari. Waandishi wa habari wanahitaji kuenziwa na kuhifadhiwa na kupewa heshima zote.

Mhe. Spika, hivi hapa tulipo kama si waandishi wa habari hawa ripoti zetu leo zingetoka huko nje, zingekuwa humu ndani wananchi wasingeweza kuzifahamu. Waandishi wa habari mimi nikupongezeni kwa dhati kabisa, kazi munayoifanya ya kuelimisha jamii ni kazi moja kubwa sana. Tulikuwa tunazungumza ndani tu ripoti zetu zingetoka? Lakini waandishi wa habari wamekuwa wakizichukua kwa jitihada zote. Mhe. Spika, nishukuru vyombo vyote vya habari vilivyopo Unguja na Pemba kazi wanayofanya ni ya mfano.

Mhe. Spika, kipindi kinachokaribia ni cha Uchaguzi Mwenyezi Mungu ajaalie uchaguzi huu uende salama, amani na kwa utulivu wa hali ya juu.

Waandishi wa habari hawa watakuwa na wakati mgumu katika kipindi hiki cha uchaguzi. Mimi niwaombe tu wawe na utaratibu wa kuvaa *uniform* yasije yakatokea kama yale ya Daudi Mwangosi yaliyotokea kule Iringa.

Ni kwamba vurugu litakuwa kubwa, lakini Mwenyezi Mungu asije akajaalia kutokea, wawe na *uniforms* angalau wajulikane wasije wakapigwa mikwaju wakaja kuvurugwa wengine wakaonekana, narudia tena Mwenyezi Mungu asije akajaalia kutokea kitu hicho, uchaguzi uwe wa salama, amani na utulivu. Lakini waandishi wa habari angalau wawe na *uniforms,* kipindi tunachokwenda ni kizito na wao wanataka kuelimisha jamii.

Pia mashirikiano lazima wapewe waandishi wa habari. Mimi naomba wawe na utaratibu wa kuvaa angalau *uniforms* wasije kufika pahali wakaja wakapigwa, wakateswa, wakaja wakanyanyaswa, ni haki ya msingi kwa waandishi wa habari.
Mhe. Waziri hapa mimi sijui nitumie lugha gani, sijui niseme nitakuwa mkaidi au matata, sijui Kiswahili gani nitumie, lakini leo karibu vipindi vitatu vya Baraza hili tumo ndani mama yule kule anapigwa na baridi amejifunika kanga, mama kavaa koti kule, kuna wengine wako nyuma, wengine wako ndani shilingi elfu tano *laahaula walaa quwwata illa billahi* ama hapa Mhe. Spika, hili nitalisema mimi mpaka pumzi yangu ya mwisho.

Nimezungumza kidogo kidogo Mhe. Spika, lakini hapa kidogo itakuwa na hali nyengine, hatuwezi kuwanyanyasa hawa hata siku moja kwa shilingi elfu tano kwa siku.

Hapa Mhe. Waziri patachimbika au tutafukia, kipindi cha tatu hawa shilingi elfu tano kwa siku vipindi vitatu wanakuja humu ndani wanashindwa kulipwa, watafanya kazi vipi hawa katika mazingira haya.

Mhe. Spika, na la mwisho kama halikuweza kupatikana mimi nitaomba Waheshimiwa Wajumbe kila mmoja tutapitisha bahasha japo shilingi elfu tano tuwachangie mpaka kumi, la mwisho nitafanya hivyo.

Hatuwezi kuwanyanyasa hawa kabisa, kazi wanayoifanya tuwaheshimu hawajatuvunjia heshima. Wamefanya kazi katika mazingira magumu, hatuwezi kufika huko.

Mhe. Spika, nawaambia waandishi wastahamili, kuna msemo sijui kama *muongo muongoze* au *mwizi siku zake arubaini* lakini hii ndio bajeti ya mwisho, hii tutajua mwisho kusuka au kunyoa kwa wafanyakazi, ama pasuka ama chanika!

Mhe. Spika, baada ya hapo kidogo nije katika Shirika la Utangazaji la *ZBC*. Kidogo hapa nitoe masikitiko yangu kwa lugha ya chini kidogo.

Hebu waandishi nisaidieni hapa Waziri anapojibu hoja kuna sababu gani kutajwa waziri yule aliyechangia hatajwi, hebu nielezeni waziri nije nipewe maelezo hili limetokea kule Dodoma, wanaonekana Wabunge wengine bubu hawajui wawakilishi wao wamefanya nini, waziri utaambiwa pale kajibu swali Barazani, kachangia nini waziri yule, aliyekuuliza huku nani hajulikani.

Hapa pana kitu gani kimejitokeza kuna msingi gani, kidogo hili nije nifahamishwe, waziri utasikia hapa Mhe. Said Ali Mbarouk akijibu swali Barazani aliyeuliza Mhe. Mussa hili swali huoni hata kuulizwa.

Sasa wananchi wake watafahamu nini, kazi gani iliyompeleka pale? Hapa kidogo nina masikitiko yangu utakuja kunieleza.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije katika mwekezaji wa Kisiwa kile cha Mnemba…

Mhe. Spika: Umeomba dakika tano, tano zimekwisha nakupa na tano nyengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, mwekezaji wa Mnemba kama kuna pahali huyu mwekezaji kuufuatilia mwendo wake, na wananchi kuteseka kule wanavyoteseka kama lile eneo amemilikishwa tujue kamilikishwa.

Leo haiwezekani mtu ufukwe kwenda kuutumia au mtu akaharibikiwa na chombo kwenda kukaa pale, kuna askari wana silaha anawafukuza. Hapa nitahitaji maelezo, haiwezekani mwekezaji wa Kisiwa cha Mnemba wananchi pale wapo katika shughuli zao leo mwekezaji huyu anakwenda kuwanyanyasa watu. Hapa Mhe. Waziri nitahitaji maelezo ya kina, nataka kujua kisiwa hiki kapewa kigezo gani ikawa wananchi pale wanakwenda kuvua mita mia mbili wasikaribie,

haiwezekani kuna mtu kuharibikiwa kule hakuna mtu, angalau ukakifunga chombo pana ufukwe na ufukwe kila mtu haki yake kuutumia.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije katika Shirika la Gazeti mazingira wanayofanya kazi magumu hiki kipindi cha mwaka wa tatu napiga kelele. Gazeti ni chombo muhimu lakini mazingira yale tushapiga kelele mpaka tushachoka, mazingira ya gazeti leo hayaridhishi hata kidogo, ukienda kutizama dirisha halionekani, ukienda ukitizama feni hulijui liko wapi. Kwa hiyo, tunahitaji maelezo ya kina.

Mhe. Spika, kwa hiyo Mhe. Waziri hapo utakapokuja itabidi utueleze suala hili kwa kina kabisa.

Baada ya hapo nitahitaji maelezo kuhusu *ZFA*. *ZFA* sasa hivi inataka kufanya uchaguzi inashindwa tatizo sijui kuna kesi Mahakamani.

Mhe. Spika, mpira tunaua wenyewe, watendaji wetu tunawaumiza wenyewe, huyu nani aliyepeleka kesi Mahakamani hata mashindano haya ya Mapinduzi yalikuwa kama haikutumika nguvu hapa, nimshukuru sana kwa umakini wake aliokuwa nao kiongozi wetu Mhe. Balozi Seif Ali Iddi lakini tungepata aibu, na mashindano yale yasingefanyika.

Kwa hiyo, hili suala Mhe. Waziri hebu lifuatilie, hii kesi ni muda gani leo, tunainua mpira au tunavuruga mpira, ingawa kanuni zinakataza kitu kilichoko Mahakamani tusizungumze, lakini Mhe. Waziri hicho nakuomba lifuatilie suala hili kwani wanapata shida watendaji wetu.
Mhe. Spika, kwa kumalizia hata mimi niwashukuru waandishi wa habari hasa pale walipotuonesha jinsi ulivyofanyika unyama, walinzi wa hospitali ya Mnazi Mmoja, haya mambo ni ya kusikitisha sana.

Mhe. Spika, baada ya hapo nimalizie nilipigwa mimi, na waandishi wa habari wakanionesha hospitali ya Mnazi Mmoja, nataka maelezo nilikuwa sitaki kuzungumza hivyo, ila nilipigwa mimi kama Mwakilishi lakini waandishi wa habari wakanionea huruma wakaona ah ikiwa Mwakilishi amepata shida kama hii tumuoneshe ili wanyonge wasije wakampata.
Nimekushukuruni waandishi wa habari walitaka ufafanuzi kidogo mimi nimeliweka sawa hilo.

Mhe. Spika, kuhusu mgao wa *FIFA* hebu Mhe. Waziri na hili lifuatilie katika dola laki mbili na nusu zilizopatikana zile, na dola laki moja katika mashindano ya *CAF* karibu laki tatu na nusu Zanzibar tumefaidika nini.

Tanzania inaitwa kutokana na Zanzibar. Mimi ninachokijua baada ya nyasi bandia za Uwanja wa Gombani sijajua nyengine tulichopata, suala hili nimeshauliza Bungeni mara tatu mpaka nne tunaambiwa tupeleke programu zetu na sisi. Na mwisho nikawaambiwa je, mko tayari kutuazima mwaka huu tuchukue sisi, wakakataa. Kwa hiyo, hili suala nalo lifuatilieni *FIFA* katika mgao huu Tanzania inatokana na Zanzibar, kwa huu mgao angalau baada ya uwanja ule wa Gombani sijajua chengine kilichofanyika, mimi nitahitaji maelezo baada ya hapo.

Mhe. Spika, nafikiri nisipoteze muda nataka nipate maelezo ya kina ili tuweze kuja kupitisha bajeti hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kuchangia mawili matatu katika bajeti yetu hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na mambo mengine yote.

Mhe. Spika, baada ya kwisha kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia kwa kupitia chombo chako hiki naomba niwatakie kheri Waislamu wote katika kukabiliana na mfungo mtukufu wa mwezi wa Ramadhani, *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu atujaalie Ramadhani yetu tuifunge kwa amani na salama, na Mwenyezi Mungu akubali vile vile Ramadhani yetu pamoja na dua zetu ambazo tutaziomba wakati huo.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii, lakini kwa aina ya kipekee nimshukuru Mhe. Waziri na timu yake ya watendaji katika wizara yake, ikiongozwa na Katibu Mkuu wake ambaye pamoja na yote leo siku ya bajeti lakini hapa sijamuona, lakini pia namshukuru.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo leo naanza na pongezi katika wizara hii. Kwanza pamoja na matatizo yote tuliyonayo, napenda kuipongeza *ZBC* kwa kazi nzito na kubwa wanayoifanya katika kutuhabarisha ndani ya nchi yetu hii ya Zanzibar, Tanzania na dunia kwa ujumla.

Mhe. Spika, pamoja na changamoto tulizonazo katika taasisi hii, lakini bado tungali tunaendelea kupata taarifa muhimu kwa kutumia chombo chetu cha *ZBC;* ambacho kinasimamiwa na waziri wetu Mhe. Said Ali Mbarouk, na wananchi wa Zanzibar wanapata huduma zao muhimu.

Mhe. Spika, lakini nikiondoka hapo nakwenda katika kitabu chetu hiki leo naanza nyuma ikisha nakuja mbele.

Ukurasa wa 75 mpaka 81 hapa Mhe. Spika kuna idadi ya wanafunzi ambao wamesomeshwa na wizara hii.

Ukiangalia kiambatanisho namba 2 wafanyakazi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambao wamekwenda masomoni kwa mwaka 2014/2015 ni wafanyakazi wasiopungua 61. Hii ni tofauti kabisa na namna mawizara mengine tunavyoona inavyosomesha watu wake, ukiachilia Wizara ya Elimu lakini hii mimi niwapongeze sana wizara hii kwa kufahamu taaluma hii, na kuwapatia mafunzo watendaji wake katika kiwango kama hiki, wanafunzi 61 si mchezo Mhe. Spika, kuwapatia masomo chini ya uongozi wa serikali yetu hii tunayokwenda nayo ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo na mimi niungane na walio wengi. Wenzangu wamezungumza kila mmoja kwa *style* yake katika suala zima la hali halisi ya hawa watendaji ambao tunao humu ndani.

Mimi nasema kwamba katika buku letu kubwa ukurasa wa 509 kuna kifungu hapa S02 Uendeshaji na Usimamizi katika sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuna fungu hapa lina shilingi bilioni moja, milioni mia tatu na sabiini, laki moja na hamsini na tatu elfu.

Fungu hili mimi nitalizuia mpaka nihakikishe Mhe. Waziri amenipa hatma ya wale watendaji ambao wamo humu ndani, hilo nitalifanya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja katika sekta ya utamaduni kifungu cha 14 cha kitabu chetu. Mhe. Spika, naomba kunukuu.

> "Hatua za kuendeleza harakati za ufufuaji wa maeneo ya kihistoria zimekuwa zikifanyika ili kutoa mchango mkubwa wa kuongezeka kwa vivutio vya utalii. Mradi wa ufufuaji na uhifadhi wa maeneo ya kihistoria (*Restoration and Conservation of historical Project*) ni mambo ambayo tayari yanafanyiwa kazi".

Mhe. Spika, mimi nimefarijika sana kuona kwamba na angalau katika kitabu chetu cha mara hii kumezungumziwa suala hili la kufufua maeneo ya kihistoria kwa ajili ya kuendeleza na kutunza zile tamaduni zetu za Kizanzibari.

Mhe. Spika, kama tujuavyo Zanzibar mapato yetu asilimia 80 yanatokana na shughuli za utalii, lakini bado maeneo hasa ya kuwapeleka watalii wetu tumeyaweka nyuma. Namuomba sana Mhe. Waziri haya maelezo ambayo nimeyazungumza hapa naomba wakayafanyie kazi na waunde kamati maalum ambazo zitakwenda kufanya kazi hii kwa kina, ili kuboresha yale maeneo yetu yenye utamaduni na historia zetu na kuhakikisha kwamba hawa wageni ambao wanakuja katika nchi zetu wanakwenda kuangalia historia halisi ya nchi yetu na

sisi kuweza kunufaika na maeneo haya, ambayo wageni watakuwa wanakuja kwenda kuyatembelea na hatimaye kuchangia chochote ili kukuza sekta ya utalii.

Mengi yamezungumzwa katika masuala haya ya utalii sitaki nirudie rudie kwa sababu wenzangu wameshayazungumza sana.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sekta ya utalii kifungu cha 20 naiwacha kwa sababu wengi wameizungumza, lakini nakwenda kifungu cha 42 ambapo kuna taarifa ya masuala yanayohusiana na habari.

Mhe. Spika, malengo ambayo yamewekwa hapa ni mazuri ambayo wizara imejipangia kwenda kuyasimamia. Lakini cha kusikitisha hata mwaka juzi baadhi ya malengo haya yalikuwepo na hatujaridhika na utekelezaji wake. Tunaiomba sana taasisi haya mambo ambayo wanayaweka hapa katika vitabu vyetu angalau tuone utekelezaji wake, angalau si chini ya asilimia 40 isiwe mambo yanajirudia kila siku katika vitabu na yakawa pambo katika maeneo haya ya vitabu hivi ambavyo vinaletwa hapa mbele yetu.

Mhe. Spika, nakwenda katika kifungu cha 45 kinachohusu masuala ya michezo. Hapa kuna maeneo muhimu ambayo yamepewa kipaumbele maalum, lakini vile vile niwapongeze sana wizara chini ya waziri wake, swahibu wangu Mhe. Said Ali Mbarouk, lakini nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa na ya busara ambayo amekwisha kuifanya hatimae ikapelekea ujenzi ambao sasa hivi tunauona wa uwanja wa *Mao-Tse-Tung*, ambao tayari shughuli na harakati zake zimeanza.

Mhe. Spika, kiwanja kile hadithi yake ni ya muda mrefu lakini hatimaye sasa kweli imedhihiri na uwanja ule umeanza hatua za matengenezo na *Inshaallah* matengenezo yale yaende vizuri. Sisi kama wana jimbo la Kikwajuni tunaahidi kutoa mashirikiano ya hali na mali kuhakikisha kwamba ujenzi wa uwanja ule unafanikiwa na unasaidia, si watu wa Kikwajuni tu, lakini na wa maeneo yaliyo karibu na jimbo la Kikwajuni Zanzibar, Tanzania na dunia kwa ujumla.

Isipokuwa Waswahili wana msemo, "Mcheza kwao hutunzwa", yale mambo ya msingi, yale mambo ambayo anahisi Mhe. Waziri yanaweza yakafanywa na wana Kikwajuni wenyewe naomba asisite kutuomba na tuko tayari kushirikiana naye kuhakikisha kwamba tunakamilisha kazi hii nzito ambayo imeasisiwa na Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, tukiondoka hapo nakwenda katika kifungu cha 61. Kifungu hiki kinaelezea Idara ya Habari Maelezo. Pamoja na mikakati ya uimarishaji wa eneo hili la habari maelezo, siridhiki na namna taasisi hii inavyoweka kumbukumbu za

hotuba za viongozi wetu wakuu ambao wapo katika madaraka au wale ambao wamekwishakuondoka katika madaraka. Naomba sana juhudi zifanyike, ili zile kumbukumbu kwanza ziwepo kwa ukamilifu lakini pia zitunzwe ili vizazi vitakavyokuja viweze kuja kusikia, kuona na kupata kujua historia ya nchi yao.

Kwa sababu katika dunia mambo mawili kwa mtu yeyote lazima awe nayo, la kwanza kujua jiografia ya nchi yako na la pili kujua historia ya nchi yako. Kwa hiyo, naomba kwa kupitia katika taasisi hii kumbukumbu zile zienziwe vizuri na kama kuna bajeti ambayo ni finyu Mhe. Waziri kwa kutumia uwezo wake aliyonao ndani ya wizara kukaa na watendaji wake watengeneze utaratibu ambao utasaidia kutunza kumbukumbu na historia zile ili vizazi vinavyokuja viweze kuneemeka na kufaidika, isiwe kama sasa hivi ambapo tumekwenda kule kuna baadhi ya kumbukumbu haziwezi kupatikana tena kutokana na uhifadhi mbovu uliyoko katika taasisi ile. Naomba sana hili Mhe. Waziri walizingatie pamoja na taasisi yake.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika kifungu cha 65 Shirika la Magazeti ya Serikali. Zanzibar ni nchi ambayo ina historia katika suala zima la magazeti yale Kweupem Kumekucha, mpaka sasa hivi kuna Zanzibari Leo. Ningeliomba sasa, kwa vile Zanzibar tunaitangaza kama ni nchi yenye kutegemea utalii zaidi hawa watalii wanayo haki ya kujua taarifa zetu na kwa bahati mbaya sana lugha ambayo tunaizungumza sisi miongoni mwao wako ambao hawaijui.

Mhe. Waziri wakati umefika sasa na hili nataka alipe kipaumbele cha aina yake tufike pahala sasa Zanzibar tutoe magazeti yanayozungumza lugha ya Kiingereza, ili wageni wetu wanaofika hapa wafaidike na taarifa zetu na mambo yetu yanayoendelea katika nchi yetu. Namuomba hilo Mhe. Waziri aende akalifanyie kazi vile vile.

Nikiondoka katika ukurasa huu nakwenda kifungu cha 84 cha kitabu hiki. Kifungu cha 84 cha kitabu hiki kinazungumzia juu ya suala zima la Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie, katika historia ya nchi hii na katika kuenzi kumbukumbu za Mapinduzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar basi sisi Hoteli ya Bwawani ni moja kati ya kielelezo cha Mapinduzi yetu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Ningeliomba Mhe. Waziri atapokuja hapa atufahamishe hasa hatma na mwelekeo wa serikali juu ya Hoteli ya Bwawani ni nini? Nataka Mhe. Waziri akija hapa anisaidie, anielezee ili niondokane na wasiwasi na hofu niliyonayo juu ya kielelezo kile cha Mapinduzi yetu ya Zanzibar ambacho kimeasisiwa na baba yetu Marehemu Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, sasa nakuja ukurasa wa 90 wa kitabu chetu hiki, hapa kuna Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Mimi katika idara hii sipendi sana kuizungumza kwa sababu inanisikitisha sana, kama nilivyosema mwanzo nchi yoyote duniani mambo mawili ni ya msingi sana, jiografia na historia, majumba haya ya kumbukumbu yamekuwa ni majengo tu sasa hivi katika Zanzibar yetu, vile viashiria, vile vitu ambavyo vinazungumzia kumbukumbu ya Zanzibar vingi havipo a vingi havikutunzwa vizuri na matokeo yake wenzetu katika nchi nyengine wanafaidika navyo.

Je, ni nini mwelekeo wa serikali katika kuwasaidia vizazi vyetu vinavyokuja juu ya suala zima la kumbukumbu na mambo ya kale, ambayo itakuwa ni kielelezo sahihi kwa ajili ya kutambua utamaduni, silka na mila zao ndani ya nchi zao ambazo watoto hawa watakuwa wamezaliwa. Mhe. Waziri tunamuomba atakapokuja hapa atusaidie hilo.

Mhe. Spika, nakwenda kifungu cha 93 Baraza la Kiswahili, Tanzania kwa kupitia Zanzibar kwa sababu Kiswahili hasa penyewe ni Zanzibar, tumepata bahati ya kwamba Kiswahili kianze kutumika duniani na hususan katika Umoja wa Kitaifa. Kuna *facility* nyingi sana Tanzania na Zanzibar imepewa katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili.

Je, haya mambo yamefikia wapi mpaka sasa hivi, mbona kishindo kilikuwa kikubwa na hatimaye sasa hivi mambo yote yamelala je, kulikoni Mhe. Mhe. Waziri katika kukusa hihi Baraza letu la Kiswahili. Naomba Mhe. Waziri atapokuja hapa atusaidie.

Mwisho si kwa ulazima katika kifungu cha 58 cha kitabu hiki naomba kwa mara nyengine tena niwashukuru, niwapongeze, ndugu zetu wa *ZBC* pamoja na changamoto nyingi walizonazo lakini bado wanasaidia kwa namna fulani harakati na uwezekano wa kuweza kupatikana taarifa muhimu yakiwepo Matangazo ya vifo, asubuhi yale mawio, lakini kubwa zaidi taarifa za habari zinapatikana katika *ZBC* yetu na kwa kweli tunafarihika, tunafurahika na tunafuatilia kwa karibu sana katika mambo hayo, Inshaallah Mwenyezi Mungu akuwezesheni sasa kwa sababu haya mambo yote yanataka fedha na fedha katika taasisi yetu hii ni haba mno.

Mhe. Spika, nilikuweko nje hapo nimepata bahati ya kukaa na Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hii tunazungumzia maendeleo nini changamoto hasa, nini kifanyike ili tuweze na sisi kuw akama vyombo vyengine vya habari. Ananambia Mhe. Mwenyekiti bwana wenzetu ambao wana vyombo vya habari wana mitambo tu wamenunua mtambo mmoja una-*cost* shilingi 31 milioni, sisi tunanunua vifaa kwa shilingi milioni moja tutaweza vipi kushindana nao tukiangalia hali yetu,

tukiangalia na keki yetu tuliyonayo wanayoyazungumza watendaji wetu yana usahihi ndani yake.

Naomba basi Mwenyezi Mungu atujaalie tufike pahala tupate uwezo mzuri tuwezeshe taasisi zetu hizi na sisi tuwe kama walivyo wenzetu ambao wana uwezo mzuri wa kifedha na hatimaye tunyanyue taasisi yetu na iwe kuliko hizo nyengine ambazo zinaendelea.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nimalizie kwa kusema kwamba, naiomba sana serikali hususan kupitia Wizara ya Fedha kile chuo cha masuala ya utangazaji hebu wapewe hizi shilingi 30 milioni ule ujenzi uendelee pale Kilimani Baa. Naiomba sana serikali, waziri namuomba kwa kusaidiana na Waziri wa Fedha nipate maelezo ni lini serikali itatoa hizi shilingi 30 milioni ili kile chuo pale palipokuwa Kilimani Baa kitaanza ujenzi wake na hatua za utekelezaji wa masuala haya yaweze kuanza mara moja.

Baada ya maelekezo hayo mimi sitokuwa na buti nzito sana katika taasisi hii isipokuwa eneo moja tu ambalo nimekwishakuliainisha. Kama sikupata maelezo yatakayoweza kuniridhisha mimi na hao ambao tunawatetea hapa shughuli itakuwepo kama wenzangu walivyosema, lakini nataka kujua mustakabali mzuri wa masuala haya. Baada ya maelezo hayo naunga mkono bajeti ya wizara hii kwa asilimia mia moja na nawatakia funga njema ya Ramadhani. Mhe Spika, ahsante sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa na mpaka muda huu tukaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Pia nakushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa fursa bila ya kuleta karatasi.

Mhe. Spika, mimi nampongeza Mhe. Waziri kwa kitabu chake hiki ambacho kimejaza mambo yote tunayoyahitaji. Mimi nitaanza mchango wangu ukurasa wa 5 kifungu cha 14 Sekta ya Utamaduni.

Mhe. Spika, utamaduni uko mwingi sana, kuna utamaduni wa kivazi, utamaduni wa michezo, lakini hasa utamaduni mkubwa katika nchi ni wa lugha. Lugha yetu sisi ni ya Kiswahili lakini bado lugha ya Kiswahili hatujaweza kuitilia nguvu hasa, hata wale wenzetu wageni wakaja tukaweza kuzungumza nao Kishwahili.

Muingereza anapokuja hapa anatamani sana kuzungumza Kiswahili lakini sisi Waswahili hatuthamini tunakwenda kuzungumza Kiingereza, lakini sisi tukienda Uingereza Waingereza wana hamu wafundishe Kiingereza kwa sababu ndio utamaduni wao, lakini sisi haturidhiki kukithamini Kiswahili mbele ya mgeni.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba Kiswahili ndio utamaduni wetu na kithaminiwe. Hata pale uwanja wa ndege tukifika Muingereza aelekezwe Darajani kwa Kiswahili ndio atajua kwamba Waswahili wanathamini lugha yao.

Vile vile utamaduni mwengine wa kivazi; mmasai ana utamaduni wake wa kuvaa rubega hata akienda katika mkutano wa Umoja wa Mataifa anavaa rubega kwa sababu ndio utamaduni wake na ndipo atapojulikana hasa kama Mmasai. Sasa na sisi Wazanzibari tuwe na utamaduni wa kivazi, lakini sasa leo utamkuta kijana yuko Darajani pale kavaa kaawoshi anatoka Matemwe mpaka Darajani mjini kavaa fulana tupu haina shati, haina chochote, ndio utamaduni gani ule, ule sio utamaduni wetu. Mimi naufahamu utamaduni wa kivazi chetu hapa tunavaa kanzu, kofia, koti na kikowi, Mzanzibari huyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba utamaduni unatumika vilivyo.

Wakati wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume wanapokuja watalii anawawekea nguo pale za kizanzibari, haingii Mzungu kavaa kisuruali mpaka mapajani yuko uchi hapa kwa sababu sio utamaduni wetu, utamaduni wetu unawekwa pale anawekewa nguo na kila kitu anaambiwa sasa hivi ingia katika nchi kwa sababu utamaduni wa huku sio kuvaa vikaawoshi utamaduni wa huku wa kuvaa nguo watu wakajistiri mwili wao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba uwanja wa ndege, bandarini, pawekwe nguo za utamaduni wetu, wageni wakija wahakikishe kwamba wanavaa nguo za utamaduni wetu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda kwenye Sekta ya Utalii ukurasa wa 6 kifungu cha 20. Tuna mahoteli ya utalii yametuzunguka hasa kule kwetu mashamba Mkoa wa Kaskazini, Mkoa wa Kusini na humu mna watu wa aina mbali mbali, mna wafanyakazi, mna wapeleka *tender*, *tender* ni wapelekaji wa biashara. Mahoteli haya wakati wananchi wanapopeleka *tender* zao wanapata tabu malipo na wengine masikini mifuko yao wanakopa na wanaweza kufika miezi saba hawajapewa chochote. Kwa hivyo, naiomba wizara jambo hili ilifuatilie sana katika mahoteli, wenye mahoteli wanawanyanyasa sana wananchi wanaopeleka *tender* kwa kuwanyima malipo yao.

Mhe. Spika, sasa nakwenda katika ukurasa wa 9 kifungu cha 28, Sekta ya Michezo. Mhe. Spika, tuna michezo ya aina mbali mbali; tuna michezo ya mipira, ngoma na ndio utamaduni vile vile. Kwa hivyo, ili kukuza michezo wizara iwape kipaumbele hawa watu wa michezo. Kuna wasanii ambao ndio kioo cha nchi na ndio wanaoitangaza nchi katika midola mengine. Kwa hivyo, naomba serikali kupitia Wizara hii ya Habari wasanii watunze, watu wa michezo watunzwe. Leo tuna timu zetu za mpira, ziko chini sana katika kiwango. Kwa hivyo, ili kwa kukuza huu mchezo lazima Serikali kupitia Wizara yake ya Habari na utamaduni tuhakikishe kwamba wanatunzwa wanamichezo pamoja na wasanii.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nasafiri mpaka ukurasa wa 13 kifungu cha 42 Sekta ya Habari na Utangazaji. Wajumbe wengi wamezungumza juu wa watangazaji wafanyakazi. Kama kazi kubwa baada kazi ya kijeshi na hii kazi ya habari nayo ni kubwa sana. Kwa sababu mwandishi wa habari popote pale anapotakiwa mwanajeshi na yeye muandishi wa habari awepo, kama anapigwa risasi mwanajeshi basi na muandishi apigwe risasi, kwa sababu ya kutafuta bahari na habari lazima zipatikane, kwa sababu habari ndizo silaha ya kulinda nchi.

Kwa hivyo, Mheshimiwa hawa waandishi wa Habari lazima na wao watizamwe. Kuna waandishi wengine humu wanajitolea kwa muda wa miaka 6,7,8. Kujitolea kuna kiasi, kwa sababu mtu anajitolea yuko katika hali ya umasikini, hajitolei kwa sababu tajiri anajitolea miaka 6 miaka 5. Kwa hivyo, atizamwe na aajiriwe kama yeye mfanyakazi halali na awe anapata haki zote za kifanyakazi. Mtu akijitolea tu kunaumiza.

Kwa hivyo, na wao serikali kupitia Wizara ya Habari na Utangazaji, lazima hawa wafanyakazi waangaliwe kwa sababu mimi nafikiri hapa hawa wafanyakazi wetu, kutwa hawa mimi kusimama kama anavyosimama yule siwezi. Kwa hivyo yule anasimama kuanzia asubuhi saa tano mpaka saa mbili kasorobo; ni kazi kubwa sana. Kwa hivyo, lazima serikali iwaangalie wafanyakazi hawa. Mhe. Spika, mimi kama nilivyokueleza sina mchango mkubwa.

Mhe. Spika, mimi nitakwenda kidogo katika mambo ya kale; historia jambo zuri katika nchi nalo linapendezesha na hata hao wageni wanaokuja wanapenda sana kujua historia ya mambo yaliyotokea. Kuna mambo ya zamani kama majengo ya zamani. Kwa hivyo, wale wageni wetu hupenda kuangalia.

Kwa hivyo, ningeliomba wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo itafute sehemu zote zile za historia waziorodheshe, ili wazitunze ili wale watalii watakapokuja pale waone hata kama kuna wazee wa zamani waliofika miaka mia basi wanaweza kuwapeleka pale, kwa sababu mtu akifika miaka mia mbili, mia tano inakuwa historia. Kwa sababu yule ikiwa atatunzwa ndie atakaeijua historia ya nchi na ndie atakaeulizwa kuanzia mwaka 1800 pametokezea kitu gani, pametokea kitu kadhaa na kadhaa.

Kwa hivyo, ni moja katika mtu ambaye ni wa kutumzwa, ni historia. Kwa sababu wengine wanasoma katika kitabu wengine wanasoma kupitia wazee husikia humu, waandishi wa habari wanapita katika kijiji wanauliza kijiji hiki asili yake nini kwa mfano mtu atakuja Matemwe, hebu tupe mzee, hebu tupe nini maana ya Matemwe. Sasa akija pale atamkuta mtoto, lakini tukija kama sisi ma- *baby* basi tutatoa tu historia.

Sasa Mhe. Spika, hawa watunzwe kama Mzee wangu Kingunge hapa ukienda kule Mtambile ukimkuta huyu Mzee Kingune ataulizwa hebu twambie hapa Mtambile kwa nini pakaitwa Mtambile. Sasa kama huyu atatunzwa ndie atakaetoa historia. Lakini sasa kama huyu atatupwa hakuna atakaejua historia. Kwa hivyo, naimba serikali kupitia wizara hii wazee kama Mzee Kingunge lazima watunzwe na ndio watakaotoa historia ya nchi.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumza mimi sina mchango mkubwa kwa sababu Wajumbe wote wameshachangia. Kwa hivyo, naiunga mkono Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari na utangazaji. Lakini namkumbusha Mhe. Waziri kina Mzee Kingunge hawa ni wa kutunzwa na ndio wanaotoa historia ya nchi. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Hivi Mzee Kingunge leo kaja hapa? nilifikiri yule mzee wa CCM. Nakushukuru Mhe. Abdi Mosi Kombo kwa mchango wako huo.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru kwa michango yenu na inaelekea tumefikia pahali pazuri na ndio maana Waheshimiwa Wajumbe wengi wanafikia kusema kwamba hili limeshachangiwa na hili limeshachangia na kanuni haipendi sana kurudia rudia. Lakini tunao muda na Mhe. Waziri pale anasema anahitaji akazungumze na kunongona na watendaji wake, ili aje afafanue vizuri sana jioni.

Lakini kwa muda huu uliopo tunaweza tukapata kitu kidogo nacho ni kumuomba Mhe. Waziri wa Minundo mbinu na Mawasiliano aje, ili aweze kuwasilisha na jioni tufanye majumuisho ya hii na hatimae tuendelee na mjadala wa hii. Naona huo muda usipotee potee ovyo. Haya Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MIUNDOMBINUNA MAWASILIANO KWA MWAKA 2015/2016

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, tulikuwa tunatarajia sana Mhe. Waziri anaposoma na sisi tuwe na vitabu tuangalie wapi paku- *point,* ili tuweze kuchangia vizuri lakini nahisi hivi vitabu bado hatujapewa.

Mhe. Spika: Watendaji leteni vitabu haraka. Mheshimiwa endelea, vitabu vinaletwa

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati, ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara Miundombinu na Mawasiliano, kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kukutana leo hii kuwasilisha na kujadili Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushauri na miongozo anayoipatia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Mhe. Spika, napenda pia kuwashukuru Makamu wa kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kwa hekima katika kutekeleza majukumu mazito ya kitaifa.

Aidha, naomba kumpongeza kwa dhati Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa kuongoza na kusimamia vyema shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, napenda pia kukupongeza wewe binafsi kwa hekima, umahiri na busara unazozitumia katika kuliongoza Baraza lako Tukufu ambalo limekua likifanya maamuzi muhimu na magumu kwa manufaa ya nchi yetu.

Aidha, pongezi zangu za dhati Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kukusaidia wewe Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kazi nzuri ya uchambuzi wa kina wa taarifa za utekelezaji wa sekta na maelekezo na ushauri katika mpango wa bajeti ya Wizara ambao umeisaidia sanaWizara katika kukamilisha maandalizi ya bajeti tunayoiwasilisha.

Mhe. Spika, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba uniruhusu kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilipangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 5.678 kwa kazi za kawaida na TZS bilioni 8.350 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS bilioni 3.717zimepatikana kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 65 ya bajeti. Aidha, jumla ya TZS bilioni 6.023kwa kipindi hicho zimepatikana kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 72 ya bajeti.

Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizarailipangiwa kukusanya jumla ya TZS milioni 426 na hadi kufika Machi 2015, TZS milioni 315.276 zimekusanywa sawa na asilimia 74 kwa mwaka (Kiambatanisho nambari 1).

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kisekta kupitia, Idara, Mamlaka na Mashirika yaliomo ndani ya Wizara, taasisi binafsi na baadhi ya taasisi za Muungano kama ifuatavyo:-

Ofisi Kuu – Pemba

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba imeendelea kuratibu na kusimaimia kazi zote za wizara kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2014- 2015, Ofisi Kuu – Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 1.339, na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS milioni 930.637zimepatikana sawa na asilimia 70 kwa makadirio ya bajeti.Aidha, Ofisi Kuu – Pemba ilipangiwa kukusanya mapato yenye jumla ya TZS milioni62,nahadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS milioni 42.426 sawa na asilimia 68 zimekusanywa.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha miezi tisa kilichoanzia Julai 2014 hadi Machi 2015 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeendelea nausimamizi wa shughuli mbali mbali za kiofisi, maslahi ya watumishi pamoja na kujenga uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali ya muda mrefu na mfupi ya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuleta ufanisi katika utendaji kazi(Kiambatanisho namba 2).

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilitengewa kutumiajumla ya TZS bilioni 3.292; na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS bilioni 2.273 zimepatikana sawa na asilimia 69 za makadirio ya bajeti.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeendelea na kazi za uratibu wa sera na mipango ya Wizara pamoja na kusimamia miradi ya maendeleo ya Wizara. Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Idara imesimamia jumla ya miradi ya maendeleo 14 ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege,

bandari pamoja na mageuzi ya taasisi. Hatua za utekelezaji wa miradi hiyo zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Miradi ya Sekta ya Usafiri wa Anga

Mradi wa Ujenzi wa Maegesho na Njia ya Kupitia Ndege katika uwanja wa ndege Karume

Mhe. Spika, Mradi huu uliokuwa na lengo la kujenga maegesho na njia ya kupitia ndege katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume umekamilikamwezi wa Disemba 2014 na kufunguliwa rasmi mwezi wa Januari, 2015.

Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria

Mhe. Spika, Ujenzi wa Jengo jipya la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume unaoendeleana umefikia asilimia 32 ya utekelezaji ambapo kazi za uwekaji wa nguzo za vyuma zimekamilika. Aidha, kazi za ujenzi wa paa, ukuta wa nje (*curtain wall*), uwekaji wa miundombinu ya umeme, vipoza hewa pamoja na mabomba ya maji zinaendelea. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS bilioni 1.950 na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS billioni2.797sawa na asilimia 143 zimepatikana kwa ajili ya malipo ya msimamizi wa ujenzi na malipo ya fidia.

Mhe. Spika, kwa vile fedha zilizotengwa kwenye mradi huu zilikuwa kidogo kuliko mahitaji halisi ya madai ya Mshauri Elekezi, Wizara imelazimikakuhaulisha TZS milioni 847 kutoka vifungu vyamiradi mengine ya maendeleo ilikuhakikishamradi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria unaendelea kwa kiwango kinachohitajika.

Mradi waUjenzi wa Uzio katika Kiwanja cha Abeid Amani Karume

Mhe. Spika, jumla ya kilometa 8.89 za uzio zimekamilika hadi Machi 2015. Kilometa 2.8 zilizobakia zinatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka 2015/2016. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 975 na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS milioni 250 zimepatikana sawa na asilimia 25.64.

Mradi wa Uimarishaji wa Kiwanja cha Ndege Pemba

Mhe. Spika, Mradi huu unajumuisha uwekaji wa taa za kuongozea ndege wakati wa kutua na kuruka *AGL* pamoja kufanya upembuzi yakinifu katika kiwanja cha

ndege cha Pemba. Hatua za awali kwa ajili ya uwekaji wa taa katika kiwanja cha ndege cha Pemba zinaendelea ambapo kazi ya utengenezaji wa taa hizo umeanza sambamba na hatua za uchimbaji kwa ajili ya ulazaji wa nyaya za taa. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi miwili ijayo.

Miradi ya Sekta ya Usafiri wa Baharini

Mhe. Spika, katika kuimarisha sekta ya usafiri wa baharini, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kipindi cha 2014/2015 imetekeleza miradi ifuatayo:-

Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri

Mhe. Spika, hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa bandari ya Mpigaduri ni kukamilika upembuzi yakinifu pamoja na uchambuzi wa athari za kimazingira (*EIA*). Wizara pia imewasilisha nyaraka zote zinazohitajika *Exim Bank* ya China kazi yakuzifanyia tathmini inaendelea. Serikali kupitia mamlaka zenye dhamana ya kufuatilia fedha zinaendelea kuwasiliana na Serikali ya China kwa ajili ya kukamilisha taratibu za upatikanaji wa rasilimali fedha. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 500 na hadi kufikia Machi 2015 hakuna fedha iliyopatikana.

Mradi wa Ujenzi wa Meli mpya ya Abiria na Mizigo ya Serikali;
Mhe. Spika, ujenzi wa meli ya MV Mapinduzi II unaendelea vyema na ukokatika hatua za mwisho kukamilika. Meli hiyo inaendelea kufanyiwa vipimo namajaribio ya baharini *(Inclining tests experiment &Sea trials*)pamoja na majaribio mengine muhimu ya vifaa na mitambo viliomo katika meli hiyo. Kama mambo yatakwenda vizuri katika vipimo na majaribio hayo meli hiyo itaanza safari kutoka Korea ya Kusini hadi Zanzibar tarehe 25 Juni 2015 na kuwasili Zanzibar wiki ya mwisho ya mwezi Julai, inshaallah 2015 kwa mujibu wa ratiba iliyopo.

Miradi ya Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu

Mhe. Spika, katika kuimarisha sekta ya usafiri wa nchi kavu, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imetekeleza miradi ifuatayo kwa kipindi cha mwaka 2014/2015.

Mradi wa Ujenzi wa Barabara Tatu za Pemba
Mhe. Spika, Mradi huu unaojumuisha barabara za Wete-Konde na Wete-Gando zenye urefu wa kilomita 30.2 umekamilika mwezi Machi 2015. Kwa mwaka wa

fedha 2014/2015, mradi huu ulipangiwajumla ya TZS bilioni 2.425 na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS bilioni 2.424 zimepatikana sawa na asilimia 100.

Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Wete-Chake

Mhe. Spika, Mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha baada ya kukamilika awamu wa mwanzo ya mradi ikiwa taratibu za upatikanaji wa mkopo kutoka *Saud Fund* zitakamilika. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya TZS milioni 100 zimetengwa na hadi kufikia Machi 2015 hakuna fedha iliyopatikana.

Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Ole-Kengeja

Mhe. Spika, Ujenzi wa barabara ya Ole-Kengeja yenye urefu wa kilomita 35 unaendelea kwa hatua mbalimbali ikiwemo upimaji (kilomita 11), usafishaji wa barabara (kilomita 9) pamoja na uwekaji wa kifusi cha awali (kilomita 5). Aidha, taratibu za ununuzi wa vifaa vya ujenzi zimekamilika na tayari baadhi ya vifaa hivyo ikiwemo Buldoza moja (1), Sagamawe moja(1) na magari manne (4) makubwa vimeshawasili - Pemba katika eneo la ujenzi. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS milioni 500 na hadi kufikia Machi 2015 hakuna fedha iliyopatikana.

Mradi wa Barabara zinazoingia Mjini Unguja

Mhe. Spika, hatua ya utekelezaji wa mradi huu ni kuwa Serikali imefanya mazungumzo na washirika wa maendeleo mbalimbali kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi. Tayari Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*kwa hatua za awali (*technical*) imekubali kugharamiaujenzi wa barabara moja, Bububu – Mahonda –Mkokotoni (kilomita 31), kati ya barabara saba ambazo zimo katika mradi huu.Kwa sasa Serikali inasubiri idhini ya bodi ya Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kuendelea na hatua zaidi.

Mradi wa Ujenzi wa Barabara Tatu za vijijini Unguja

Mhe. Spika, mradi huu unajumuisha barabara ya Jendele-Cheju-Kaebona (kilomita 11.7) na Koani-Jumbi (kilomita 6.3) unaendelea. Hatua iliyofikiwa ya ujenzi ni kukamilika kwa tabaka la pili la kifusi kwa barabara ya Jendele-Cheju-Kaebona (kilomita 11.7). Aidha, matayarisho ya uwekaji lami kwa barabara hiyo yameanza. Kwa upande wa barabara ya Koani-Jumbi (kilomita 6.3) kazi ya uwekaji kifusi cha mwanzo imeanza. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 1.6 na hadi kufikia Machi2015 jumla ya TZS milioni 551.669 zimepatikana sawa na asilimia 34.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 200 kwa kazi za kawaida na TZSbilioni 8.350 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS milioni 86.798 zimepatikana sawa na asilimia 43 kwa kazi za kawaida. Kwa upande wa kazi za maendeleo jumla ya TZS bilioni 6.023 zimepatikana sawa na asilimia 72.

Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB)
Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara imeendelea kuzijenga na kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali Unguja na Pemba**.** Hadi kufikia mwezi Machi 2015, Idara kupitia Mfuko wa Barabra imekamilisha ujenzi wa barabara ya Amani – Mtoni (kilomita 4) na barabara ya Njia Nne - Umbuji (kilometa 5). Kwa upande wa matengenezo ya kawaida ya barabara, Idara imezifanyia matengenezo barabara mbali mbali Unguja na Pemba, kama inavyoonekana kwenye **(Kiambatanisho namba 3).**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara hii ilipangiwa jumla TZS milion 165.488 kwa matumizi ya kawaida na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS milioni 65.337 zimepatikana sawa na asilimia 39.

Idara ya Usafiri na Leseni

Mhe. Spika, Idara ya Usafiri na Leseni imefanya ukaguzi wa vyombo vya moto na kutoa leseni za njia na usafirishaji pamoja na ruhusa za njia kwa magari ya biashara. Idara imewafanyia mitihani ya nadharia na vitendo madereva wanafunzi pamoja na kutoa vyeti vya umahiri kwa madereva waliofaulu mitihani hiyo**(Kiambatanisho namba 4).**

Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, jumla ya vyombo vya moto 228 vimefanyiwa matengenezo kupitia Karakana Kuu na sehemu ya Mitambo Pemba. Kati ya hivyo, 85 ni magari ya Serikali na 143 magari ya watu binafsi. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ilipangiwa kutumia TZS milioni 200.585 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS milioni 73.644 zimepatikana sawa na asilimia 37 ya makadirio. Aidha, Idara imepangiwa kukusanya jumla ya TZS milioni 364.00 na kukusanya jumla ya TZS milioni 272.85 sawa na asilimia 75.

Idara ya Mawasiliano

Mhe. Spika, Idara ya Mawasiliano imesimamia na kuimarisha huduma za teknolojia ya habari na mawasiliano hapa Zanzibar.Kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Idara imefanya matengenezo ya mkonga wa taifa maeneo yalioharibika katika barabara ya Tunguu –Istiqama, Kiwengwa, Paje na Nungwi Unguja. Kwa upande wa Pemba hatua za matengenezo zinaendelea katika maeneo mbali mbali kama vile Machomane, Wete, Kwale, Kizimbani, Kiungoni na Kifumbikai zimekamilika. Aidha, uwekaji *'Alarm System'* kwenye vituo vyote 12 vya mkonga vilivyopo Zanzibar umefanyika ili kuvilinda na kuviwezesha kutoa taarifa Makao Makuu pale maharibiko ya aina yoyote yatakapotokezea.

Mhe. Spika, kuhusu uunganishwaji wa Mkonga kwenye taasisi za Serikali, hadi kufikia Machi 2015, taasisi 84 tayari zimeunganishwa na mkonga kwa kushirikiana na Kampuni ya *Zantel*, ikiwa taasisi 50 zinatumia huduma hiyo na taasisi 34 zipo katika hatua za mwisho za kuwekewa vifaa husika ili nazo ziweze kutumia huduma hii. Wizarakwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ya SMT imeweka mitambo ya mawasiliano picha *(Video Conference)* katika sehemu 5 tofauti Unguja na Pemba na mitambo hiyo inafanya kazi. Aidha, Wizara kwa kushirikia na Kampuni ya *ZTE* ya China imefunga *computer 50* kwa ajili ya Kituo Jamii cha *TEHAMA* katika skuli ya Kiembe Samaki na kuunganishwa na mkonga wa Taifa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Mawasiliano ilitengewa kutumia jumla ya TZS milioni 179.53; na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZS milioni 62.63 zimepatikana sawa na asilimia 35 za makadirio ya bajeti.

Mamlaka ya Viwanja vya ndege

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea na kazi zake za msingi za kuviendesha, kuvisimamia, na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali pamoja na kutoa huduma na usalama kwa safari za abiria na mizigo katika viwanja vya ndege vya Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 Mamlaka imetoa huduma mbalimbali kwa abiria na mizigo**(Kiambatanisho nambari 5).**

Mhe. Spika, **k**wa upande wa miradi midogo midogo ya uimarishaji wa Kiwanja cha Ndege cha Unguja, Mamlaka imefanya yafuatayo:-Ujenzi wa kipaa (*canopy*) kwa ajili ya abiria wanaowasili umeanza. Aidha, matengenezo ya sehemu ya kuondokea abiria wa ndani *(domestic passengers)* katika jengo la huduma *(service building)* yamekamilika kwa asilimia 100 na kuanza kutumika.

Mhe. Spika, kutokana na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali kuimarisha viwanja vya ndege kumekuwa na ongezeko la abiria na Mashirika ya ndege yanayotumia viwanja hivyo. Shirika la ndege la *Fly Dubai* tayari limeanzisha safari zake kuja Zanzibar. Aidha, *Qatar Airways* wamethibitisha kuanza safari zao rasmi tarehe 1 Julai, 2015, na mashirika ya *Turkish Airways* na *Egypt Air* wao wameonesha nia ya kuanza safari zao kuja Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege -Zanzibar ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya TZS bilioni 6.2. Hadi kufikia Machi 2015, jumla ya TZS bilioni 4.9 zimekusanywa na kutumika kati ya fedha hizo jumla ya TZS bilioni 3.7 zilitumika kugharamia kazi za kawaida na TZS bilioni 1.2 zilitumika kwa kazi za maendeleo.

Kwa mwaka wa fedha 2015/16 Mamlaka inakadiria kukusanya jumla ya TZS bilioni 5.7 kupitia vyanzo vyake vya ndani na kutumia jumla ya TZS bilioni 6.7 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Nakisi ya bajeti itajazwa kupitia vyanzio vya nje vya mapato.

Shirika la Bandari
Mhe. Spika, Shirika la Bandari limehudumia meli katika Bandari za Unguja na Pemba pamoja na kusimamia usalama wa usafiri ndani ya maeneo ya bandari hizo. Kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi, 2015, Shirika limehudumia jumla ya meli za Kigeni 144 zenye uzito *wa GRT 1,914,246*, meli za ndani 2,927 pamoja na vyombo vya kienyeji 3,283. Aidha, Shirika limehudumia jumla ya tani 145,226 za mzigo mchanganyiko na makontena 44,601 pamoja na mzigo wa majahazi tani 106,934. Kwa upande wa abiria, jumla ya abiria 1,805,208 wa ndani na nje 5,190 wamehudumiwa hadi Machi, 2015**(Kiambatanisho nambari 6).**

Mhe. Spika, kuhusu kazi za kiufundi, Shirika limebadilisha maboya 14 na maboya 3 ya *solar* yamebadilishwa katika bandari za Pemba. Shirika pia limeyafanyia matangenezo maboya saba(7) ya *Solar* pamoja na kuunda maboya matatu (3) yasiotumia taa kwa ajili ya Bandari ya Mkokotoni. Mhe. Spika,kwa upande wa miradi ya maendeleo ya Shirika kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, jumla ya miradi saba (7) imetekelezwa kwa hatua mbali mbali kama ifuatavyo:-

Matengenezo ya Sakafu ya Eneo la Kuhifadhi Makontena Bandarini Malindi

Kazi ya kuweka sakafu ya zege pamoja na *"paving blocks"* imeendelea, ambapo jumla ya TZS milioni 404.60 zimetumika. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya robo ya nne 2014/2015.

Ununuzina Ufungaji wa Taa za *Solar*

Mhe. Spika, Shirika limekamilisha ununuzi na ufungaji wa taa katika minara mikubwa minane (8) ya Unguja na Pemba ambapo taa hizo zinafanya kazi kama kawaida. Mradi huu utagharimu Dola za Kimarekani 725,768 ambazo zitalipwa kwa awamu ndani ya kipindi cha miaka 7. Hadi kufikia Machi, 2015 Shirika limelipa jumla ya TZS milioni 150.02.

Ununuzi wa Tagi Kubwa

Mradi huu umekamilika na kugharimu jumla ya *EURO* milioni 4.7 sawa na TZS bilioni 10.3. Kwa ujumla hadi kufikia Machi 2015 Shirika tayari limelipa jumla ya TZS bilioni 4.8 kugharamia mradi huo.

Ujenzi wa Gati Ndogo ya Mkokotoni na Tumbatu

Mhe. Spika, Shirika limekamilisha kazi ya utafiti wa kimazingira (*EIA*) katika maeneo ya Mradi na kazi ya ujenzi wa Gati ya Tumbatu inaendelea. Ujenzi wa gati ndogo ya Mkokotoni unategemewa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2015/16. Hadi kufikia Machi 2015, Mradi huu umetumia jumla ya TZS milioni 43.60

Mradi wa Uvunjaji wa Mabanda Bandarini Malindi na Kuweka Sakafu

Mhe. Spika, mradi huu umekamilika kwa uwekaji sakafu ya zege eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 1,400 na tayari eneo limeanza kutumika. Jumla ya TZS milioni 148.77zimetumika kukamilisha Mradi huo.

Ununuzi wa Vifaa vya Kunyanyulia Mizigo Bandarini

Mhe. Spika, zabuni kwa ajili ya ununuziwa Kreni 2, *Terminal Tractor 2, Traillar 2, Reach stacker 2, Fork lift 3* na *Empty Handler 1* zimetolewa.

Matengenezo ya Mnara wa Kigomasha

Shirika limekamilisha matengenezo ya Mnara wa Kigomasha. Kazi hiyo imegharimu jumla ya TZS milioni 98.52.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TZS bilioni 19.81. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya TZSbilioni17.795 zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 89.83 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TZSbilioni 16.22 kwa

kazi za kawaida na maendeleo na hadi kufikia Machi 2015 jumla ya TZSbilioni 11.48 zimetumika sawa na asilimia 70.78 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2015/2016, Shirika limepanga kuhudumia meli 190 za kigeni zenye uzito (*GRT*) wa tani milioni 2.71, Meli za ndani 4,000 na Majahazi 5,000 pamoja na kuhudumia mizigo mchanganyiko yenye uzito wa tani 120,000 na makontena 60,000 (sawa na TEUs 77,027).

Kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Shirika linakusudia kuikamilisha miradi iliyoanzishwa mwaka wa fedha unaomalizika. Pia, Shirika litafanya matengenezo makubwa ya minara ya Chumbe, Makunduchi, Pungume, matengenezo ya Gati ya Wete, ujenzi wa *Beacon* za Wete na Wesha, uimarishaji wa kituo cha mnara wa Kigomasha pamoja na uimarishaji wa ulinzi na usalama (ununuzi wa *CCTV na X-Ray Machine*) kwa ajili ya hapo gatini Malindi.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Shirika limekadiria kukusanya jumla ya TZS bilioni 26.97 na kutumia jumla ya TZS bilioni 19.99.

Shirika la Meli na Uwakala
Mhe. Spika,Shirika la Meli na Uwakala limeendelea kutoa huduma za usafiri wa baharini kati ya Visiwa vya Unguja na Pemba, pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni zinazoingiakatika bandari za Zanzibar. Shirika pia, limeendelea kutoa mchango wa kitaalamu katika ujenzi wa meli mpya ya abiria na mizigo ya Serikali unaoendelea nchini Korea ya Kusini.

Kwa upande wa usafirishaji wa abiria na mizigo**,** katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015**,** meli ya MV Maendeleo imefanya safari 76 baina ya visiwa vya Unguja na Pemba na kuhudumia abiria wapatao 85,117 na tani 18,284 za mizigo.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho, Shirika limekusanya jumla ya TZS bilioni 4.91 sawa na asilimia 74 ya makisio ya mwaka na kutumia jumla ya TZS bilioni 3.95 sawa na asilimia 69. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Shirika linatarajia kukusanya jumla ya TZS bilioni 13.308 kutokana na vianzio vyake vya mapato na kutumia jumla ya TZS bilioni 12.303.

Mamlaka ya Usafiri Baharini
Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri imeendelea kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli. Kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Mamlaka imefanya zoezi maalum la udhibiti wa uuzaji wa tiketi za magendo na utumiaji wa vitambulisho wakati wa

ununuzi wa tiketi na uingiaji bandarini Unguja na Pemba. Mamlaka imesajili meli saba (7) zenye uzito wa jumla *GRT 3347* kwa usajili wa ndani (*Tanzania Zanzibar Registry).* Mamlaka kupitia Kampuni ya *Philtex Corporation* iliyopo Dubai ilisajili jumla ya meli 65 zenye uzito wa jumla *GRT5,783,519.72* kabla ya mkataba na kampuni hiyo kusitishwa rasmi tarehe 13/10/2014**(Kiambatanisho nambari 7).**

Mhe. Spika, Mamlaka imetoa leseni za usajili kwa vyombo vidogo vidogo 70, vitabu vya mabaharia *(Discharge Book)* 377, vitambulisho vya kimataifa vya mabaharia vitatu (3) na leseni tatu (3) za manahodha na uhandisi *(Boat Master Licences & Boat Engineer licences).*Pia, Mamlaka imethibitisha mikataba 116 ya mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia Kampuni ya *DANAOS*.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Mamlaka ilikagua meli 36 ambazo ni sawa na GT 15,240. Kati ya hizo, kaguzi za chelezoni zilikuwa ni meli 4 sawa na GT 2,749 na kaguzi za mwanzo zilikuwa meli 7 ambazo ni sawa na GT 377. Katika ukaguzi wa kiusalama Mamlaka ilifanya ukaguzi wa meli 21 ambazo ni sawa na GT10, 156 kwa upande wa kaguzi za dharura zilikuwa 4 ambazo ni sawa na GT 1958.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilikadiria kukusanya jumla ya TZS bilioni 1.38 na ilikadiria kutumia jumla ya TZS bilioni 1.36 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2015 jumla ya TZS bilioni 1.421 zimepatikana sawa na asilimia 103 ya makadirio ya mwaka, na kutumia jumla ya TZS bilioni 1.33 sawa na asilimia 97 ya makadirio ya mwaka. Matumizi hayo yanajumuisha uanzishaji wa Ofisi Mpya ya Mamlaka nchini *UAE*. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka imekadiria kukusanya TZS bilioni 2.127 na kutumia jumla ya TZS bilioni 2.127 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mashirikiano na Taasisi za Muungano

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Usafiri na Mawasiliano. Miongoni mwa Taasisi za Muungano tunazoshirikiana nazo ni:- Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (TCAA), Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (TMA), Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (TCRA), Shirika la Posta la Tanzania (TPC) na Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). Mashirikiano na Taasisi yamechangia sana kukuza Sekta ya Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

C. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyoelezwa katika utekelezaji wa kazi zetu kwa mwaka 2014/2015, kumekua na changamoto kadhaa ambazo zilisababisha utekelezaji wa baadhi ya kazi zetu kuwa ngumu. Changamoto hizo ni;

- Uhaba na uchakavu wa zana zinazotumika katika ujenzi na utunzaji wa barabara;
- Upungufu wa rasilimali fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- Ukosefu wa vifaa vya kisasa na jengo la kufanyia ukaguzi wa vyombo vya moto;
- Ukosefu wa sheria na kanuni katika kusimamia huduma na miundombinu ya mawasiliano;
- Uvunjaji mkubwa wa sheria za usafiri wa barabarani;
- Utegemezi mkubwa wa washirika wa maendeleo katika kutekeleza miradi ya maendeleo; na
- Kutuwama kwa maji kwenye baadhi ya maeneo ya barabara zetu na eneo la nje la uwanja wa ndege kutokana na ufinyu wa miundombinu (Mitaro) ya kupitishia maji ya mvua.

D. MWELEKEO WA MATUMIZI YA BAJETI INAYOTUMIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kila Idara, Mamlaka na Mashirika yaliyomo ndani ya Wizara kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, sasa kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inayotumia programu kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, s-erikali imeamua kufanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma. Mageuzi hayo ni kutoka mfumo wa sasa wa bajeti unaotumia vifungu (*line item*) kwenda katika mfumo unaotumia programu (*Program Based Budget-PBB*). Kama ilivyoelezwa katika matoleo mbalimbali ya Serikali, mageuzi ya bajeti inayotumia mfumo huu yatapelekea ufanisi katika kutatua changamoto zinazoikabili bajeti ya Serikali kwa sasa. Inategemewa kuwa kuingia katika mageuzi hayo ya mfumo wa bajeti italeta uwiano mzuri katika kutekeleza Dira ya Zanzibar 2020, MKUZA II na mwendelezo wake, Sera ya usafiri Zanzibar, Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano pamoja na sera mbali mbali za Taifa. Aidha, mfumo wa programu

utaiwezesha Wizara kuweka malengo yake kwa uwazi zaidi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inasimamia programu kuu nne zifuatazo:-

- Programu ya kwanza: Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara;
- Programu ya pili: Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya Ndege;
- Programu ya tatu: Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEHAMA*); na
- Programu ya nne: Mipango na Utawala katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatarajia kutumia jumla ya TZS bilioni 189.108 kwa programu zote nne ikiwa kati ya fedha hizo, TZS bilioni 171.695 ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya ujenzi wa Barabara na Viwanja vya ndege na TZS bilioni 17.414 ni kutoka Serikalini ambapo jumla TZS bilioni 5.514 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na jumla ya TZS bilioni 11.90 ni mchango wa Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara.

D.1 PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRI WA BARABARA

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri wa barabara zilizobora, salama na endelevu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni uwepo wa miundombinu imara na huduma bora katika sekta ya Usafiri wa barabara. Aidha, programu hii inatekeleza lengo la ukuaji wa uchumi na kupunguzau maskini wa kipato Zanzibar.

Mhe. Spika, Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara inasimamiwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (*UUB*), Idara ya Usafiri na Leseni na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Jumla ya TZS bilioni 33.621 zimepangwa kutumika kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa programu hii, ikiwa ni sawa na asilimia 17.8 ya matumizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, Kati ya fedha hizo jumla ya TZS bilioni 24.996 ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa barabara na Jumla ya TZS bilioni 8.625 ni kutoka Serikalini ambazo zitatumika kwa matumizi ya kawaida pamoja na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara za Wete – Konde

na Wete – Gando, Wete – Chake, Ole – Kengeja, Jendele – Cheju – Kaebona na Koani – Jumbi, Bububu –Mahonda - Mkokotoni, Matemwe – Muyuni, Pale – Kiongele na Fuoni - Kombeni ikiwa ni mchango wa Serikali.

Mhe. Spika, Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara inasimamia programu ndogo mbili zifuatazo:-

(1a) Ujenzi na Matengenezo ya Barabara; na
(1b) Usimamizi wa Usafiri wa Barabara.

D.1.1 Programu ndogo ya Ujenzi na Matengenezo ya Barabara

Mhe. Spika, Programu ndogo ya kwanza – (1a) Ujenzi na Matengenezo ya Barabara, ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara kwa kuzijenga na kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za Unguja na Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa katika programu hii ndogo ni utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, na matengenezo mbali mbali ya barabara ikiwemo usafishaji wa barabara, usafishaji mitaro, ujenzi wa madaraja na makalvati, uzibaji wa viraka, uwekaji wa kifusi na lami na uwekaji alama na michoro mbali mbali ya barabarani.

Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 33.043 kati ya fedha hizo jumla ya TZS bilioni 24.996 ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo na jumla ya TZS bilioni 8.047 ni kutoka Serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

D.1.2 Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafiri wa Barabara

Mhe. Spika, Programu ndogo ya pili – (1b) Usimamizi wa Usafiri wa Barabara, ina lengo la kupatikana huduma bora za usafiri wa barabara zilizo salama kwa Unguja na Pemba. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ni usimamizi wa utoaji wa huduma za usafiri wa barabara, usimamizi wa usalama barabarani pamoja na matengenezo ya vyombo vya moto. Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 577.7 kutoka Serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

D.2 PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA BANDARI NA VIWANJA VYA NDEGE

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya Viwanja vya Ndege na Bandari. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni kuwepo kwa miundombinu na huduma za usafiri wa baharini na anga. Aidha,

programu hii inatekeleza lengo la ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato nchini.

Mhe. Spika, Programu ya Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya Ndege inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Shirika la Bandari, Shirika la Meli na Uwakala na Mamlaka ya Usafiri Baharini. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 152.357 sawa na asilimia 80 ya Programu za Wizara. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS bilioni 146.557 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na jumla TZS bilioni 5.80 ni kutoka serikalini. Fedha hizo ni kwa ajili ya Mradi wa Bandari ya Mpigaduri, Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria, Ujenzi wa Uzio, Uwekaji wa Taa katika Kiwanja cha ndege cha Pemba pamoja na huduma za usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, Programu ya Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya Ndege inasimamia programu ndogo mbili ambazo ni:-

(2a) Miundombinu ya Viwanja vya Ndege; na
(2b) Miundombinu ya Bandari na Usimamizi wa Usafiri wa Baharini.

D.2.1 Programu ndogo ya Miundombinu ya Viwanja vya Ndege

Mhe. Spika, Programu ndogoya kwanza – (2a) Miundombinu ya Viwanja vya Ndege, ina lengo la kuwepo miundombinu ya viwanja vya ndege inayotunzwa salama na endelevu. Programu hii inatarajiwa kutoahuduma mbili kuu ambazo ni: Uimarishaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume kwa kujenga jengo jipya la abiria na kukamilisha ujenzi wa uzio katika kiwanja hicho.

Aidha, huduma ya pili inayotolewa na programu hii ndogo ni Uimarishaji wa kiwanja cha ndege cha Pemba kwa ajili ya uwekaji wa taa za kuongozea ndege (*AGL*) pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa huduma mbali mbali za kiwanja hicho.

Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 151.457. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS bilioni 146.557 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na jumla ya TZS bilioni 4.90 ni kutoka Serikalini.

D.2.2 Programu ndogo ya Miundombinu ya Bandari na Usimamizi wa Usafiri wa Baharini

Mhe. Spika, Programu ndogo ya pili – (2b) Miundombinu ya Bandari na Usimamizi wa Usafiri wa Baharini, ina lengo la kuimarisha miundombinu ya bandari na huduma za usafiri wa baharini. Programu hii inatarajiwa kutoa huduma

kuu mbili ambazo ni kuimarisha huduma za bandari ikiwemo ujenzi wa bandari ya Mpigaduri na usimamizi wa usafiri wa baharini. Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 900 kutoka Serikalini kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mpigaduri na huduma za usafiri wa Baharini.

D.3 PROGRAMU YA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Lengo la programu hii ni kuhakikisha huduma bora na zenye kuendelea za Technolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEHAMA*) zinapatikana kwa muda wote hapa nchini. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana ni kuwepo kwa huduma bora za *TEHAMA* - Zanzibar.

Mhe. Spika, Programu ya Huduma ya Technolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEHAMA*) inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama vile Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) na Shirika la Posta. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 262.382 sawa na asilimia 0.14 ya Programu za Wizara. Fedha hizi ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mhe. Spika, Programu ya Technolojia ya Habari na Mawasiliano inasimamia programu ndogo mbili ambazo ni:

(3a)Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano; na

(3b)Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano.

D.3.1 Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano

Mhe. Spika, Programu ndogo ya kwanza – (3a) Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano, ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu imara ya *TEHAMA* nchini. Huduma zinazotarajiwa kutolewa katika programu hii ni usimamizi wa miundombinu ya mawasiliano ikiwemo kufanya ukaguzi wa mkonga, usimamizi na ukaguzi wa minara ya mawasiliano pamoja na kusamabaza na kuufanyia matengenezo mkonga wa mawasiliano wakati athari zitakapoonekana. Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 84.646 kutoka Serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

D.3.2 Programu ndogo ya Usimamizi wa huduma za Mawasiliano

Mhe. Spika, Programu ndogo ya pili – (3b) Usimamizi wa huduma za Mawasiliano, ina lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za *TEHAMA* zilizo salama. Huduma zinazotarajiwa kutolewa katika programu hii ni kuratibu na upatikanaji wa huduma za *TEHAMA* kwa jamii. Miongoni mwa shughuli ambazo

zinatarajiwa kufanyika ni kuendelea na uratibu wa uwekaji wa anuani za makaazi (*postcode*), kuanzisha vituo vya kutoa huduma na mafunzo ya *TEHAMA* kwa jamii. Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 177.736 kutoka serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

D.4 PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA KATIKA SEKTA YA USAFIRI NA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Progamu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa wizara inatayarisha mipango bora na usimamizi nzuri wa rasilimali watu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni kuwepo mipango bora na uendeshaji mzuri wa shughuli za utawala na utumishi katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano.

Mhe. Spika, Programu ya Mipango na Utawala inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi; Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; na Ofisi Kuu Pemba. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 2.869 sawa na asilimia 1.52 ya Programu za Wizara; ikiwa kati ya fedha hizo jumla ya TZS milioni 141.855 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na jumla ya TZS bilioni 2.727 ni fedha kutoka serikalini. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na Mradi wa Mageuzi ya Muundo wa Wizara.

Mhe. Spika, Programu ya Mipango na Utawala inasimamia programu ndogo tatu ambazo:-

(4a)Utawala na Uendeshaji**;**
(4b)Mipango na Sera katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano; na
(4c)Uratibu shughuli za Wizara Pemba.

D.4.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji

Mhe. Spika, Programu ndogo ya kwanza – (4a) Utawala na Uendeshaji**,** ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano**.** Huduma zinazotarajiwa kutolewa katika programu hii ni upatikanaji huduma mbali mbali za kiutawala na utumishi katika Wizara. Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 986.230 kutoka Serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

D.4.2 Programu ndogo ya Mipango na Sera katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano

Mhe. Spika, Progaramu ndogo ya pili – (4b) Mipango na Sera katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano, ina lengo la kuhakikisha mipango na sera mbalimbali za Sekta ya Usafiri na Mawasiliano inatayarishwa na kufuatilia utekelezaji wake. Huduma ambayo zinatarajiwa kutolewa katika programu hii ni kupanga, kuratibu

na kusimamia shughuli za Wizara ikiwemo kuandaa na kusimamia bajeti ya Wizara, sera, miradi ya maendeleo, ufuatiliaji wa kazi za Wizara pamoja na kuratibu tafiti za Sekta ya Usafiri na Mawasiliano.

Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS milioni 476.548. Kati ya fedha, jumla ya TZS milioni 141.855 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na jumla ya TZS milioni 334.693 ni kutoka serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

D.4.3 Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Spika, Programu ndogo ya tatu – (4c) Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba, ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa kwa upande wa Pemba. Huduma inayotolewa katika programu hii ni uratibu wa kazi za Wizara Pemba ikiwemo kusimamia shughuli za utawala na utumishi, mipango na bajeti, huduma za usafiri wa Barabarani, huduma za *TEHAMA* pamoja na ujenzi na matengenezo ya Barabara mbali mbali kwa upande wa Pemba. Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS bilioni 1.406 ambazo zote ni kutoka Serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

E. HITIMISHO

Mhe. Spika, Kabla ya kumaliza hotuba yangu sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuendelea kutekeleza majukumu yake na kutatua changamoto mbali mbali zilizojitokeza katika kipindi kilichopita na hatimae, kuipitisha bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, Shukurani za dhati ziende kwa Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia (*WB*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (*BADEA*), Benki ya Exim ya China, Saudi *Fund*, Mfuko wa Maendeleo ya Nchi zinazotoa Mafuta Duniani (*OFID*) na wengine wote ambao wanasaidia kutoa huduma za usafiri hapa nchini, ikiwemo Mashirika ya Serikali na binafsi kwa kuendelea kutuunga mkono katika kuimarisha sekta ya usafiri na mawasiliano kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu, Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka kwa ushirikiano alionipa katika kipindi kifupi ambacho nimekuwa naye wizarani. Vile vile, nampongeza Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil pamoja na Naibu Katibu

Mkuu Ndugu Tahir M. K. Abdullah, Wakurugenzi, Watendaji Wakuu wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ushirikiano na juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, natoa shukurani kwa wadau wote wa Sekta ya Usafiri na Mawasiliano pamoja na Makampuni na Mashirika mbali mbali ya ndani na nje ya nchi yanayotoa huduma katika Sekta ya Usafiri. Michango ya makampuni na mashirika hayo yamesaidia sana kutoa huduma mbali mbali za usafiri na mawasiliano hapa Zanzibar. Shukurani za pekee nazitoa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wake wote kwa kuchapisha vizuri hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba pia nitoe shukurani zangu za dhati kuishukuru familia yangu kwa kuniunga mkono, kunistahamilia na kunipa moyo muda wote katika kutekeleza kazi zangu.

F. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/ 2016

Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya TZS 189,108,700,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2015/2016 kwa utekelezaji wa kazi zilizoainishwa katika programu nne za Wizara ikiwa:-

- Matumizi ya kawaida kutoka Serikalini ni TZS 5,514,100,000;
- Matumizi kwa kazi za maendeleo kutoka Serikalini ni TZS 11,900,000,000; na
- Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 171,694,600,000.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Usafiri wa Barabara inayotekelezwa na Idara ya Usafiri na Leseni imepangiwa kukusanya jumla ya TZS 1,169,873,000 kwa mwaka 2015/2016 kwa Unguja na Pemba kupitia huduma wanazozitoa.

Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe makusanyo hayo ya TZS 1,169,873,000 kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa heshima zote naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

***KIAMBATANISHO NAMBA 1*: MUHTASARI WA MAKADIRIO YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWAIDA, MAENDELEO NA MAPATO KWA KIPINDI JULAI 2014 – MACHI 2015**

SEHEMU A: MATUMIZI YA KAWAIDA

KASMA	MATUMIZI HALISI 2013/2014	MAKADIRIO 2014/2015	FEDHA HALISI JULAI 2104- MACHI 2015			ASILIMIA
			MISHAHARA/ MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA	%
0301 OFISI KUU PEMBA	1,149,556,686	1,339,001,000	809,637,300	121,000,000	930,637,300	70
0901 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	2,731,720,720	3,292,814,000	1,996,491,101	276,716,739	2,273,207,840	69
IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI	117,618,270	200,585,000		86,798,000	86,798,000	43
IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA	103,661,842	165,488,000		65,337,000	65,337,000	39
IDARA YA USAFIRI NA LESSENI	76,865,499	200,585,000		73,644,000	73,644,000	37
IDARA YA MAWASILIANO	90,551,000	179,527,000		62,616,000	62,616,000	35

MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI	238,000,000	300,000,000		225,000,000	225,000,000	75
JUMLA	**4,507,974,017**	**5,678,000,000**	**2,806,128,401**	**911,111,739**	**3,717,240,140**	**65**

KASMA	MAKADIRIO 2014/2015	FEDHA ZILIZO PATIKANA JULAI-MACHI 2014/2015	ASI LIMIA %
0301 PEMBA	3,025,000,000	2,424,000,000	80
0401 MIPANGO	3,725,000,000	3,047,500,000	81
0701 UUB	1,600,000,000	551,669,479	34
JUMLA	**8,350,000,000**	**6,023,169,479**	**72**

KASMA	MAPATO HALISI 2013/2014	MAKADIRIO 2014/2015	FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI-MACHI 2014/2015	ASILIMIA %
0301 PEMBA	54,244,000	62,000,000	42,426,000	68
0701 UUB	6,650,000			
0801 LESENI	349,946,800	364,000,000	272,850,000	75
JUMLA	**410,840,800**	**426,000,000**	**315,276,000**	**74**

KIAMBATANISHO NAMBA 2

SEHEMU A: WAFANYAKAZI WALIOPATA MAFUNZO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2014/2015:

	SHAHADA YA UZAMILI		STASHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA YA KWANZA		STASHAHADA YA JUU		DIPLOMA		CHETI	
	M/KE	M/ME	M/KE	M/ME	M/KE	M/ME	M/KE	M/ME	M/KE	M/ME	M/KE	M
TUMISHI	2	2	-	1	1	-	-	-	9	-	-	-
A UTAFITI	-	2	1	-	-	-	-	-	-	-	-	-
	-	1	-	-	-	2	-	-	1	-	-	-
I	-	1	-	-	1	1	-	-	3	1	-	-
AJI BARABARA	-	-	-	-	1	2	-	-	-	1	-	5
	1	2	-	-	1	3	-	-	3	2	2	1
	3	**8**	**1**	**1**	**4**	**8**	**-**	**-**	**16**	**4**	**2**	**6**

SEHEMU B: MASOMO YA MUDA MFUPI

IDARA	W/KE	W/ME	JUMLA
UENDESHAJI NA UTUMISHI	2	5	7
MIPANGO, SERA NA UTAFITI	2	6	8
MAWASILIANO	-	5	5
USAFIRI NA LESENI	-	3	3
UJENZI NA UTUNZAJI BARABARA	2	7	9
AFISI KUU PEMBA	1	7	8
JUMLA	**7**	**33**	**40**

KIAMBATANISHO NAMBA 3:

KAZI ZA MATENGENEZO YA BARABARA UNGUJA NA PEMBA – JULAI 2014 –MACHI 2015

AINA YA MATENGENEZO.	KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015.	KAZI HALISI ILIYOFANYIKA KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015.
Matengenezo ya kawaida ya barabara (Routine Maintenance paved)	Kukata majani, kuchonga mabega, kusafisha misingi na Culvert/Madaraja kwa kutumia wafanyakazi wa Idara.	Ukataji wa majani umefanyika barabara ya Mkwajuni – Matemwe 32,700m2,Mshelishelini- Pwanimchangani 31,950m2, Tunguu-Makunduchi 64,935m2, Dunga- Chwaka 43,200m2, Kaebona – Unguja - Ukuu 49,700m2, Jozani- Muyuni 56,000m2, Kibuteni-Muyuni 29,250m2, Chake – Wete 300,000m2,Konde – Kiuyu cha manda 40,000m2, Chanjaani – Melinne 40,000m2, Mbuguani – M'Port 20,000m2, Kilindini – Micheweni 60,000m2, M'port – Ngomeni School 3,600m2, Mkoani – Makombeni 40,000m2, Bogoa – Michezani 30,000m2, M'geni – Shidi 22,000m2, kukata na kiziba mashimo 1230m2 kwa barabara za Pemba.
	Kuziba mashimo barabarani (1200m2) na 222 m3 kwenye barabara mbalimbali za Mjini na vijijini.	Barabara ya Amani- U/ndege eneo la Makutano ya barabara na kuelekea Kiembesamaki (60m2) na kuweka kifusi 4m3 eneo la Saateni.
Matengenezo ya kawaida ya barabara za kifusi (Routine Maintenance for unpaved roads)	Kufanya matengenezo ya barabara kwa kiwango cha kifusi katika maeneo mbalimbali.	Uwekaji wa kifusi kwenye sehemu korofi pamoja na kuchonga kwa maeneo ya Kwakisasi-Bububu school 19,000m2, Nyaugusu - Kijitoupele 17,500m2, Donge – Muwanda, Fuoni – Kwarara.
	Kufanya matengenezo ya barabara kwa kiwango cha kifusi katika maeneo mbalimbali.	Hakuna kazi iliyofanyika katika matengenezo ya barabara ya Kama - KMKM 12,500m2.
	Uchangiaji wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Uzi-Ng'ambwa (2.5km)	Uwekaji wa kokoto barabarani (250m) na majaribio ya ujenzi wa barabara kwa zege (50m).

AINA YA MATENGENEZO.	KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015.	KAZI HALISI ILIYOFANYIKA KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015.
Matengenezo ya muda maalum barabara za Lami (Periodic Maintenance Paved)	Matengenezo ya Barabara ya M/kwerekwe - Makaburini - Fuoni meli tano 1.7 km na Tomondo Magereza-Mchina mwisho 1.5km, Bumbwini – Kiongwe 4.5 km, Ole – Konde kwa kiwango cha lami. Matengenezo ya barabara ya Gamba -Kikobweni (5.3km) kwa kiwango cha lami nyepesi yalifanyika.	Ununuzi wa lami tani 160 na maandalizi ya zabuni ya kumpata Mkandarasi wa kujenga barabara kwa kiwango cha Kifusi yanaendelea.
	Matengenezo ya barabara mbali mbali kwa muda maalum ulivyopangwa.	Matengenezo ya barabara za Njia nne Umbuji 5km, Amani Mtoni 0.8 km, Kiswandui – Wailess – Kikwajuni 0.8 km, Chukwani – Buyu 0.9km, Michezani – Mtendeni 0.9 km, Kikobweni – Gamba, na Pandani – Mlindo. Kuchonga na kuweka kifusi kwa barabara ya Wesha – Mkumbuu 2km na Pandani Mlindo 2km
Matengenezo ya Sehemu korofi (Sport improment Maintenance).	Matengenezo ya barabara kwa maeneo korofi kwa barabara za Unguja na Pemba.	Kuwekwa lami na kufanya matengenezo ya sehemu zilizoharibika pamoja na kujengwa kiko za Zege kwa maeneo yaliyoathirika kwenye barabara ya Chake – Mkoani na eneo la kwa Changawe.
Matengenezo ya Mitaro, Madaraja na Makalvat (Drainage Works).	Ujenzi wa drifty, kalvati kasha mbili, ujenzi wa kuta kwenye kalvati ya bati Mtoni – Kidatu na Chake Mkoani kwa kutomea mawe na saruji kwenye msingi.	Ujenzi wa vizuizi vya mmomonyoko wa ardhi (scour checks) kwenye mtaro sehemu ya Mtoni Kidatu, kutomea mawe kwa saruji (stone pitching) kwenye baadhi ya sehemu za mtaro (200m) pamoja na ujenzi wa kuta kwenye kalvati ya bati. Matengenezo yalifanyika kwa mitaro ya barabara ya Chake – Mkoani 400m pamoja na kujengwa kwa mawe na saruji pamoja na kalvat kasha moja kwa barabara ya Mgagadu – Kiwani. Ujenzi wa kalvat kasha na uwekaji wa kifusi 200m umekamilika kwa barabara ya Kiuyu – Ngomeni.
Matengenezo ya dharura	Matengenezo ya dharura yanayojitokeza nje ya Mpangokazi wa mwaka.	Matengenezo ya barabara kwa maeneo ya Micheweni – Kiuyu, Kuyuni – Ngomeni, Jonza – Micheweni – Shumba mjini yamefanyika pamoja na ununuzi wa Transformer mpya ya Umeme Kibele.

AINA YA MATENGENEZO.	KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015.	KAZI HALISI ILIYOFANYIKA KWA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015.
Alama mbalimbali za usalama barabarani (Road safety)	Uwekaji wa alama mbalimbali za barabarani (roa safety) na uwekaji wa Viguzo vya hifadhi ya barabara za Unguja na Pemba.	Kuliwekwa viguzo vya hifadhi ya barabara kwa barabara ya Njia Nne – Umbuji 4.5 km, Kuweka michoro ya barabara ya Amani – Mtoni 4 km kumekamilika.
Uwekaji wa taa za kuongezea Magari kwenye Makutano ya Barabara	Uwekaji wa Taa za Sola na CCTV Camera kwenye makutano ya Barabara ya Mkunazini, Mchinamwanzo na Malindi.	Uwekaji wa Taa kwenye makutano ya Barabara Mchina mwanzo na Mkunazini umekamilika.
Shughuli shirikishi / Mtambuka (Cross cutting issues)	Shughuli zinazosaidia katika kufanikisha kazi za kila siku kwa Idara kama vile matengenezo ya mbali mbali ya mitambo, zana nzito, magari pamoja na gharama za uendeshaji wa miradi.	Kulifanyika upandaji wa miti kwa maeneo ya barabara ya Mkwajuni – Nungwi 18.3km. Kulifanyika ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto na mafunzo ya huduma ya mwanzo. Kulifanyika ununuzi wa vifaa vya huduma ya mwanzo na kinga kwa wafanyakazi (First aid kid).
RMMS Programe Unit	Mfumo wa Computer wa RMMS (Roads Inventory, Traffic Counts and Condition Survey, Allowances to RMMS staff na Stationaries).	Kulifanyika uimarishaji wa mfumo wa matengenezo ya barabara (RMMS) Roads Inventory, Traffic, Condition Survey, data entry, Stationaries na posho la watendaji wa kitengo cha mfumo wa komputa wa matengenezo ya barabara (RMMS).
Matengenezo ya Magari	Ununuzi wa Vipuri vya Zana, Mitambo na Magari yanayotumika katika kazi za matengenezo ya barabara.	Kulifanyika matengenezo ya mitambo na zana nzito pamoja na magari. Ununuzi wa matairi ya Grader na wheel loader pamoja na vipuri vya magari.
Posho la Watendaji na gharama za Uendeshaji.	Usimamizi wa kazi za matengenezo ya barabara na gharama za shughuli za Uendeshaji	Malipo yalifanyika kwa kuwapatia Maposho ya watendaji kwa safari za ukaguzi wa kazi za matengenezo ya barabara, Ununuzi wa pikipiki nne na mafuta ya ufuatiliaji shughuli za barabara kwa Pemba pamoja na ununuzi wa Vifaa vya kuandikia.

KIAMBATANISHO NAMBA 4

SEHEMU A: UKAGUZI WA VYOMBO VYA MOTO JULAI 2014 HADI MACHI 2015:

AINA YA VYOMBO	IDADI YA VYYOMBO VYA MOTO VILIVYOKAGULIWA						JUMLA
	UKAGUZI WA KAWAIDA		UKAGUZI WA SHAKA		UKAGUZI WA AJALI		
	UNGUJA	PEMBA	UNGUJA	PEMBA	UNGUJA	PEMBA	
GARI	14,680	1,475	73	32	690	40	16,990
MOTORCYCLE	13,009	2,158	0	2	174	15	15,358
JUMLA	**27,689**	**3,633**	**73**	**34**	**864**	**55**	**32,348**

SEHEMU B: RUHUSA ZA NJIA NA USAFIRISHAJI:

MAHALI ZILIPOTOEWA	AINA YA HUDUMA ILIOTOLEWA								
	Daladala	Shamba	P/Hire	Taxi	Mizigo	School	Staff	H/Drive	JUMLA
UNGUJA	404	244	589	158	382	16	28	64	1,875
PEMBA	40	185	01	13	121	0	0	0	357
JUMLA	**444**	**429**	**590**	**171**	**503**	**16**	**28**	**64**	**2,232**

SEHEMU C: TAKWIMU ZA MADEREVA WALIOJARIBIWA KUENDESHA VYOMBO VYA MOTO:

AINA YA MADEREVA	WALIOJARIBIWA KUENDESHA			WALIOFAULU KUENDESHA			WALIOFELI KUENDESHA		
	Gari	M/c	JUMLA	Gari	M/c	JUMLA	Gari	M/c	JUMLA
UNGUJA	2,462	1,534	**3,996**	1,867	1,432	**3,299**	531	102	**633**
PEMBA	936	1,104	**1,966**	646	786	**1,432**	259	331	**936**
JUMLA	**3,398**	**2,638**	**5,962**	**2,513**	**2,218**	**4,731**	**790**	**433**	**1,569**

SEHEMU D: UTOAJI WA LESENI KWA MADEREVA WANAFUNZI:

DARAJA	M	A	B1	B	C1	C	D1	D	E	G	JUMLA
UNGUJA	57	3,555	3,641	02	302	192	182	266	02	00	**8,199**
PEMBA	01	458	262	40	48	26	29	82	0	0	**946**
JUMLA	**58**	**4,013**	**3,903**	**42**	**350**	**218**	**211**	**348**	**2**	**0**	**9,145**

KIAMBATANISHO NAMBA 5

SEHEMU A: IDADI YA NDEGE ZILIZOHUDUMIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015:

AINA YA NDEGE	IDADI YA NDEGE 2013/2014		JUMLA	IDADI YA NDEGE 2014/2015		JUMLA
	UNGUJA	PEMBA		UNGUJA	PEMBA	
SCHEDULE	21,977	7,014	28,991	20,422	7780	28,202
CHARTER	15,257	268	15,525	17,744	576	18,320
CARGO	124	-	124	142	-	142
PRIVATE	421	-	421	137	-	137
MILITARY	38	-	38	8	-	8
OTHERS	636	66	702	1043	84	1127
JUMLA	**38,453**	**7,348**	**45,801**	**39,496**	**8440**	**47,936**

SEHEMU B: IDADI YA ABIRIA WALIOHUDUMIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI MACHI 2015:

KIWANJA	IDADI YA ABIRIA 2013/2014		JUMLA	IDADI YA ABIRIA 2014/2015		JUMLA
	INTERNATIONAL	DOMESTIC		INTERNATIONAL	DOMESTIC	
UNGUJA	302,460	366,344	668,804	307,487	367,354	674,841
PEMBA	19	58,328	58,347	8	69,532	69,540
JUMLA	**302,479**	**424,672**	**727,151**	**307,495**	**436,886**	**744,381**

SEHEMU C: KAMPUNI ZA NDEGE ZILIZOTUMIA KIWANJA CHA NDEGE CHA ABEID AMANI KARUME KWA MWAKA 2014/2015:

S/N	JINA LA KAMPUNI	VITUO	NCHI INAYOTOKA
1	Precision	Dar,Kilimanjaro,Mombasa,Nairobi	Tanzania
2	Coastal Travel	Zanzibar,Dar,Arusha	Tanzania
3	Zan Air	Zanzibar,Dar,Arusha	Tanzania
4	Ethiopian Airline	Addis- Ababa	Ethiopia
5	540 Aviation	Mombasa,Nairobi	Kenya
6	Fly Dubai	Dubai	Dubai
7	Meridian fly	Milan	Italy
8	Condor	Frankfut, Mombasa	Germany
9	Tui Airline	Brussels	Belgium
10	Travel Service	Budapest	Hungary
11	Neos Air	Milan	Italy
12	Oman Air	Muscat	Oman
13	Jet Air	Brussels, Mombasa	Belgium
14	Livingston	Milan, Mombasa	Italy
15	Arkefly	Amsterdam,Huhgada, Mombasa	Netherlands
16	Kenya Airways	Nairobi	Kenya
17	Fly Mango	Johannesburg	South Africa
18	Flight link	Dar,Zanzibar,Pemba	Tanzania
19	Auric Air	Dar,Zanzibar,Pemba	Tanzania
20	As salaam Air	Dar, Zanzibar, Pemba, Tanga.	Tanzania
21	Pelican Air	Dar,Zanzibar,	Tanzania
22	Regional Air	Dar,Zanzibar.	Tanzania
23	Safari Air Link	Dar,Zanzibar.	Tanzania
24	Shine Aviation	Dar,Zanzibar.	Tanzania
25	Tanzania Air	Dar,Zanzibar.	Tanzania
26	Tropical Air	Dar, Zanzibar, Pemba, Arusha .	Tanzania

27	Zenith Aviation	Dar, Zanzibar, Pemba.	Tanzania
28	Air Excel	Dar, Zanzibar, Arusha.	Tanzania
29	Astral Aviation	Kenya, Zanzibar.	Kenya
30	Twin Wings	Dar,Zanzibar.	Tanzania
31	Flying Doctor	Kenya ,Zanzibar	Kenya
32	Mass wood	Dar,Zanzibar.	Tanzania
33	Safari plus	Dar,Zanzibar.	Tanzania
34	Zantas Air	Dar,Zanzibar.	Tanzania
35	T.F.C	Dar,Zanzibar.	Tanzania
36	Northern Air	Dar,Zanzibar.	Tanzania
37	Z R P	Zanzibar,Dar.	Tanzania

KIAMBATANISHO NAMBA 6

SEHEMU A: HUDUMA ZA MELI:

S/NO	AINA YA MELI	KIPINDI		ONGEZEKO/ PUNGUZO (%)
		JULAI 2013 – MACHI, 2014	JULAI 2014 – MACHI, 2015	
1.	Meli za Nje	152	144	(5.26)
2.	Uzito wa Meli (GRT)	2,227,955	1,914,246	(14.08)
3.	Meli za Ndani	2,913	2,927	0.5
4.	Majahazi	4,617	3,283	(28.90)

SEHEMU B: HUDUMA ZA MIZIGO:

S/NO	AINA YA MIZIGO	KIPINDI		ONGEZEKO/ PUNGUZO (%)
		JULAI, 2013 – MACHI, 2014	JULAI, 2014 – MACHI, 2015	
1.	Mzigo mchanganyiko	49,363	145,226	194
2.	Makontena(TEUS)	44,276(57,704)	44,601(57,704)	0.73
3.	Mzigo wa Majahazi	116,802	106,934	(8.45)
4.	Abiria wa Ndani	1,776,101	1,805,208	1.64
5.	Abiria wa Kigeni	2,654	5,190	95.55

SEHEMU C: MAPATO NA MATUMIZI:

S/No	MAELEZO	JULAI, 2013-MACHI,2014	JULAI, 2014 – MACHI, 2015	ONGEZEKO/ PUNGUZO (%)
1.	Mapato (T.Shs)	14.60 Bln.	17.795 Bln.	**21.9**
2.	Matumizi (T.Shs)	10.470 Bln.	11.480 Bln.	**9.7**

KIAMBATANISHO NAMBA 7

SEHEMU A. MELI ZA NJE ZILIZOSAJILIWA KUANZIA JULAI 2014 – MACHI 2015:

	Official Number	Type of Vessel	IMO Number	GRT
	300465	Tug/Supply	8126991	1316
	300466	Oil Carrier Tanker	8808501	22607
	300271	General Cargo	7740491	2466
	300005	General Cargo	8872617	2576
	300130	Supply Vessel	9037537	616
	300166	Oil Tanker	9569700	165784
	300418	Oil Tanker	9569633	164796
	300468	Oil Tanker	9356593	164241
	300380	Oil Tanker	9187629	56068
	300267	General Cargo	8965141	202
	300294	General Cargo	7920338	664
	300375	Oil Tanker	9187643	56068
	300377	Oil Tanker	9569669	165784
	300376	Oil/ Chemical	9283758	25214
	300378	Oil Tanker	9569619	164796
	300069	Oil Tanker	9357365	85462
	300469	Oil Tanker	9171462	81479
	300470	Oil Tanker	9171450	81479
	300471	Oil Tanker	9357389	163660
	300101	Oil Tanker	9362061	163660
	300134	Oil Tanker	9187631	56068
	300221	Oil Tanker	9218478	160576
	300037	Oil Tanker	9212888	160930
	300371	Oil Tanker	9212929	160930
	300136	Supply Vessel	8447311	486
	300277	Landing Craft	7211464	625
	300086	LPG Carrier	7021887	6961
	300379	Oil Tanker	9218480	160576
	300381	Oil Tanker	9218492	160576

300382	Oil Tanker	9218466	160576	
300427	Oil Tanker	9569695	165784	
300089	Oil Tanker	9218454	160576	
300203	Cargo Ship	-	146.72	
300118	General Cargo	7126774	847	
300426	Oil Tanker	9569645	164796	
300135	Oil Tanker	9357377	85462	
300071	Oil Tanker	9569621	164796	
300198	Container	8997106	476	
300478	Oil Tanker	9212917	160930	
300161	Oil Tanker	9569671	165784	
300481	Oil Tanker	9569712	165784	
300480	Oil Tanker	9569657	164796	
300073	Crude Oil	9569205	164796	
300479	Oil Tanker	9357391	163660	
300207	Oil Tanker	9357183	163660	
300473	Oil Tanker	9357729	164241	
300475	Oil Tanker	9172038	81479	
300062	Oil Tanker	9187667	56068	
300068	Oil /Chemical	9283760	25214	
300103	Oil Tanker	9187655	56068	
300191	LPG	9615092	12216	
300474	Oil Tanker	9357717	164241	
300476	Oil Tanker	9172040	81479	
300477	Oil Tanker	9172052	81479	
300170	Oil Tanker	9079107	156809	
300373	Oil Tanker	9079092	156809	
300370	Oil Tanker	9357353	85462	
300374	Oil Tanker	9362059	163660	
300165	Crew Boat	9240603	102	
300187	Tug	9098385	242	

	300116	Tug /Supply Vessel	7366817	758	
	300230	General Cargo	7424061	1440	
	300011	Cargo Ship	8906767	5234	
	300233	Landing Craft Transport	7397361	485	
	300416	Oil Tanker	9053995	498	
				5,783,519.72	

SEHEMU B: MELI ZA NDANI ZILIZOSAJILIWA KUAZIA JULAI 2014 HADI MACHI 2015:

L	TYPE	YEAR OF BUILT	DATE OF REGISTRATION
	Coastal Dredging	Split Hopper Barge	19th Sept,. 2014
	TUG (AHTS)	1982	01ST DEC., 2014
	GENERAL CARGO	1990	01ST DEC., 2014
	BARGE	2015	19TH FEB, 2015
	TANKER LANDING CRAFT	2014	23RD FEB, 2015
	DREDGE BAEGE	2014	12TH MAR, 2015
	WORK BOAT	2014	12TH MAR, 2015

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na hoja imeungwa mkono. Muda uliopo naona hautoshi kumuomba Mhe. Mwenyekiti, aweze kuwasilisha maoni ya Kamati. Kwa sababu hiyo basi, naomba sasa tusitishe shughuli zetu na kuahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:45 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni leo)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea hoja hii iliungwa mkono naona humu ndani si mzuri vyema kwa sasa, tuendelee na ule mtindo wetu ambao anavyoanguka ndivyo hivyo hivyo atakavyochinjwa, kwa hivyo naomba sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Husein Ibrahim Makungu(Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba niisome hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Makadirio, Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru M/Mungu muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia uzima na afya njema kiasi cha kuweza kukutana tena katika mkutano huu wa mwisho wa Bajeti katika awamu hii ya saba inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt Ali Mohammed Shein kwa malengo ya kuwatumikia wananchi wetu waliotuchagua na taifa letu kwa ujumla.

Mhe. Spika, Pili napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2015/2016, Aidha napenda kumshukuru Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri na mashirikiano makubwa waliyotupa katika kipindi chote cha miaka miwili na nusu cha maisha ya kamati hii na hadi leo hii wanawasilisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu linaendelea kumkumbuka Marehemu Salmin Awadh Salmin kwa mchango wake mkubwa hasa katika mkutano kama huu wa bajeti kwani alikuwa ni mahiri sana katika kuchambua makadirio ya Bajeti kwa

Wizara mbali mbali hususan Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano, hivyo tunaendelea kumuombea kwa Allah amlaze mahali pema peponi Amin, sambamba na hilo nachukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wote walioathirika katika mvua kubwa zilizonyesha siku chache zilizopita hakika Serikali itachukua kila jitihada kuhakikisha kuwa waathirika hao wanarejea katika hali zao za kawaida za maisha.

Mhe. Spika, Kwa namna ya pekee sasa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano makubwa waliyonipatia wakati wote wa uhai wa Kamati yetu, hakika tulifanya kazi kwa pamoja hadi leo hii nawasilisha maoni ya Kamati kuhusu makadiro ya bajeti kwa wizara hii, Insha'Allah M/Mungu atatujaalia tutarudi tena kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar kwa umoja wetu. Kwani kwa hakika mashirikiano yao yamekuwa yakipelekea kazi zetu kufanyika kwa ufanisi wa hali ya juu. Hivyo naomba kuwatambua Wajumbe wenyewe kwa kuwataja majina kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
4.	Mhe. Marina Joel Thomas	Mjumbe
5.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mohammed Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	Mjumbe

Aidha Kamati yangu katika kutekeleza shughuli zake ilikuwa na makatibu wawili ambao wamekuwa wakishirikiana nasi kwa karibu sana katika kuratibu shughuli zetu mbali mbali za Kamati nao napenda kuwatambua kama ifuatavyo:-

1.	Ndg Maryam Rashid Ali	Katibu
2.	Ndg Saad Othman Saad	Katibu

Mhe. Spika. Kabla ya kuanza kutekeleza kazi iliyonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu ni vyema ikafahamika kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yangu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka kama ambavyo Kanuni ya 112(e) toleo la mwaka 2012 inavyoelekeza, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo la kikanuni, Kamati yangu ilichambua kwa umakini wa hali ya juu makadirio ya Wizara hii mnamo tarehe 07/05/2015 na leo hii nawasilisha maoni kwa niaba ya Kamati.

Mhe. Spika. Baada ya utangulizi huo sasa naomba uniruhusu kuanza kuchambua bajeti hii moja kwa moja, kama hivi ifuatavyo:-

KUHUSU BAJETI INAYOTUMIA PROGRAMU (PBB)

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza Serikali imewasilisha bajeti inayotumia mfumo wa Programu (*PBB*), ambayo kimsingi inalenga kwenye utoaji wa huduma na kuangalia matokeo yake, kimsingi mfumo huu bado ni mpya sana kwa wajumbe wa Baraza lako tukufu na unahitaji mazingatio makubwa zaidi ili kuweza kuuelewa, mfumo huu unaendeshwa kupitia Programu kuu na program ndogo.

Mhe. Spika, Wizara ya miundombinu na Mawasiliano katika Bajeti hii imepangiwa kuwa na program 4 zenye program ndogo ndogo kwa kila programu kuu. Programu zenyewe ni kama zifuatazo:-

1. Porgramu ya Miundombinu na Huduma za usafiri wa barabara.
2. Programu ya Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya ndege.
3. Programu ya Huduma za Teknologia ya Habari na Mawasiliano (*TEHAMA*).
4. Programu ya Mipango na Utawala katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano.

Porgramu ya Miundombinu na Huduma za usafiri wa barabara

Programu hii ina program ndogo 2 ambazo ni program ya ujenzi na Matengenezo ya Barabara na program ya usimamizi wa usafiri wa Barabara, Programu hii imepangiwa TZS Thelathini na tatu bilioni, mia sita ishirini Milioni, laki sita na sitini na nane elfu (33,620,668,000). Program hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri wa barabara zilizobora, salama na endelevu.

Mhe. Spika, Katika programu ndogo ya Ujenzi na Matengenezo ya Barabara ambayo imekasimiwa TZS Thelathini na tatu Bilioni, arobaini na mbili Milioni, laki tisa na thelathini na sita elfu (33,042,936,000). Kamati yangu imekuwa ikitafakari sana juu ya kasma hii na kuona kuwa kasma hii ni ndogo kutengwa kwa ajili ya program hii kwani program hii ina shughuli nyingi zinazohusiana na ujenzi wa barabara ambao kwa ujumla wake una changamoto nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ikiwemo fidia pamoja na madeni ya wakandarasi wa barabara hizo. Hivyo kwa kutengewa kiasi hichi cha fedha kamati yangu inaona malengo na shabaha hazitafikiwa na hatimae kubakisha mzigo wa madeni ya wakandarasi wa miradi ya barabara kwa Wizara.

Kuhusu Madeni Yanayotokana na Ujenzi wa Barabara

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa muda mrefu imekuwa ni wahanga wa madeni yanayotokana na miradi ya ujenzi wa barabara madeni ambayo yamekuwa yakiathiri bajeti yao kutokana na kulipia madeni ya nyuma badala ya kutekeleza mipango yao ya kibajeti waliyojipangia, nayasema haya kutokana na kamati yangu kushuhudia bajeti ya mwaka 2014/2015 kuwa finyu kwa kulipa madeni ya ujenzi wa barabara mfano wa mradi huo ni mradi wa ujenzi wa barabara tatu ambapo mkandarasi bado anaidai Serikali deni kubwa licha ya kukamilisha ujenzi wa barababra hizo hivyo kupelekea kuathiri bajeti ya Wizara.

Mhe. Spika, Kamati yangu katika utekelezaji wa Bajeti hii ya mwaka 2015/2016 inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuachana na utaratibu wa kutumika fedha za bajeti kulipia madeni ya nyuma, na badala yake Wizara ya Fedha iyachukue madeni ya miradi ya ujenzi wa Barabara na kuwa ni miongoni mwa madeni ya Mfuko mkuu wa Hazina ili bajeti hii itekeleze program ambazo Wizara imejipangia kwa lengo la kuleta matokeo yaliokusudiwa kwa wananchi kupitia programu hii, aidha kamati inashauri katika utekelezaji wa program hii kutosahau kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali ambazo hali yake hairidhishi hasa baada ya mvua kubwa zilizonyesha katika nchi yetu.

Mhe. Spika**, k**atika Programu ndogo ya usimamizi wa usafiri wa barabara iliyokasimiwa TZS Mia tano sabini na saba Milioni, Laki saba thelathini na mbili elfu (577,732,000). kamati yangu imekuwa ikishuhudia changamoto nyingi katika usafiri wa barabarani kunakopelekea ajali nyingi na kupoteza maisha ya wananchi, lakini bado usimamizi wa usafiri wa barabarani hauridhishi kutokana na kuwepo kwa changamoto nyingi kama vile kukosekana kwa kituo maalumu kwa ajili ya daladala kwani eneo ambalo kwa sasa kimekuwa ni kituo (Kisiwandui Makao Makuu ya CCM) kamati yangu inaona ipo haja ya kutafuta eneo jengine kwa ajili ya kituo hicho ili kuweka haiba ya mji wetu na kukiondosha pale kilipo kwani sio sehemu sahihi kwa kituo kile kutokana na kuwepo kwa msongamano mkubwa na kusababisha usumbufu kwa wananchi hasa wanafunzi wa skuli ya Kisiwandui.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaomba maelezo ya kina kuhusu kituo kile kwani kamati na Baraza kwa ujumla imekuwa ikilipigia kelele sana suala hillo hivyo tunaomba waziri atakapokuja atupe ufafanuzi juu ya hatma ya kituo kile kwani imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Sambamba na hilo kamati inashauri Wizara kusimamia vyema suala la usimamizi wa usafiri wa Barabara kwa kuhakikisha kuwa inatoa leseni za udereva kwa wale ambao wanastahiki ili kupunguza wimbi la ajali katika nchi yetu.

Programu ya Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya ndege

Program hii inatekelezwa na Mamlaka ya viwanja vya ndege na Shirika la bandari na ina lengo la kuimarisha miundombinu ya Viwanja vya ndege na Bandari ambayo ina program ndogo mbili nazo ni program ndogo ya miundombinu ya Viwanja vya ndege na programu ndogo ya Miundombinu ya Bandari na usimamizi wa usafiri wa Baharini, kiujumla program hii imekasimiwa kutumia TZS Mia moja Hamsini na mbili Bilioni, mia tatu hamsini na saba milioni na ishirini elfu (152,357,020,000). Huduma zitakazotolewa katika program hii ni pamoja na uimarishaji wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume kwa kujenga jengo jipya la abiria, maegesho ya ndege na maegesho ya magari na huduma ya pili ni uimarishaji wa kiwanja cha ndege cha Pemba kwa uwekwaji wa taa za kuongozea ndege pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa huduma mbali mbali za kiwanja hicho. Aidha katika program ndogo ya pili ya miundombinu na ya Bandari na usimamizi wa usafiri wa baharini huduma zitakazotolewa ni kuimarisha huduma za bandari ikiwemo ujenzi wa bandari ya mpigaduri na usimamizi wa usafiri wa Baharini.

Mhe. Spika, Kamati yangu kwa namna ya pekee inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya ndege kwa juhudi zao kubwa wanazochukua za kuboresha uwanja wa kimataifa wa Amani Abeid Karume, sote ni mashahidi hapa wa maendeleo hayo ya kiwanja hicho na tunaomba Serikali waipe Mamlaka hii uwezo zaidi wa kifedha ili kuweza kulikamilisha jengo jipya la Abiria la Terminal II ili uwanja wetu uwe na hadhi kubwa zaidi kimataifa utakaoruhusu ndege mbali za kimataifa kutua nchini kwetu,

Mhe. Spika, **s**ambamba na pongezi hizo za dhati ninazozitoa kwa Mamlaka ya uwanja wa ndege kwa juhudi zao kubwa za kuboresha huduma katika kiwanja chetu naomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ya hotuba yake anipe maelezo ya kina kuhusu kampuni ya *Transworld* inayotarajiwa kutoa huduma ya *ground handling* kuanzia kuitishwa kwa tender, kufunga kwa Mkataba pamoja na mambo mengine yanayohusiana na Kampuni hii, kwani kwa mara kadhaa kamati imekuwa ikihoji kuhusiana na suala hili, lakini kwa masikitiko makubwa bado haijapata majibu ya kuridhisha hadi tunaandaa hotuba hii.

Mhe. Spika, aidha katika hili Kamati yangu inashauri kwamba Katika utekelezaji wa program hii kuendelezwa uwanja wa ndege wa Pemba ili nao uwe katika hali nzuri utakaowezesha ndege kutua wakati wote, uendelezaji huo ujumuishe uwekaji wa taa, utengezaji na njia za kutua na kurukia ndege nk, kwani hali ilivyosasa ni kwamba ndege haziwezi kuruka au kutua wakati wa usiku kutokana na kukosekana kwa taa za kuongozea ndege.

Kuhusu Bandari ya Mpigaduri

Kwa muda mrefu kamati yangu imekuwa ikishuhudia kuzorota kwa taratibu zitakazowezesha kuanza kwa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri licha ya mipango yake ya kiutekelezaji kuwemo katika bajeti iliyopita hivyo kamati inashauri kuwa katika utekelezaji wa program hii ujenzi wa bandari hii ufanyike ili kuimarisha miundombinu ya Bandari na usafiri wa baharini na ili wananchi waweze kunufaika na malengo yaliokusudiwa.

Mhe. Spika, Kamati inatoa shukurani na pongezi za pekee kwa Serikali kwa uamuzi wa kununua meli mpya ya abiria ambayo gharama zake ni karibu 30. 8 Bilioni, ni imani ya Kamati yangu kuwa kuwasili kwa meli hii na kuanza kazi lile tatizo la usafiri wa baharini litaondoka katika nchi yetu, aidha Kamati inashauri kuwepo na utaratibu wa ukaguzi wa meli wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa zinaubora unaohitajika kwa lengo la kuepusha ajali zinazoweza kuepukika.

Programu ya Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Programu ya huduma za teknologia ya Habari na Mawasiliano ni program ya 3 ambayo imepangwa katika Wizara ya Miundombinu na Mawasilliano ambayo ina lengo la kuhakikisha huduma bora zenye kuendelea za teknolojia ya habari na Mawasiliano zinapatikana kwa muda wote hapa nchini. Programu hii ina program ndogo mbili ambazo ni program ndogo ya usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano, ambayo itatoa huduma ya usimamizi wa miundombinu ya mawasiliano ikiwemo kufanya ukaguzi wa Mkonga , usimamizi na ukaguzi wa minara na kusambaza na kuufanyia matengenezo mkonga wa mawasiliano na program ndogo ya usimamizi wa huduma za Mawasiliano, Huduma zitakazotolewa ni pamoja na uwekaji wa anuani za makaazi (*postcode*), kuanzisha vituo vitakavyotoa huduma za *TEHAMA* pamoja na mafunzo ya *TEHAMA* kwa jamii ambapo jumla ya fedha zilizotengwa kwa porgramu hii ni TZS Mia mbili sitini na mbili Milioni, Laki tatu themanini na mbili elfu (262,382,000).

Mhe. Spika, Katika program hii kamati inapendekeza kuwa katika utekelezaji wa program hii mradi wa *E - Governmen*t upewe kipaumbele kwani kwani Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inahusika katika kutandaza mkonga katika taasissi mbali mbali za Serikali, ili mradi huu wa *E-Government* uliotumia gharama kubwa ambazo ni fedha za walipa kodi wa nchi hii uonekane matunda yake yaliokusudiwa. Kwani kamati yangu ya Baraza lako tukufu kwa ujumla wake imekuwa ikihoji juu ya mradi huu bila ya kupata majibu yenye kuridhisha. Hivyo naomba Waziri atakapokuja anipe maelezo yenye siha juu ya mradi huu wa *E – Government* ili wananchi wapate kujua hatua iliyofikia ya utekelezaji wa mradi huu wa muda mrefu.

Programu ya Mipango na Utawala katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano
Mhe. Spika, Program ya Mipango na Utawala katika sekta ya Usafiri na Mawasiliano ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inatayarisha mipango bora ya usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Program hii ina programu ndogo tatu ambazo ni programu ndogo ya utawala na uendeshaji, na programu ndogo ya mipango na sera katika sekta ya usafiri na mawasiliano na program ndogo ya kuratibu wa shughuli za Wizara Pemba, kwa ujumla Programu hii imetengewa TZS bilioni mbili, Mia nane sitini na nane Milioni, Laki sita na thelathini elfu (2,868,630,000).

Mhe. Spika, programu hii imejikita zaidi katika kusimamia masuala ya utawala na mipango na rasilimali watu, ambapo shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kupanga, kuratibu na kusimamia shughuli za Wizara na mradi wa kuimarisha muundo wa taasisi wa sekta ya usafirishaji na mawasiliano, Kamati yangu haina tatizo na kasma iliyopangwa kwa ajili ya programu hii kwani shughuli zilizopangwa kwa ajili ya programu hiii zimejikita katika kuzingatia maslahi ya watumishi ya Wizara pamoja na kusimamia masuala ya mafunzo ya watumishi hao ili kuhakikisha kuwa programu zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Kamati yangu pia ilipata nafasi ya kupitia idadi ya watenda kazi kwa programu na imegundua kuwa katika programu ya Miundombinu na Huduma za usafiri wa Barabara ambayo imekadiriwa kuwa na jumla ya watenda kazi 485 lakini katika hao mhandisi ni mmoja tu na kama ambavyo tunafahamu kuwa ujenzi wa barabara unahitaji utaalamu sana hivyo kuwepo kwa mhandisi huyo mmoja kamati yangu inahisi ni changamoto hivyo tunashauri kuwa Wizara iongeze idadi ya wahandisi ili programu hii itekelezeke ipasavyo na shabaha zilizokusudiwa ziweze kufikiwa. Aidha katika idadi ya watendakazi kwa programu nyengine Kamati yangu imeridhika nayo na inashauri watenda kazi wapatiwe stahiki zao kama ambavyo utaratibu unavyoelekeza ili kuwapa ari ya kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, kwa kumalizia, kamati yangu imejaribu kuelezea kwa kifupi kuhusu mambo mbali mbali yaliomo katika Wizara hii na tumejaribu kutoa ushauri na mapendekezo mbali mbali ambayo kamati yangu inaamini kuwa yakizingatiwa ipasavyo yatapelekea ufanisi katika utekelezaji wa Programu zilizomo katika bajeti ya mwaka 2015/16.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie Bajeti hii kwa lengo la kuiboresha, kushauri, kuelekeza na hatimae waipitishe Bajeti hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nawashukuru kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja, asante. (*Makofi*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, kwanza nishukuru sana jioni ya leo hii kuweza na mimi kutia baraka katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri, leo amesoma zivuri sana na nilimsikia vizuri sana. Siku zote nakuwa namsikiliza babu lakini leo amenikosha, nimemfahamu. Ameelewesha vizuri, ametwambia *point* vizuri na ametuomba tumsaidie kama kawaida yetu.

Mhe. Spika, mimi nianze na UUB. Kwanza niwapongeze sana wataalamu wetu pamoja na msimamizi wake Mkurugenzi. Pongezi zenyewe kwa kuwa tunaweza kutengeneza barabara zenye *standard,* kwa hiyo hiyo ni moja katika sifa nzuri. Nitowe ushauri wangu kwamba tungejaribu kukasimu madaraka. Nafikiria zamani tulikuwa katika Wilaya, tulikuwa tunazo sehemu nyengine kule mashamba watu walikuwa mara nyingi sana kulikuwa kuna kijumba kimoja tulikuwa tunatia viraka. Sasa sijui sasa hivi kutokana na hali ya bajeti imekuwa finyu au kutokana na hali ya sasa hivi mpya ambayo itatuwezesha ya PBB kuweza kufanikisha vizuri.

Mhe. Spika, hapa kuna wataalamu huwezi kuamini. Watu wengine wanaona kuwa na mabanda ndio kusoma, lakini kumbe ukiweza ufundi ndio kusoma. Mimi nimsifu huyu jamaa kasoma sana. Kijana huyu mwenye jina la Amin *wallahi* huwezi kuamini na ndio jina lake hilo. Ukiona zile barabara, mimi siku moja nilijiuliza katika akili yangu hivi kweli hawa ndio wataalamu wa Zanzibar au hii barabara imetolewa nchi za Ulaya tukaletewa Zanzibar, tukawa kama zile nyumba za kuta.

Kwa sababu barabara ni nzuri sana, unatiririka, ukifanya mchezo kama gari yako haina *brake* kidogo unaserereka kutokana na ule umahiri na ulaini zile barabara zinavyojengwa vizuri sana. Niwapongeze sana.

Lakini pongezi hizi zinakwenda kwa msimamizi mwenyewe Mkurugenzi jemedari Mkuu wa ile Idara yenyewe. Kwa sababu sifa ya kiongozi lazima awe na sifa na utendaji wake. Huwezi ukasifu mtu bila ya kuwa hana utendaji. Mkurugenzi ni mtendaji mzuri sana pamoja na wataalamu wake, maana pale pana *team work* nzuri.

Watu kama hawa inafaa Mhe. Waziri tuwaenzi, hawa wenye taaluma kama hizo kwenye sehemu hizo, tuwaenzi wenyewe tuwa-*promote*, tuwagaiye angalau vifungu vya juu, haki yao tusiwanyime . Naomba sana tuwapatie watu kama hawa, ili waendelee zaidi tusione tabu yoyote. Na ndio mambo tu lakini kama nchi za wenzetu mtu kama huyu angeweza kupewa tunzo.

Mhe. Spika, mimi huyu sifurahi kuendesha lile tukutuku. Siku hizi kuna vijana hata zile gari zipo zinaitwa tako moja, sio vespa tu. Vijana wanaendesha vibaya sana gari. Kwa hiyo na yeye huyu lile honda mimi sipendelei, ndio mambo tu, mpeni angalau mkopo wa gari japo kile ki- *Escudo* kile kidogo ili iendane na ule uhalisia aliokuwa nao. Nimeomba sana hilo tuweze kumsaidia kijana wetu, ili kufika mahali pazuri.

Mhe. Spika, Idara ya Leseni. Idara hii juzi tu mngesikia Mshimba al-marhum. Hili suala siku zote mimi nakuwa nalisema. Jamani tunaposema mimi napenda sana mtusikilize vizuri. Ilipita gari, ilibeba kontena la *forty feet* Maruhubi, lilikuwa linakwenda *speed* kubwa sana, watu wote walishangaa. Mimi ile hepu hepu nilikwenda nikajitia kwenye kile kiguzo cha upande wa ukuta wa Maruhubi. Si mchezo, jamaa anapita *speed* zote. Nimeshasema sana hili suala, Mhe. Waziri leo nazuia kifungu kwa sababu nimeshakwambieni watatumaliza, wanatuuwa. Dar-es-Salaam *container* lile lilibanja watu wanane, liliwaangukia likawakandamiza watu wamekufa kwa michezo kama hii.

Mheshimiwa niliwahi kutoa wazo. Jamani wazo langu ni zuri, watakuja kunichukua Wazungu nyinyi mtakuja kulia. Eeh! maana yake nyinyi Waswahili wenzangu hamtaki kunifuata mawazo yangu ninayokupeni. Mimi nakupeni mawazo mazuri kabisa. Ingekuwa nchi za nje mimi nalindwa, nahifadhiwa kwa akili niliyokuwa nayo. Lakini sasa tatizo lililokuwepo mpaka mimi nachoka, kila ninapotoa mawazo mazuri hamtaki.

Nilisema wenye magari ya aina yale ili waweze ku-*run* katika barabara, barabara zetu ni ndogo, *Wallahi* kapita *speed* kubwa sio masihara. Watu wanajiuliza ile gari rangi gani? Wameshindwa kulitambua gari lenye *container* rangi, haki ya Mungu nakwambia Mheshimiwa. Enzi zangu mimi yule angeniona, lakini sasa hivi nina jina la Muheshimiwa.

Mhe. Spika, naendelea kutoa ushauri wa bure wala sitaki. Nasema tuwawekee *time* ambazo wale wenzetu magari yale waweze ku-*run* vizuri, ni muda mchache tu, kwani ukisema kitu gani. Ni kumwambia tu mwana nyinyi sasa hivi mkitaka magari yetu kuendesha, endesheni *time* fulani ambazo lile zogo la watu halipo. Shauri yake muache aende mbio anavyotaka mwenyewe yeye na Munguu wake. Lakini leo kuna watu wengi atasababisha ajali kubwa.

Siku moja *container* lilianguka pale Mikunguni, nani asiyejua, Mwenyezi Mungu akaleta kheri yake watu wakanusurika. Lakini pale watu wengi wangekwenda na maji, si mchezo. Mwenyezi Mungu kaleta Rehma pale amenusuru viumbe, amenusuru viongozi wa kesho, lakini vyenginevyo ingekuwa hatari, tungekosa spika, tungekosa mawaziri, tungekosa maraisi. Kwa kweli hili jambo naomba sana

Mhe. Waziri kaeni jamani mfikirie jinsi gani ya kuweza kuwapeleka hao watu katika hali halisi.

Mhe. Spika, nende katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. "Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni" Juzi nilikaa na Mzee Ali alinionyesha kumbukumbu ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kwa picha. Maana Mzee Ali sasa hivi haoneshi tena magazeti ananiletea kwa picha hapa. Nikiangalia Zanzibar ya leo Uwanja wa Ndege, *Alhamdulillah* sasa tunajiringia. Mtu akitaka asitake sasa hivi Zanzibar tunaringia tunasema kwamba tuna *International Air Port*. Zamani ilikuwa unaogopa hata kusema ule uwanja wangu wa Ndege wa Zanzibar, unaona haya, unajificha ficha. Lakini leo na mimi nikifika nje ninaonesha huu Uwanja wa *International,* Zanzibar. Ukianza kuingia tu unaona ile haiba ya kuwa huu ni uwanja wa *International*. Ukiingia tu angalia *face* yake si mchezo, ujemedara wa Mkurugenzi mwenyewe ni mtendaji mzuri. Tena unajua kuna vitu mtu ukimpa na fani yake kwa sababu mkurugenzi alikuwa *pilot*. Sasa anajua nini maana ya uzuri wa uwanja wa ndege. Leo unakwenda kunipa mimi Mshimba ukaniweke pale, siwezi hata siku moja kuweka vitu kama vile. Kila siku ule uwanja unabadilika.

Tizama leo VIP pale tunakwenda vizuri, lakini ile kodi tu ndiyo inayotupiga chenga. Pale VIP sasa hivi nikuzuri ukitahamaki umelala au umeachwa na ndege, raha mustarehe *Wallahi La'adhim*. Tatizo la VIP ni dogo tu, kuwa ile kodi tuliyoambiwa Sh. 20,000/= tunakimbia, lakini kama anatupunguzia ila basi mimi namshukuru sana kuwa kaitengeneza VIP unajisikia kama VIP.

Run away kwa kweli huwezi kuamini, hebu angalia hapa huwezi kuamini ukioneshwa kwenye picha, utasema kama *United State*. *run away* hii si mchezo, huwezi kuamini Zanzibar hiyo kazi yake. Kwa hivyo naomba sana pongezi hizi ziende huko, matatizo binaadamu anakuwa nayo, hakuna aliyekuwa hana matatizo, tumchukulie kiubinaadamu, lakini kiutendaji nambari *one*.

Mimi naomba sana ajitahidi na ile *terminal* iliyobakia imalizike. Ikimalizika ile Zanzibar itainuka kiuchumi. Kwa sababu kitu chochote kinachokuja na uchumi mzuri kutokana na majengo, kutokana na *ile run away* yenyewe hiyo inakuwa nzuri, basi mambo yanakuwa mazuri sana, tusimamie kwa vizuri, tusimamie kwa jitihada kubwa, ili tufike pahali pazuri sana.

Mhe. Spika, tunakwenda Bandari. Shirika la Bandari alhamdulillah.

Mhe. Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, haya lakini hii bajeti. Niende katika Bandari, sasa hivi *Alhamdulillah*, hata ule urundikanaji wa masuala ya

container naona inaanza kupungua uhalisia wake. Niseme kuwa anajitahidi sana Mkurugenzi kwa jitihada zake zote ambazo, kwa sababu yeye ni mtaalamu kusema ukweli. Yeye alikuwepo kwa miaka mingi sana na imefika sasa hivi kwa kazi za ufanisi zinakwenda vizuri sana. Nimpe hongera sana na nimshukuru sana. Wakala wa meli tunashukuru sana kwa hilo, tunakwenda vizuri, tunasubiri meli mpya na si vibaya tukatafuta mawakala, ili kuweza kusaidia na Shirika la Meli.

La mwisho nikwambie, nirudi katika changamoto ya mambo ya usimamizi wa leseni. Hapa tungepata muwekezaji mzuri, tungepata wakala mzuri katika masuala ya upasishaji wa gari, hapa mapato yanakuwa yanapotea. Basi kama yupo ambaye ameshaleta *application* yake ya kuomba basi tunaomba sana, hili suala likamilike kwa haraka haraka.

Mhe. Spika, namalizia ZMA, naomba sana kwa hapa, kuna utaratibu wa kupasisha vile vyombo vyetu. Ningeomba sana muda wa kupasishwa uwende na *time* na ripoti. Mtu anapokuwa anataka kufanyiwa *sea try*, basi kwa vyovyote tunaomba isichukue muda mwingi. Tatizo lipo hapa tu. Mkurugenzi yeye anaamua, lakini wale mainjinia tena wasichukue muda mwingi. Nimeona hilo nilisemee, kwa kweli kwa Wizara hii imenifilisi sana. Wamefanya mengi sana mazuri, haki zao tuwape.

Nimsifu sana Katibu wangu na yeye ni msimamizi mzuri, tunauona usimamizi wake hauna kasoro pamoja na Naibu Katibu wake kwa *experience* yake, kwa kweli hawa watu nawapongeza sana.Waheshimiwa wenzangu nikuombeni sana tumsaidie Mhe. Waziri, tumkosoe lakini kidogo kidogo na hata zile tusizifunge kutokana na hali yake Mheshimiwa, ndio kwanza kapewa juzi wizara hii, nawaombeni sana.

Mhe. Spika, wamenikubali vijana wamenipiga kofi na mimi naungamkono kwa asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, leo *scorer* kakosa *midfield*, kwa hivyo, ndio naingia mimi. Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii leo nikiwa mtu wa pili baada ya Mhe. Mshimba.

Mhe. Spika, na mimi nampongeza Waziri pamoja na timu yake kwa kuleta hotuba hii nzuri ya bajeti. Mimi mchango wangu wa mwanzo nitaanza kuchangia ukurasa wa 6, kifungu cha 3(2) Mradi wa Sekta ya Usafiri wa Baharini. Mhe. Spika, Zanzibar tumezungukwa na bahari pande nne; tuna vyombo vya meli, tuna majahazi, tuna ngalawa na vyombo vyengine vidogo vidogo ambavyo vinasafiri baharini.

Mhe. Spika, katika siku chache zilizopita tulipata misiba ya uzamaji wa meli pande mbili zote Kaskazini na Kusini na maafa haya yametufika sisi Wazanzibari pamoja na Tanzania kwa ujumla. Ningeliiomba Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu kuhakikisha kwamba bandarini pana vyombo vya uokozi vya uhakika. Tuna bandari zetu mbili tunazotumia ambazo bandari hizi wakati wa upepo mkali basi vyombo vyetu vinataharuki hasa bandari yetu ya mkondo wa Nungwi na bandari yetu ya mkondo wa Kusini kwendea Dar es Salaam. Kwa hivyo, ninaihimiza wizara, ninaihimiza vile vile Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu kununua vyombo vya uokozi vyenye uhakika.

Mimi ninakumbuka ilipozama ile meli moja hapa ilikwenda kuokoa meli, sasa meli ile iliyokwenda okoa na hiyo iliyokuwa imezama mwendo wake sawa sawa. Kwa hivyo, ikiwa mwendo ule kwa mfano meli inayokwenda kuokoa Serengeti, Serengeti kutoka bandarini mpaka ikafika pale Chumbe masaa 5, kwa hivyo, itakuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, nikenda katika uokozi, nchi yetu ya Zanzibar tuna vijana ambao wanaweza sana hii *diving*, lakini sasa bado serikali yetu haijawatunza vijana hawa ili kuwanunulia nyenzo za kuweza kuokoa. Serikali hapa iligharimu kuwaleta watu kutoka Afrika Kusini wakati wapo vijana wanaweza kazi ile kuliko Afrika Kusini, wako vijana Zanzibar wanakwenda pima 14 bila ya kutumia *gas*, Muafrika Kusini mpaka atumie *gas*, mimi kule Nungwi nilikwenda vijana walioweza kuokoa watu waliokuwa wamezama ni vijana wa Zanzibar, lakini aliletwa mtu kutoka Afrika Kusini kufika mkondo wa Nungwi kasamehe.

Gharama za *diver* yule kutoka Afrika Kusini akaletwa hapa kwa gharama ya fedha, maji yake ya kunywa akanunuliwe Dar es Salaam, pa kulala achague, lakini yule Mzanzibari aliyeokoa pale lakini hakuthaminika. Wamekuja Afirika ya Kusini hapa wakachukua fedha wakenda zao hawakumuokoa mtu hata mmoja. Wale vijana Wazanzibari Nungwi pale wakaokoa watu wengi tu. Kwa hivyo, ninaiomba Serikali vijana wa Zanzibar wanaweza kuwaokoa watu pindipo wakipatiwa zana. Kwa hivyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba kununua zana za uokozi na kuwapa *training* vijana wakawapa kazi ile tunaweza sana sisi kuokoa. Kule Matemwe tunao vijana ambao wanaweza wakaokoa sana watu waliozama bila kuletwa watu kutoka Afirika ya Kusini au kutoka Uingereza, uwezo huo tunao tupatiwe zana tu basi kwa sababu kila kitu ni zana.

Mhe. Spika, ninaendelea katika Usafiri wa Nchi Kavu, ukurasa wa 7, kifungu cha 3.3. Usafiri wa nchi kavu kwa hivi sasa na magari tuliyokuwa nayo ni hatarishi sana, madereva sasa hivi wanakwenda mwendo wa kasi, magari yamekuwa mengi, njia zetu zimekuwa nyembamba sana, sasa magari ya Zanzibar yamekuwa na yanakwenda kwa kasi, wengine huwa wamelewa na wanakwenda mwendo wa

kasi. Kwa hivyo, Serikali lazima ihakikishe kwamba kuwachukulia hatua madereva wanaokwenda kwa kasi wanahatarisha, kuna magari ya daladala yanapakia watu mpaka wananing'inia. Kwa hivyo, lazima Serikali ichukue hatua juu ya madereva hawa ambao wanachukua watu bila ya sheria.

Mhe. Spika, ninakwenda katika mradi wa barabara za vijijini. Tuna barabara za vijijini ambazo barabara hizi ni muhimu sana kwa wananchi kama kule kwetu Matemwe mimi ninazo barabara ambazo zinaleta maendeleo kwa wananchi lakini zimechafuka, kwa hivyo, naiomba Serikali, naiomba Wizara ya Miundombinu waje waziangalie barabara hizo ambazo ni tatizo kwa wananchi na nitazitaja hapa haidhuru hapo katika kitabu hazipo lakini ninamuomba Mhe. Waziri. nimtajie barabara hizo na UUB wapo hapa watazijua.

Barabara moja kutoka Mfurumatonga kwenda Kachongwa na moja kutoka Mfurumatonga kwenda Mikuuni, hizi bandara ni kubwa haidhuru ni barabara zinaitwa *feeder road* lakini kubwa na zinapita watu wengi. Ninaomba wizara kupitia shirika lake la UUB waje waziangalie barabara hizi wanipe msaada wa kuzikarabati kwa njia hiyo ya fusi.

Mhe. Spika, kwa vile nimechangia mchango wangu, hapa naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano mia kwa mia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu mfupi kuchangia hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2015/2016 ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika Baraza lako Tukufu. Mhe. Spika, kwanza nitoe pongezi kwa namna Mhe. Waziri, alivyokisoma kitabu chake kwa utaratibu kabisa na kukifahamu na kumaliza kazi yake ndani ya wakati na pia Mwenyekiti wa Kamati kwa namna alivyotoa hotuba yake.

Mhe. Spika, mimi naomba kutoa maelezo yangu kama ifuatavyo. Kwanza nianze na mradi wa maegesho na njia ya kupitia ndege katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ambao ni kwenye kifungu ukurasa wa 4. Katika ukurasa wa 4 imeelezwa kuwa mradi huu uliokuwa na lengo la kujenga maegesho na njia ya kupitia ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume, umekamilika mwezi Disemba, 2014 na kufunguliwa rasmi mwezi wa Januari. Mimi ninashukuru kwa kupata taarifa hii na ni taarifa ambayo ni ya kuridhisha.

Lakini Mhe. Spika, katika ujenzi wa uwanja huu nakumbuka umeanza zamani sana na umechukua muda mrefu sana, iliwahi kuja kampuni hapa ikaondolewa na fedha nyingi imekwishatumika halafu kama kumbukumbu zangu ziko sawa ikaja kampuni nyengine kwa uwanja huo huo, kwa hivyo, mimi ninaridhika na maelezo

yaliyopo, lakini kwa ruhusa yako ningeliomba kujua ujengaji huu ulitumia fedha kiasi gani za wahisani na ulitumia fedha kiasi gani za Mfuko wa Serikali tokea kuanza kwake mpaka kumalizika kwake. Kama kuna mkopo vile vile tujue ulikuwa kiasi gani na kama fedha hiyo imeshalipwa kwa sababu uwanja tayari umeshakamilika na unatumika ipasavyo.

Mhe. Spika, halafu nikitoka hapo naomba nizungumze kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume. Ujenzi wa jengo tunaujua, jengo hili lilikuwa na ramani yake mwanzo halafu ukasita, jengo hili lilikopewa fedha ikamalizika na ikakopwa fedha nyengine, jengo hili lilikuwa na ramani yake na nasikia ikatengenezwa vyengine. Kwa hivyo, mimi naomba kujua, mpaka hii hatua iliyofika jengo hili ni kiasi gani ya fedha ambazo mwanzo ilikuwa zitumike lakini zimetumika kutokana na hayo yaliyojitokeza hapo katikati. Kwa sababu kutokana na maelezo ni kuwa jengo hili limegharimu fedha nyingi na halijamalizika na hatua iliyofikia ni asilimia 32 tu ya hatua inayotarajiwa mpaka kumaliza kwake ningeliomba kujua mpaka hivi sasa ni kiasi gani cha fedha kimetumika kwa asilimia hiyo 32.

Mhe. Spika, jengine ni kuwa jengo hili kwa mujibu wa maelezo tumeelezwa kuwa lilikadiriwa au lilipangiwa kutumia jumla ya Tanzania shilingi bilioni 1.950, lakini fedha iliyochangwa kwa ajili ya shughuli hiyo hiyo ilikuwa ni bilioni 2.797, yaani ni sawa sawa na asilimia 143 na kuwa fedha hii ilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya msimamizi wa ujenzi na malipo ya fidia. Mimi ningeliomba kujua kwa nini fedha iliyokadiriwa kutumika ilikuwa ni bilioni 1.950 lakini ikachangwa bilioni 2.797 ilikiwa ni sawa sawa na asilimia 143 na huyu msimamizi wa ujenzi malipo ya fidia aliyolipwa ni fidia gani hiyo kwa sababu hapa haikuelezwa, naomba nipate maelezo.

Mhe. Spika, jengine ninaloomba kupata maelezo ni kuhusu ujenzi wa bandari ya Mpigaduri ambayo inapatikana ukurasa wa 19, kifungu cha 19, ukurasa wa 6. Katika ujenzi huu maelezo tuliyopewa ni kuwa ujenzi huu wa Bandari ya Mpigaduri hatua iliyofikiwa ni ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri ni kukamilika upembuzi yakinifu pamoja na uchambuzi wa athari za kimazingira, ninashukuru kwa hilo. Lakini mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni mia tano, lakini hadi kufikia Machi, 2015 hakuna fedha iliyoingia. Sasa naomba kujua kwanza ni lazima tujuwe umuhimu wa kuwa na Bandari ya Mpigaduri, Bandari yetu ya Malindi ni ndogo haikidhi haja, teknolojia inaongezeka kwa wenzetu wanaongeza maeneo ya kuongeza bandari nyengine, kujitahidi kupata bandari mpya ya Mpigaduri itakuwa ni yenye manufaa sana kwetu.

Lakini bandari hii ilikuwa ikizungumzwa siku zote mara washakuja hawa, mara washakuja hawa, kumbe ndio kwanza mpaka hii leo bandari hii iliyofanyika ni

kama iliyoeleza ni upembuzi yakinifu pamoja na uchambuzi wa mambo ya kimazingira, halafu huku ndio shughuli zinafanywa za kutafuta fedha na zikipatikana ndio shughuli hiyo itaendelea. Mimi nataka nipate kuelewa hasa hii Bandari ya Mpigaduri itaendelea vipi kwa sababu hakuna maelezo ya kutosha kuona hapa kuwa iko hatua itaendelea baada ya hapa ilipofika. Na naomba nipate maelezo ya kina kutokana na umuhimu wake ili na sisi Zanzibar iweze kujikomboa kiuchumi kwa kutumia bandari zake.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha 23 ambacho kifungu hiki kiko kwenye ukurasa wa 7 na naomba kukisoma kwa ruhusa yako na kifungu kinachohusiana na ujenzi wa barabara ya Wete/Chake, kinasema;

> "Mhe. Spika, mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha baada ya kukamilika awamu ya mwanzo ya mradi ikiwa ni taratibu ya upatikanaji wa mkopo kutoka *Saudi Fund* zitakamilika. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya Tanzania shilingi milioni 100,000,000 zimetengwa na hadi kufikia Machi hakuna fedha iliyoingia."

Mhe. Spika, hii inasikitisha sana barabara ya Wete/Chake Chake ni barabara mbovu sana, ni barabara ya asili inatumika hata kabla ya Mapinduzi, imeachwa mpaka leo haijafanyiwa matengenezo ipasavyo imo katika hali mbaya sana. Na tulivyosikia ni kwamba hii barabara tayari ilikwishatiliwa mikataba, kwa hivyo, ni kitu gani hasa mpaka ikavunja moyo kutokana na hii sentensi inayosema kwamba "kukamilika awamu ya mwanzo ya mradi ikiwa taratibu za upatikanaji mkopo kutoka *Saudi Fund* zitakamilika".

Ina maana ikiwa haukupatikana mkopo ndio barabara hii haijengwi wakati iko katika hali mbaya sana na wakati kumbe ilikwishatiliwa mikataba. Kwa hivyo, naomba maelezo ya kina ina maana ikiwa mkopo huo haukupatikana ndio basi tunakwenda na maji na tubakie katika barabara kwenye hali mbaya vile ilivyo.

Mhe. Spika, jengine ninaloomba kuzungumza ni kwamba hii ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na wizara hii kutokana na Zanzibar ilivyo ni visiwa na tunatumia bandari zetu. Kwanza jambo ambalo linanisikitisha sana ni kuwa sote tunajua kama bandari zetu zitaimarika na usafiri wetu utaimarika, kwa hivyo, huduma itakuwa ni nzuri na fedha nyingi zitaingiza. Lakini kwa bahati mbaya Wete kuna bandari, Mkoani kuna bandari, Wesha kuna bandari, Mkokotoni kuna bandari hizi ni bandari za asili na asili na hakuna moja kati ya bandari hizi iliyokuwa haitumiki na kuingiza fedha katika serikali, lakini hazishughulikiwi. Inasikitisha mpaka leo kuwa Wete hakuna meli inayokwenda wakati zamani zilikuwa meli zinakwenda, hii ni kuingiza shida katika uchumi wa nchi na kuwaweka wale watu waliokuwepo Wete kule kuwa ni wamasikini wakubwa na

Wapemba kuhangaika kutoka sehemu yoyote mpaka kuelekea katika bandari moja tu iliyoko Mkoani.

Mhe. Spika, mimi kwa ruhusa yako naomba nijue, ni nini hasa hatma ya bandari hizi nilizozitaja, kwa nini zibakie mpaka leo katika hali ile zisiimarishwe kiasi ambacho ikatumika na wananchi kuweza kusafiri kwa urahisi na serikali kupata fedha zake ilivyo. Na kwa nini mpaka leo Zanzibar ikiwa ina watu wengi sana itumie bandari moja tu ya Malindi wakati tuna bandari ya Mkokotoni mpaka leo imeshindikana kuimarishwa kiasi ambacho mara nyingi inatumika kwa usafiri ambao si mzuri na nisingependa kuutaja hapa. Kwa hivyo, nataka kujua hasa serikali ina mpango gani wa kuona kuwa na kule Mkokotoni bandari yake imeimarishwa imekuwa ya kisasa na inatumika ipasavyo kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine Shirika la Bandari moja katika kazi yake ni kuhakikisha usalama wa usafiri wa abiria wao. Siku za nyuma hapa tulikuwa tukizungumza sana kuhusu upakizi wa kupita kiasi ikawa haitiliwi maanani na kuhusu ubovu wa vyombo vyetu mpaka likatokea lilotokea na Mwenyezi Mungu atunusuru lisitokee tena. Leo hapa tulipo Mheshimiwa, naanza tena kusema kuwa kuna ulazima kwa kujali maslahi ya Wazanzibari wetu wanaosafiri kuona kuwa meli yetu ya serikali iliyobakia hiyo ya abiria ya *MV*. Maendeleo ama inazuia kupelekwa chelezoni au ifanyiwe marekebisho kwa sababu hivi sasa tayari imo katika hatua ya kuhatarisha amani.

Mhe. Spika, juzi iliondoka Pemba ikafika Unguja saa mbili za usiku na jana mpaka saa tano mchana kuanzia asubuhi inakorokochwa huku, inakorokochwa huku haishiki moto halafu watu wakapelekwa kama si binaadamu. Kwa hiyo, naiomba serikali kwa makusudi ione kwamba hakuna ulazima wa kuwapeleka watu katika meli mbovu itengenezwe, isije ikawa yakaja yakatokea mambo ambayo hatutakuwa na lugha nyengine ya kuzungumza. Safari ile tulisema *Inalilahi waina ilayhi rajiuna,* sijui safari hii tutawaambia vipi wananchi.

Mhe. Spika, jengine ninalopenda kuzungumza ni kwamba tuna bandari yetu na bandari ile ina chelezo na chelezo kinatumika kwa kutengeneza meli zetu, na tulisikia zamani kuwa chelezo ile itarefushwa mpaka kina kikubwa cha maji ili badala ya kuchukua meli zetu kupeleka sehemu nyengine kama Mombasa na kadhalika chelezo ile iweze kutumika kwa matengenezo ya meli zetu zenyewe na meli nyengine zitakazoingia ikiwa ni kuingiza fedha katika nchi. Lakini tokea hatua iliyofikia mpaka leo hatuoni hatua inayoendelea ya kuimarisha ile chelezo na ilijengwa kwa nia safi sana. Kwa hiyo, naomba Mhe. Spika, nipate maelezo hatma ya chelezo hii.

Mhe. Spika, la mwisho katika kuchangia kwangu ni kwamba tumesikia kuna meli mpya inakuja na inafanyiwa majaribio kama yalivyoelekezwa, halafu mambo yakikamilia meli hii itakuja na itatumika kwa mujibu wa maslahi ya wananchi wetu na kadhalika na ni meli ya mizigo na abiria. Mimi Mheshimiwa, naomba kusema kuwa Mwenyezi Mungu atujaalie hii meli ije na najua meli hii ikija itapelekwa katika Mamlaka ya Meli na Shirika hili la Meli na Uwakala tunavyojua ni kwamba mara zote wanakuwa na meli walikuwa *MV*. Maendeleo mpya, walikuwa *MV*. Mapinduzi mpya, walikuwa *MV*. Ukombozi mpya, wakazitumia na zilikuwepo kongwe, linalosikitisha wakati meli zile zilikuwa zinafanya kazi zinaingiza, hatuoni sababu kwa nini meli zote zikafa ikawa pasiwezwe kuzalishwa meli nyengine.

Kwa hivyo, naomba lazima tufanye utaratibu pesa nyingi imetumika lakini isije ikawa kama meli zilizotangulia zikafa bila ya meli hii kuzalisha kwa maslahi yetu sote. Mhe. Spika, nashukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naambiwa sasa tumo 41 humu ndani na utaratibu wetu huwa tunachangia changia tukishapata wajumbe tupitishe jambo letu, Katibu hebu ni-*introduce* Wizara ya Habari.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na kama ingekuwa haitokuwa kinyume na heshima ule mlango ningefunga ili waliomo humu ndani wasitoke, lakini nataka wengine kumbe waje, kwa hiyo, itabidi tusiufunge ili wengine waje. Hivyo, walioko nje wote Waheshimiwa Wajumbe, waingie ndani sasa ili tuweze kuendelea kusikiliza majumuisho kwa Wizara ya Habari na baadae kupitisha mafungu yanayohusika. Nimuombe basi Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, aanze kufanya majumuisho, tujitahidi tubaki humu ndani, na nadhani tunafanya kwa ufupi kidogo ili tuweze kupitisha mambo haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu…

Mhe. Spika: Tumsikilize Mhe. Naibu Waziri, anaanza kutoa majibu ili tuweze kumaliza shughuli hii, Mhe. Naibu Waziri, endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia jioni hii nikaweza kusimama hapa na nikaweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo na Uwezeshaji na Habari. Pili, niweze kumpongeza Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuweza kunipa mashirikiano ya pamoja kwenye wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Pia, nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari pamoja na Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na Wakurugenzi, vile vile, nisimsahau Afisa Mdhamini Pemba na wafanyakazi wa Wizara ya Habari pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano wanayonipa kwa ufanisi kwenye Wizara yetu ya Habari.

Mhe. Spika, nikiendelea nianze mchango aliochangia Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile, amezungumzia kuhusu wawekezaji pamoja na mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Mwakilishi kuhusu wawekezaji na mwezi mtukufu wa Ramadhani Kamisheni ya Utalii imeandaa taarifa rasmi ya kuweza kuwapelekea wawekezaji kuhusu mavazi na kutokula ovyo kwenye maeneo ambayo yamo katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Pili, niende kwa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, yeye amezungumza kuhusu soka la wanawake, kuhusu soka la wanawake ni kwamba tunaye kocha ambaye ni mzaliwa wa hapa Zanzibar ni kocha mwanamke ndiye anayefundisha timu zetu za Tanzania. Pia, nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kuna timu ambazo zinatoka Kusini Pemba na Mikoa yote ya Unguja mitatu zipo timu za wanawake nazo pia zinaendelea kwa ufanisi zaidi na kuendeleza juhudi zetu za michezo hapa Zanzibar.

Vile vile, niende kwa Mhe. Panya, yeye alizungumzia kuhusu mila na desturi na mambo mengine ambayo yanahusiana na utamaduni wetu wa Kizanzibari. Mhe. Panya, utamaduni wetu wa Kizanzibari una nyanja nyingi ambazo zinaendelea, pia kuna mila na desturi ya utamaduni wetu wa Kizanzibari, kuna utamaduni wa mavazi na malezi ya Kizanzibari.

Mhe. Ashura na yeye alizungumzia kuhusu utamaduni wetu wa Kizanzibari hasa kwenye wasanii. Wasanii wetu ni wasanii wana mila na desturi ya Kizanzibari, lakini kama tunavyojua wasanii wana nyanja nyingi na kama tunavyojua sasa hivi

ni wakati sayansi na teknolojia. Kama tunavyojua wasanii ni vijana wa leo sio wale wasanii wa zamani, lakini pia kwa sababu ya kusema hivyo tunao wasanii ambao ni wa kizazi ambacho kimepita nao pia wanaendeleza usanii wao.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Ashura pamoja na Mhe. Panya pamoja na Mhe. Mwanajuma Mkoa wa Kaskazini Pemba, Wilaya ya Micheweni kulikuwa na mama mmoja alikuwa anapiga msondo kwa mkono mmoja. Sasa tusione kama wasanii hawa wanapoigiza wanashika kwenye maungo yao, ni kila mtu na vile alivyokuwa anashabikia ule usanii wake. Kwa hiyo, mama huyu alikuwa na washabiki wengi sana kwa ule msondo wake aliokuwa anapiga kwa mkono mmoja, wajue kwamba wasanii wana-*style* zao na wasanii wa sasa wana-*style* zao za sayansi na teknolojia.

Mhe. Spika, pia, nikiendelea mbele nimpongeze Mhe. Mgeni na yeye nampongeza sana kwa jinsi alivyochangia na kwa kweli kwa ufasaha zaidi na akaeleza mambo mbali mbali yanayohusiana na mila na desturi na unyanyasaji wa kijinsia pale wanapopeleka vipindi vyao kwenye *ZBC*. Mhe. Mgeni, usione kama *ZBC* inawanyanyasa au inawadharau kupeleka vipindi vyenu, kwa kweli vipindi vile vinatoka na Mhe. Mgeni, nakuhakikishia wizara kwa kushirikiana na wanawake ambao wanatoa vipindi vyao vinavyohusu unyanyasaji, hilo litashughulikiwa kwenye wizara yetu pamoja na *ZBC* na wala usione shida na sisi tukiwa ni wanawake tutazidi kupeleka vipindi vyetu ili tuone jinsi vipindi vyetu vinatolewa.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele kuna Waheshimiwa mbali mbali ambao wamezungumzia kuhusu wizara yetu, nawaomba sana ndugu wajumbe kwa sababu ya kuzungumza hayo nimesema nitoe ufafanuzi mdogo tu ili Mhe. Waziri na yeye aje atoe ufafanuzi vizuri ili muweze kuipitisha bajeti yetu, na kama mnavyojua hii ni bajeti ya mwisho. Naomba sana ndugu wajumbe bajeti muipitishe kwa hekima na busara na muone kwamba leo hii ni siku ambayo ni ya utamaduni wa Kizanzibari, maana wizara hii inahusiana na mambo mengi muone leo ni siku ya utamaduni wa Kizanzibari muuendeleze, musiipigie buti muweze kuipitisha kwa salama na amani. Ndugu wajumbe nawashukuru sana na mimi hapa nimesimama naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia, mimi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia salama, wazima *Alhamdulillah* jioni ya leo kuendelea kufanya shughuli zetu. Pia, nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka uajo wa fedha 2015/2016.

Aidha, naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa maelekezo na ushauri mbali mbali ambao wamekuwa wakinipa katika kusimamia wizara hii, kwa kweli maelekezo yao yamekuwa dira muhimu sana na imekuwa ikinisaidia sana. Naomba pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliojaaliwa kuchangia bajeti hii ya mwaka huu kwa hakika michango yao ilikuwa ni ya kujenga, kunielekeza, kuniongoza na kunishauri kwa maslahi ya wananchi, nawashukuru sana.

Mhe. Spika, miongozo na ushauri wa kibajeti katika bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nimeipata kutokana na Waheshimiwa Wajumbe 16 wafuatao naomba niwatambue.

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Saleh Nassor Juma
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Mohammed Haji Khalid
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Mgeni Hassan Juma
9. Mhe. Hija Hassan Hija
10. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
11. Mhe. Ashura Sharif Ali
12. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
13. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
15. Mhe. Mohammedraza Hassanali
16. Mhe. Abdi Mosi Kombo
17. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, kwa kweli wajumbe wote nawashukuru na nawapongeza sana kama nilivyosema wametoa michango ya kunisaidia na kuisaidia wizara yangu, wametusaidia katika kuelekeza, kutuongoza na kutuhakikisha kwamba mambo yetu yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, naomba nianze na mambo ya jumla, kwanza Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Utalii na Habari. Kwa kweli tunamshukuru hasa kwa namna ambavyo ametupa ushauri wa mambo mbali mbali. Ushauri wake tutaufanyia kazi na kama kawaida yake huwa anatupa ushauri mara nyingi, ushauri wa kujenga anatuelekeza sana na pongezi ambazo ametupa tunazichukua. Watendaji wamezisikia, ni zao hasa mana wao ndio wanaotenda itakuwa kama ni hamira ya kuzidisha ari ya usimamizi na utendaji kazi tunamshukuru sana.

Wa pili ambaye tunataka kuzungumza mambo ya jumla ni Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Makamu Mwenyekiti wa kamati hii, naye alikuwa anazungumzia suala moja tu la wale wakuu wa idara Pemba wana posho gani. Kimsingi katika mfumo mzima wa serikali hadi hivi sasa hakuna posho maalum kwa wakuu wa idara Pemba, lakini jambo hili kama ninavyofahamu ni kwamba taasisi zinazohusika na mambo ya utumishi serikalini wanalizingatia na baadae bila shaka watatoa toleo moja kwa ajili ya wakuu wote wa idara na taasisi mbali mbali Pemba ambazo wanastahiki chochote kama ambavyo alipendekeza.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze la jumla ni la Mhe. Hija Hassan, suala la tofauti ya mishahara na *OC* katika taasisi zetu. Hili ni jambo la kawaida sana, kwa kawaida taasisi nyingi mishahara huwa mikubwa kuliko *OC*, kwa sababu kuna baadhi ya taasisi ni za utoaji wa huduma. Mfano, katika wizara yangu Bodi ya Sensa shughuli zao nyingi ni za ukaguzi zaidi kuliko ambazo za kununua kitu hiki na kile. Kwa hiyo, katika hali kama hiyo wafanyakazi wale watakuwa na fungu kubwa la mshahara na fungu la matumizi mengineyo ni dogo la kutafuta labda mafuta na mambo mengine madogo madogo.

Kuna taasisi nyengine utaziona kama Chuo cha Habari, Chuo cha Utalii, Gazeti, haya yana ruzuku lakini pia wameruhusiwa kukusanya na kutumia. Kwa hiyo, utaona *OC* yao kutoka serikalini ni ndogo, lakini pia wameruhusiwa hawa wakusanye na watumie na *trend* utaona kila mwaka ruzuku inapungua kwa sababu lengo ni kwamba haya ni mashirika yanalelewa baada ya muda yawe yameshajiweza iwe wanaweza kujichumia wenyewe kutokana na uwezo wao. Kwa hivyo, ni kweli kuna baadhi ya taasisi utaziona kwamba *OC* zao ni ndogo lakini nyengine zina ruzuku lakini pia zina uwezo wa kuchuma na kutumia wenyewe.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo naomba nilizungumze ni la Tume ya Utangazaji, kalizungumza sana Mhe. Mgeni Hassan Juma. Nampongeza sana kwa michango yake, kama kawaida yake huwa ana michango mizuri sana ya kujenga na kutuelekeza, na katika hili alituelekeza na kutushauri kwamba, tutoe motisha mbali mbali kwa redio zile ambazo zinashajihisha masuala ambayo yanapiga vita udhalilishaji katika jamii yetu.

Mhe. Spika, ushauri wake tumeuchukua na tokea hapo tumeanza kuufanyia kazi. Redio hizi tumekuwa tukizisaidia mafunzo mbali mbali ya utendaji wake, tumekuwa tukiwasaidia vifaa, fedha ya kuandaa vipindi na pia kusaidia matengenezo ya vifaa vyao. Kwa hivyo, tutaendelea pia kuchukua ushauri wao kuangalia na kushirikiana pamoja na *UNESCO* kuangalia namna gani tutaweza kuwasaidia katika masuala yao.

Mhe. Spika, katika Baraza la Kiswahili kulikuwa na mchango mmoja kutoka kwa Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa, ambaye alitaka kujua nini hatma ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Jibu lake ni kwamba, vikao mbali mbali vya uandaaji kwa hatima ya Kamisheni ya Afrika Mashariki hapa Zanzibar vimeshafanyika, usaili wa wafanyakazi watakaoendesha ofisi hiyo tayari umeshafanyika, jengo kwa ajili ya ofisi hiyo hapa Zanzibar tayari lishapatikana, kinachokamilishwa ni kukaa kikao cha mwisho kwa mawaziri wanaohusika katika masuala ya Kiswahili katika Afrika Mashariki ili kuja kukamilisha, tunategemea kwamba katika mwaka ujao wa fedha *Inshaallah* kituo hiki kitafunguliwa.

Mhe. Spika, katika Hoteli ya Bwawani kulikuwa na michango minne, mitano naomba niijubu kwa pamoja kama ifuatavyo: Ni kweli Hoteli ya Bwawani tulizungumza serikali kwamba inataka mwekezaji. Tumepata mwekezaji mzalendo serikali inaendelea kuzungumza naye, tumefikanaye pahala pazuri, lakini sharti la serikali ni kwamba hoteli ile yenyewe ya Bwawani ina historia kubwa katika nchi yetu na kwa hivyo, bado itaendelea kubakia.

Kwa hivyo, haya ndio mambo ambayo bado serikali inalikamilisha hili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe ndiye anayelisimamia hili na kadiri tunavyofahamu ni kwamba baada ya muda mfupi suala hili litakuwa limemaliza kwa masharti kwamba, hoteli ile ambayo ina historia kubwa katika nchi yetu bado itaendelea kuwepo na mwekezaji atayekuja atapata nafasi nyengine ya kufanya uwekezaji wake katika maeneo mengine kwa ramani ambayo itakubaliwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja ya wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani ambao hawakupata nafasi ya kuajiriwa. Ni kweli kulikuwa kuna wafanyakazi hao hawakutimiza vigezo vya kuajiriwa walighushi vyeti vyao. Sisi kwa sababu hiyo hatukuweza kuwachukua hawakuridhika wakakata rufaa Ofisi ya Rais Kamisheni ya Utumishi wa Umma na uamuzi ni huo huo kwamba hawawezi kuajiriwa.

Mhe. Ashura Sharif Ali, alizungumza suala dogo kuhusu kwa nini makusanyo ya Hoteli ya Bwawani yamekuwa kidogo mwaka huu? Ni kweli yalikuwa kidogo kuliko ambavyo tulikusudia, lakini ushindani umekuwa mkubwa na tunajipanga vizuri mwaka huu tukijaaliwa kuona kwamba malengo yetu tunaweza kuyafikia.

Mhe. Spika, katika eneo la Makumbusho tulikuwa na michango na maelekezo mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe, nawapongeza sana kwa kuona umuhimu wa makumbusho katika nchi yetu na historia ya nchi yetu. Kwa hivyo, kwa ujumla ni kwamba Gofu la Mkamandume wizara inalifahamu vizuri tunalishughulikia, tumekuwa tukilitembelea mara kwa mara, kuna wafanyakazi tumewaweka pale kuhakikisha kwamba haliharibiwi, halichukuliwi mawe, kwa

sababu wananchi wetu wana matatizo kidogo, wamekuwa wakienda pale wakichukua mawe katika eneo lile. Kwa hivyo, tumeweka wafanyakazi maalum kwa ajili hiyo na tumelitia katika maabara ya utalii kuangalia namna gani tutaweza kulifufua. Lakini pia tumeandika *project write-up* kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani kuangalia namna gani tutaweza kulihuwisha zaidi.

Ushauri wa maeneo mengine Liko la Ngezi, Vitongoji tutahakikisha kwamba tunapata nafasi ya kulitembelea na kulitia katika maeneo ambayo yangehifadhiwa. Kuhusu historia ya Field Marshal Okello ushauri tumeuchukua kwamba pamoja na viongozi wengine tutaangalia namna gani kuweza kuenzi historia zao sahihi.

Mhe. Spika, kulikuwa na ushauri wa Mtule na kisima chake tutaufanyia kazi, lakini naomba niseme kwamba si kweli kuwa serikali haishughulikii kuenzi kumbukumbu zetu na sio sahihi kudhani kwamba watu binafsi wao ndio ambao wanafanya kuenzi kumbukumbu kuliko serikali, nyote mnaelewa serikali ina idara nzima ya *archive* kuona kuwa kumbukumbu zetu mbali mbali kuanzia miaka ya nyuma hadi leo zinahifadhiwa vizuri sana.

Mhe. Spika, katika Idara ya Habari Maelezo kulikuwa na hoja moja kutoka kwa Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa na ushauri juu ya namna ya uwekaji wa kumbukumbu vizuri. Ushauri wake tumeuchukua na tutaweka vifaa vizuri zaidi vya kisasa kuona kwamba kumbukumbu za picha na vitabu vinavyohifadhiwa pale vinakuwa vizuri zaidi na kumbukumbu za hotuba mbali mbali za viongozi wetu hivi vinatakiwa vihifadhiwe katika *archive* ya *ZBC*. Jambo hilo limeanza vizuri na *Inshaallah* tutaendeleza vizuri kama ushauri wa Mhe. Mjumbe, aliyotupa.

Mhe. Spika, kuhusu Baraza la Sanaa na Bodi ya Sensa tumepata ushauri mzuri kutoka kwa Waheshimiwa, ushauri kwa Mhe. Saleh Nassor Juma, kuhusu wasanii tumeuchukua, majibu ameyatoa sana Mhe. Naibu Waziri, kwamba kila msanii ana matao yake ya kuimba, wengine wanajikamata kichogo, wengine bega, wengine magoti, yote hayo ni katika matao ya kuhakikisha kwamba usanii wake umevutia.

Kuhusu ngoma za asili Mhe. Mohammed Haji Khalid, ametushauri kwamba tuendelee kuzitunza. Naomba hili tushirikiane na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi. Katika maeneo yetu kuna ngoma mbali mbali ambazo ni muhimu sana kwa historia ya nchi yetu, tuwarithishe watoto wetu pamoja na vikundi vingi vya dini ambavyo tunavyo katika maeneo yetu ambavyo kwa kiasi kikubwa ndivyo vinavyoturejesha nyuma katika hili. Lakini ninawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukubaliane kwamba suala la kuenzi ngoma zetu za asili ni jamboambalo ni urithi wa Taifa letu.

Mhe. Panya Ali Abdalla, tunamshukuru kwa mchango wake na tutahakikisha tunashirikiana naye katika kuona yale ambayo ametushauri tunayafanyia kazi. Kuhusu Sheria ya Mavazi bado tunashauriana na ofisi ya kurekebisha sheria iliyo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Ni jambo ambalo linahitaji mashauriano na washirika mbali mbali katika nchi yetu, watu wengi sana hili jambo wana maslahi nalo, kwa hivyo, bado tunaendelea kushauriana nalo.

Mhe. Nassor Salum Ali, katika eneo hili ametushauri kufanya kazi ya ziada kuhakikisha kwamba tunawawezesha wasanii wetu, ushauri wake tunauchukua na tunaufanyia kazi.

Mhe. Spika, katika Kamisheni ya Utamaduni kulikuwa na michango mingi na ushauri tuliopewa na Waheshimiwa Wajumbe kwa kuuenzi utamaduni wetu tumeuchukua na hili kama nilivyosema ni letu sote. Watoto tunao sisi tuna wajibu wa kuwafundisha utamaduni wetu, tusiwaachie tu wakaiga tamaduni za nje, watoto tunao majumbani mwetu, walezi ni sisi, wazazi ni sisi, tuone namna gani tutashirikiana pamoja kuona kwamba tunawarithisha utamaduni wetu. Nimefurahi Mhe. Bi. Panya, ametupa utamaduni wa namna karafuu zinavyotumika kukanda kanda ni jambo zuri. Hili suala linahitaji kurithishwa kwa vijana wetu waelewe rasilimali hii muhimu na Waheshimiwa Wawakilishi, hasa wanawake wasaidieni sana wananchi wetu katika kuona kwamba suala hili linafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, tunakushukuru sana hasa pale ulipotilia maanani kwamba wazee na wazazi tutilie maanani suala la kuwafundisha watoto wetu wanawake namna ya kurithi utamaduni wetu hasa kabla ya kuolewa ili wanapoolewa wahakikishe kwamba wanawafanyia mema waume zao. Mheshimiwa, hili ni jambo zuri na naona kwamba tushirikiane sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, alikuwa na mchango mzuri katika eneo hili na kwa kweli yale aliyozungumza tunayachukua tutayafanyia kazi. Kuhusu pongezi zake kwa ukumbi wa kurikodia muziki tunauchukua, kuhusu suala la kuweka ukumbi maalum wa kuweza kuonesha sanaa zilizorikodiwa, tunalifanyia kazi, tutaangalia namna gani ukumbi ulioko Rahaleo tunaweza kuufanyia kazi hiyo na kama huo hautoshi basi tutaangalia upande mwengine kwa ajili ya kuwasaidia vijana wetu ili waweze kujiajiri vizuri zaidi.

Kuhusu Ngome Kongwe ushauri wake tumeuchukua, tayari tumetoa tangazo la kuomba wanaotaka waje, wamewahi kuja lakini bado hawajakamilisha masharti. Nimeelekeza kwamba yatolewe matangazo mengine ili kuona kwamba tunapata mtu ambaye anaweza kukodi Ngome Kongwe kuweza kuonesha mambo mbali mbali ya usanii bila ya kuathiri wananchi wanaoishi maeneo yale. Kwa hivyo, haya ndio mambo ambayo masharti yetu, nadhani kwamba Mjumbe yeyote wa Baraza la

Wawakilishi akiwa na *interest* na hilo tafadhali aje apeleke barua na tutaangalia namna gani tunaweza kufanya hii kazi.

Mhe. Spika, kulikuwa na ushauri zaidi kutoka kwa Mhe. Ashura Sharif Ali, hasa kuhusu mavazi ya kanzu na kofia. Ni kweli siku hizi wengi tumeacha kuzivaa, hata humu Barazani utaona wanaovaa kanzu ni kidogo kina Mhe. Hamza Hassan, lakini kwa kweli wengi tumeacha utamaduni huu na ni jambo ambalo linatutambulisha sana Wazanzibari. Kwa hivyo, si jambo la kulionea haya hata kidogo ni jambo ambalo ni muhimu sana. Wenzetu kama alivyosema mchangiaji mmoja Mmasai unamuona Ulaya na rubega yake, lakini Wazanzibari bado kofia yetu hii ambayo ina heshima kubwa, inatutambulisha vizuri tunaionea haya kuivaa katika maeneo mbali mbali. Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo tumepewa na Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tuendelee kuhimizana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa, alitushauri tuunde kamati maalum ya kufufua maeneo ya kihistoria. Ushauri wake tunauchukua, tutaufanyia kazi na tutamshirikisha yeye kwa sababu katika maeneo yake kuna maeneo mengi ambayo tunaweza kushauriana.

Mhe. Abdi Mosi (Kepteni), alitoa mchango mmoja muhimu na naomba nimtambue hasa katika kutumia lugha yetu ya Kiswahili na hili ni jambo muhimu sana. Mhe. Spika, kuna wakati utakwenda katika semina utawakuta Wazanzibari 200, lakini kuna Wazungu wawili, mada zitakazotolewa zote ni za Kiingereza. Sasa hapa hatukipi nafasi Kiswahili chetu kukua, Wazungu wawili, watatu katika semina mada zitakazotolewa ni kwa Kiingereza, sasa hii haiwezekani, lazima hawa wageni wajifunze Kiswahili wenzetu hawafanyi hivyo.*(Makofi)*

Ukienda China hata Mchina kama anajua Kiingereza atazungumza kwa Kichina na anakijua kweli kweli Kiingereza, ukienda Ujerumani Wajerumani wanajua Kiingereza, lakini watazungumza Kijerumani. Sasa sisi hili nadhani ni letu sote, taasisi mbali mbali za serikali na sisi katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tutalipa kipaumbele kuona kwamba tunatumia lugha yetu katika mikusanyo mbali mbali tukiwemo sisi na wageni. Mheshimiwa Kepteni, kwa kweli nakushukuru sana kwa mchango wako.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii imechangiwa sana, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu huu ndio uchumi wa nchi yetu. Tumepewa maelekezo mengi, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ametushauri suala la ushauri wa vyama vipya vya utalii, tumeanza kulitekeleza kupitia maabara ya utalii, hilo tutaliendeleza. Fedha ndogo za kutangaza utalii ni kweli, lakini keki tunayoikuisanya ndio hiyo, kwa hivyo, ikishagawiwa gawiwa kidogo kile ambacho tunapata sisi tunakitumia.

Vile vile, kulikuwa na mchango ambao Wajumbe wengi wamelizungumzia suala la wananchi wetu wanaopeleka bidhaa katika mahoteli mbali mbali ambao hawalipwi. Ni kweli, kumbukumbu yangu ni kwamba kuna karibu shilingi bilioni moja ambayo wananchi wetu mbali mbali wanazidai hoteli.

Suala hili mimi nalijua wamekuja wizarani kwangu tumeweka vikao vingi baina ya Wizara, Kamisheni ya Utalii na wenye mahoteli husika. Serikali imeunda kamati ya taasisi husika, lakini hatimae mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amelibeba. Anasema haiwezekani wananchi wetu wapeleke bidhaa mahoteli halafu wasilipwe, lakini tatizo ni lipi.

Tatizo watu wetu wanakwenda kienyeji, wakishasikia hoteli ipo wanakwenda kutafuta mtu mnunuzi wa mahoteli wanamwambia bwana nitakuletea bidhaa anamwambia lete, hakuna mikataba hakuna lolote, akiona halipwi baada ya muda anaenda kufanya zogo mwengine ambaye hajapeleka anasema aah, mwache anakwenda yeye na yeye anapigwa. Kwa hivyo, mtu mwenye hoteli moja anadaiwa na wananchi wetu watano, sita, bila ya wao wenyewe kujuana na bila ya mikataba yoyote.

Sasa hili jambo tumeliona na tumewambia hawa jamaa waunde taasisi yao ya ku-*supply* vifaa vya mahoteli wameshaunda. Lakini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ametupa kazi kuona kwamba tunafatilia hawa na ama mambo mawili wafanya maekelezo ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais; ama walipe wananchi wetu au waondoke. Kwa hivyo, kazi hiyo tunaifanya na baada ya muda tutafika pahala pazuri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, amezungumza suala la *emergence unit*. Mhe. Spika, hili liko katika maabara lakini watekelezaji ni Wizara ya Afya, sisi hatuwezi kuweka *emergence unit* kwa sababu haya kila wizara ina *field* yake. Kwa hivyo, fedha zinatiwa katika maabara ya utalii lakini watekelezaji ni wenyewe Wizara ya Afya, naona wamelianza vizuri na naamini kwamba watalitekeleza vizuri.

Lakini pia Mhe. Makame Mshimba, kalizungumzia suala la Utalii kwa upana sana. Mhe. Spika, nataka niseme kwamba shughuli za utalii katika nchi yetu ni Mtambuka sana. Wizara nyingi zinashughulika na kuendesha utalii. Wizara ya Fedha inashughulika na masuala ya wawekezaji na kukusanya mapato, Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kazi yake ni ulinzi, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma inashughulika na ajira, kafukuzwa na kwa nini, iko Utumishi wa Umma, Wizara ya Mambo ya Ndani masuala la *visa*, yaani Magresheni na sisi Wizara ya Habari kupitia Kamisheni ya Utalii tunashughulika zaidi katika kuutangaza utalii.

Sasa shughuli za utalii ni *cross cutting* sana, sasa ikiwa wafanyakazi wanafukuzwa mahotelini serikali imesikia hasa na waziri mwenyewe yupo ambaye anaeshughulikia na Utumishi wa Umma, Wizara ya Kazi, sio Wizara ya Habari,sisi kazi yetu ni kuutangaza utalii na tunafanikiwa vizuri, *Alhamdulillah* na tunafanikiwa vizuri, watalii laki tatu na kumi na moja wamekuja mwaka jana na tunaendelea kuutangaza.

Sasa Mhe. Waziri, mwenyewe amesikia na amekuwa akiifanyia kazi sana kadhia hii, nampongeza sana, tumekuwa tukishauriana sana mimi na yeye kuangalia namna gani wananchi wetu hawataendelea kunyanyaswa. Na kwamba Wazanzibari hawaajiriwi, ni wageni walioko na hili pia naomba Mheshimiwa, amelisikia. Lakini na hili nimeshawahi kulizungumza, naomba nizungunze tena. Mimi nilijaribu kutembelea hoteli mbili, tatu, nne, kuangali hili, ni kweli.

Mhe. Spika, si kweli, ukienda kule utawakuta wafanyakazi na Wazanzibari ni *Cosmopolitan,* huwezi kumjua Mzanzibari kwa kumtizama uso, ndio tabu yenyewe, kuna Wazanzibari wa aina mbali mbali. Lakini ili umjube Mzanzibari muulize kitambulisho, sasa ukimuuliza mfanyakazi kitambulisho anacho cha Mzanzibari Mkaazi sasa utasema huyo vipi, huyo ni Mzanzibari huwezi kusema aah, haajiriwi ni Mzanzibari. Sasa kama sie amepataje kitambulisho, tutilieni mkazo huko. Kwa hivyo, tusilalamike tu kwamba wale ni wageni ma-*PO* inawezekana na hii ili tuhakikishe kwamba hilo tunalidhibiti tuendelee kuwasomesha watoto wetu kuhakikisha kwamba wanasomeshwa masuala ya *Administration,* lakini pia wanashughulika na mambo ya utalii. Kwa hivyo, sisi tumeanza Chuo cha Utalii kimeanza kutoa *course* ya wale vijana waliomaliza *Human Resource* wamepewa dozi kidogo ya *Tourism* ya miezi mitatu ili kuweka tayari kwa *PO* katika mahoteli.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alizungumzia Kikosi cha Ulinzi na Utalii. Kilikuwepo lakini baada ya kuanzisha hichi kikosi rasmi kinachosimamiwa na JKU shughuli zile sasa zimehamishiwa katika Kikosi cha JKU. Mhe. Mohammed Haji Khalid, suala lake la Ramadhani Mhe. Naibu Waziri, amelijibu vizuri. Mhe. Panya Ali Abdalla, nadhani nimejibu, nadhani watalipwa wote ni *process,* si suala la mwaka mmoja au miwili litachukuwa muda kidogo lakini tunaendelea vizuri, tunatoa taaluma hasa ya uzalishaji mbali mbali ili wananchi wetu waweze kuhakikisha kwamba wana bidhaa za kuweza kufaidika na soko la utalii. Hivi sasa utaona sana zawadi nyingi zinatoka nje ya Zanzibar tunataka kuona kwamba watalii wanapokuja hapa wanapata zawadi kutoka kwa Wazanzibari wenyewe. Sasa hili lazima tushirikiane kuona kwamba tunawaanda watu wetu katika hilo. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, suala la mazalia ya kasa tutahakikisha kwamba *ZIPA* inapota vibali vya uwekezaji wanalizingatia hilo. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, nimeshalijibu suala lako hasa kuhusu *suppliers*. Mhe. Mgeni Hassan

Juma, ushauri wako kama kawaida tumeuchukua na tumejaribu sana kuona kwamba kama ulivyosema kwamba soko la wajasirimali hasa wanawake tutajaribu kwenda nao, juzi nilikuwa Ujerumani na Mheshimiwa Rais tulichukuwa wanawake watano wajasirimali kwenda kuonesha namna ambavyo sanaa zao zinaweza zikauzwa na zinapendwa sana, tulikwenda na watu wachoraji hina walikuwa hawalali kuanzia asubuhi mpaka usiku wanatia hina tu wao, tulikwenda na wasukaji ikawa hawana nafasi mpaka mikono inauma wanasuka tu. Kwa hiyo, maana yake bidhaa hizi zikitangazwa vizuri inaweza ikawa soko zuri hasa kwa watu wetu. Tulikwenda maonesho ya Oman Mnazi Mmoja kulikuwa na wajasirimali hasa wanawake 15 walikuwa na bidhaa mbali mbali waliuza mpaka zikamaliza, wakaagiza nyengine zikamaliza. Kwa hiyo, tunaenda nao kidogo kidogo kuona kwamba tunapata nafasi.

Mhe. Hija Hassan Hija, ni kweli bajeti ya maabara ya Utalii mwaka huu imetoka kidogo, lakini hali ndio hiyo na *Inshaallah* mwakani huenda mambo yetu yakawa mazuri zaidi. Mhe. Abdalla Moh'd Ali, fedha ya utanzaji ya utalii ni kidogo lakini kila mwaka *Alhamdulillah* mwaka juzi sio mwaka jana na naamini kwamba mwaka ujao Mhe. Waziri wa Fedha atatuingiza nyingi zaidi.

Mhe. Ashura Sharif Ali, nakushukuru kwa mchango wako suala la kufukuzana katika mahoteli, wizara inayohusika na ajira italishughulikia. Kuhusu vituo vingapi viko Mwangapwani. Kuna vituo vitatu vya Utalii; kuna kisima cha chini kwa chini, kuna *Slave Chamber*, mnara na *bunkers* zile za kumbukumbu za vita vya pili za dunia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, suala la muwekezaji wa Mnemba nimelisikia nitalifanyia kazi kwa kushirikiana na *ZIPA* pamoja na Wizara ya Uvuvi kwa sababu hili ni suala la Mtambuka haiwezekani kama alivyosema kwamba muwekezaji aje hapa anyanyase wananchi tunapaswa kulifanyia kazi, tuliambia kuwa kuna eneo la hifadhi limewekwa. Kwa hivyo, tunahitaji kukaa pamoja baina ya Kamisheni ya Utalii *ZIPA* pamoja na Idara ya Uvuvi kuona namna gani ambapo wananchi wataweza kufanyakazi zao bila ya kunyanyaswa. Sisi katika hili tunaona kwamba muhimu kuliko yote kuhakikisha kwamba Wazanzibari wanapata nafasi ya kufanya kazi zao bila ya kunyanyaswa. Mheshimiwa. hilo tutalifanyia kazi.

Kuhusu Baraza la Michezo Mhe. Spika, nashukuru kwa michango iliyotolewa Mhe. Saleh Nassor Juma, ametupa mchango mzuri sana. Lakini nataka niseme kwamba katika sekta ya michezo sisi serikali ina jukumu lake, vilabu vina jukumu lake, viongozi wa vilabu wana jukumu lao na wachezaji wana jukumu lao. Sisi serikali tuna mambo manne, makubwa matatu na moja dogo:

(1) Sera, sera ya michezo ipo nzuri sana.

(2) Sheria, sheria ya Baraza la Michezo ipo ambayo inawapa nafasi Mazanzibari yeyote anaetaka kucheza aje acheze, aje asajili mchezo wake hatuna tatizo. Kwa hivyo, jukumu letu kuhakikisha kwamba sheria yetu haitoi vipingamizi kwa Wazanzibari ambao wanataka kucheza michezo iliyoruhusiwa.

(3) Kusaidia miundombinu ya michezo, ndio ukaona tumejitahidi viwanja hivi tunaviimarisha na tutaendelea kuviimarisha kwa kadiri ya hali ya fedha itakapopatikana.

Sasa na dogo hili ni jukumu la wanaokuja kusajili viongozi, *training*, makocha na ufundi tunasaidia. Lakini kwa msingi hili ni la wenye vilabu, sasa ukisema kwamba wizara inashiriki katika kuuwa michezo mambo yetu matatu ya msingi sisi tumeyafanya vizuri, tuna sera iliyo nzuri, tuna sheria iliyopitishwa Baraza la Wawakilishi na tunasaidia kuhakikisha kwamba miundombinu ya michezo siku baada ya siku inaimarika. Sasa hilo ndilo jukumu la msingi la serikali.

Sasa mambo mengine viongozi wa vilabu waliokuja kusajili wasimamie, huwezi kuja kunambia mimi nitaka ofisi, sasa wewe vipi shekhe umekuja kusajili mchezo lakini huna hata ofisi, si mtihani, nataka kufanya mashindano nipe pesa, haiwezekani hivyo, sasa wewe ulipokuja kuomba usajili ulikuwa una maana gani. Yapo mambo serikali inaweza kusaidia unakwenda mashindano ya kitaifa umekwama tunasaidia. Sasa hili naomba sana tushirikiane na kwa kweli tumekuwa tukisaidia sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma, alizungumzia suala la makocha akamtaja Tambwelea. Twambelea alikuwa anatoka Zaire nakumbuka. Sisi tumekuwa na makocha kutoka Uingereza John Hot tumeajiri kocha kutoka Misri na zaidi tumekuwa na kocha *cross continent* wamefundisha timu ndogo hizi za *Juvenile team* nyingi sana kwa muda wa miaka mitatu mradi huo umemaliza juzi. Sasa mkisema serikali, Baraza la Michezo walisaidie katika kufundisha kwa kweli sio sahihi. Kwa hivyo, tujitahidi katika hili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, tunakushukuru kwa mchango wako na tunakushukuru sana kwa namna ambavyo anasimamia chama cha riadhaa, yeye ni Makamo Rais wa Zanzibar wa Chama cha Riadha. Anafanyakazi nzuri na ndio maana yake ukakiona kwamba chama cha riadha kinapiga hatua. Sasa hii ni mfano kwamba chama kikiwa na viongozi wazuri na kikiwa hakina migogoro kwa kweli kitakwenda. Lakini chama kama kimekaa pale kinasubiri bakuli wazi serikali itie pesa halafu kifanye vurugu hicho chama kitakuwa sababu ya kuua michezo katika nchi hii. Suala la ofisi Mhe. Makame Mshimba, litatafutiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwanajuma Faki, tunakushukuru ulizungumza mambo mengi, ulizungumza suala la timu za mpira wa wanawake.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, zingatia muda.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Waziri, amelizungumza, lakini na mimi naomba nitoe wito kidogo Mhe. Spika. Katika Baraza hili kuna wanawake wengi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Mimi ningeshauri waanzishe timu moja wa wanawake au mbili, iwe ni funzo kwa wanawake walioko majimboni na wilayani kuhusiana na mchezo huo wa wanawake na mimi wakishaanzisha basi angalau nitatoa seti za jezi angalau kuona kwamba wameridhika.

Mheshimiwa, kuhusu suala la timu za Ufukweni zipo na zinafanyakazi vizuri makocha wazalendo wapo wanafanyakazi vizuri Hemed Moroco ana daraja la *class A* na bibi Nasra Juma pia. Kwa hivyo, tuna makocha wazuri Zanzibar tuwape nafasi wafanyie kazi.

Mhe. Spika, kuhusu *ZFA* kuna tatizo kubwa, kuna mgogoro Mahakamani niliulizwa na hili jambo moja baya sana. Aliyepeleka kesi Mahakamani ni Makamu Rais wa *ZFA* Unguja amesababisha muda wote *ZFA* iwe haiko *stable*, athari yake ni kubwa na bahati mbaya kuna watu wanamuunga mkono wanamshabikia. Sasa Mhe. Spika, hili ni tatizo hatuwezi kuwa na watu wanashabikia mambo ya migogoro na nawaasa sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasiyashabikie mambo haya yatatufikisha pahala pabaya sana, athari yake hili ni kubwa.

Wadhamini wa *grand malta* wamechoka na migogoro, mimi nimeenda kwao Bara wiki mbili zilizopita wamesema kwa vile *ZFA* ina kesi Mahakamani hatuwezi kuendelea kudhamini. Sasa mnashabikia mambo Waheshimiwa na athari yake ni hii. Sasa kile kikosi kinachojiita UKAWA tafadhalini sana waache kushabikia mambo. Kuna kikosi nasikia cha michezo wanajiita UKAWA. Mimi nilidhania UKAWA iko Dodoma kule wale jamaa, lakini kumbe mpaka katika michezo wapo. Sasa mtihahi, hili litaweka nchi pabaya.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira), nakushukuru kwa mchango wako katika michezo, naomba sana una uzoefu mkubwa nadhani ungeisaidia sana *ZFA* iliyopo kutekeleza majukumu yake. Soka halijafa Zanzibar linafanyakazi vizuri, ushahidi wake ni kwamba wachezaji zaidi ya thalathini wanaocheza ligi kuu ya Bara wanatoka Zanzibar hivi sasa. Hii ni mfano mzuri kuona Zanzibar wanakuja kuchukuwa hapa wanakwenda kule, miaka 60 kulikuwa na mmoja Mzee Hija Saleh, lakini hivi sasa kuna zaidi ya 40 vilabu mbali mbali wa Bara wanachukuwa wachezaji wetu.

Maana yake hali ya mchezo inakuwa hapa Zanzibar vyenginevyo wasingekuja. Kwa hivyo, hii ni rahisi tuendelee, michezo mingine ambayo haina migogoro *netball*, judo, riadha inakwenda vizuri na hii inasimamiwa na Baraza la Michezo na wizara. Lakini *football* acheni sana kushabikia migogoro.

Mhe. Spika, nimalize na ushauri wa Chuo cha Habari nauchukuwa umetolewa na Mhe. Mlinde na Mhe. Mahmod Mohammed Mussa, Wizara ya Fedha ipo na amesikiwa Waziri wa Fedha. Chuo cha Utalii bajeti yake ni kweli ndogo lakini wanakusanya pia Mhe. Spika.

Mhe. Ashura Sharif Ali, alitaka kujua wanafunzi waliomaliza na wangapi wameajiriwa kuanzia mwaka 2011/14. Wamemaliza wanafunzi 1,492. Tumefanya utafiti mdogo wa kuangalia hoteli 31 tu katika hoteli 430 tulizonazo. Katika hoteli 31 kuna vijana wetu waliomaliza 285. Kwa hivyo, tukimaliza utafiti huu itaonekana kwamba tutakuwa na vijana wengi tutakaowagundua ambao wameajiriwa. Kumekuwa na tatizo la kufanya *field* lakini sasa limeondoka.

Kuhusu *ZMUX* kwamba iunganishwe na *ZBC* Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, hii ni mambo tofauti; *ZBC* ni *content provider, ZMUX* ni *channel provider*. Kwa hivyo, haya mambo mbali mbali. Kazi ya *ZBC* ni kutayarisha vipindi, kazi ya *ZMUX* ni kurusha vipindi. Hivyo, haya mambo mawili hawezi kuchanganywa.

Shirika la Magazeti Mhe. Spika, limechangiwa na Wawakilishi wengi. Ushauri wao tunauchukua na *concern* yao kubwa ni kuona kwamba Zanzibar inachapisha gazeti lake hapa hapa Zanzibar, Serikali ina-*concern* hiyo kwa muda mrefu imekuwa ikijaribu kuomba huku na kule. Kuna mwanga wa matumaini umeonekana kwamba Serikali ya Oman hivi wiki mbili zilizopita zilisaidia fedha nyingi ikiwemo suala la kuimarisha *press*. Ninaamini kwamba Serikali itafanya kila jitihada kuona kwamba inaweka mtambo pale wa magazeti ili uweze kutumiwa katika *natx* mbali mbali ikiwemo Shirika la Magazeti, ikiwa Kanuni na sheria zitarekebishwa kidogo.

Mhe. Spika, nimalize na *ZBC*, kulikuwa na ushauri mwingi wa *ZBC*. Mhe. Spika, naomba niseme kwamba *ZBC* hivi sasa kwa vipimo vyangu iko vizuri kuliko wakati mwengine wote. Ninasema hivyo kwa sababu hivi sasa *ZBC* ina vifaa vizuri kuliko wakati mwengine wowote, vifaa vipya kabisa, vifaa vya *studio* vipya ambavyo vimefungwa hata miezi miwili bado. Unguja kuna *studio* mpya na Pemba kuna studio ya *ZBC* ambayo ni ya ki-*digital* na niya kileo kabisa. Pili, ina wafanyakazi wengi ambao wana ujuzi waliosoma kuanzia *diploma, degree* ya kwanza, *master* kuliko wakati mwengine wowote tangu *ZBC* iundwe. Tatu, ina kamera nyingi kuliko wakati mwengine wowote tangu *ZBC* iundwe. Nne,

imetimiza gari tisa ambazo hazijawahi kumilikiwa na *ZBC*. Sasa niseme kwamba *ZBC* ina uwezo mkubwa hivi sasa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ushauri mbali mbali zilitolewa tutauchukua. *ZBC* bado imo katika *reform*, tumeunganisha na Sauti ya Tanzania na Televisheni, ina madeni mengi, tumerithi madeni mengi ya umeme tu karibu milioni mia tano kutoka taasisi hizo mbili, ina wafanyakazi wengi, tunajaribu ku-*reform* na ili kuli-*reform* tutafika pahali itabidi hivi sasa tuna wafanyakazi 325, hao ni wafanyakazi wengi, tunapanga kuwapunguza kidogo. Kwa ilivyo ile hoja ya Mhe. Hija, kuhusu wafanyakazi 12 waliohamishwa ni programu za kuhakikisha kwamba wafanyakazi hao 325 tutawapunguza wasizidi 100, ili kuhakikisha kwamba shirika hili limekwenda kwa ufanisi. Kuwa na wafanyakazi wengi tu 325, wengine hawana kazi na wengine hawana la kufanya kwa kweli hili linaweza kutuletea matatizo.

Mhe. Spika, kulikuwa na posho la wafanyakazi. Hili limechangiwa na Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuzungumza. Hili mimi ninalijua kwamba vijana wetu hawa wanaokuja hapa Barazani wanalidai shirika posho. Posho hili nilifunguliwa Katiba hapa nikaambiwa aah! Mhe. Panya Ali Abdalla, alinukuu Katiba. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hii sio *overtime*. Kwanza tuelewane vizuri, wafanyakazi wa *ZBC* hapa wamekuja kazini. Ni *privilege* tumewapa kwa sababu ya mazingira ya kufanya kazi kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini si *overtime*, tuelewane vizuri. Maana imejengwa hoja hapa kama kwamba sisi Wizara na Shirika tunawadhulumu hizi pesa zao. Tumesema tumekubaliana Wizarani na Shirika kwamba wanapaswa kupata *privilege* na sisi tunakubaliana kwamba hii ni ndogo. Tumekuwa tukiwalipa sana hali inaporuhusu na bado tunakusudia kuwalipa. Hivi sasa *ZBC* inadai ruzuku iliyoopo Serikalini shilingi milioni mia moja na arobaini na nane. Hawa vijana mpaka kikao kilichopita walikuwa wanadai shilingi kumi na tano milioni na hichi mpaka kikimaliza watakuwa wanatudai shilingi ishirini na nne milioni.

Mhe. Spika, nilizungumza na Mhe. Waziri wa Fedha na akanikubalia kwamba kuna umuhimu wa kuwalipa na katika fedha hizi shilingi milioni mia moja arobaini na nane ameshawaagiza watendaji wake, kwamba atutilie shilingi ishirini na nne milioni ili kuondoa kuondoa mzigo huu ambao unafanyakazi. Hili litakuwa limemaliza kwa sababu tukijaaliwa kuanzia mwakani tumekubaliana kwamba sasa Baraza la Wawakilishi litakuwa linailipa *ZBC*, tumekubaliana hivyo. Wenzetu Bungeni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anajua kwamba Bunge ndiyo inayowalipa *TBC* na *TBC* ikapata uwezo wa kuwalipa wale wafanyakazi. Hapa Baraza la Wawakilishi walikuwa hawanilipi Waheshimiwa, munawatetea watu ambao nyinyi hamunilipi, vizuri mungetetea kwanza nilipwe halafu muone nisiwalipe.

Kwa hivyo, nina furahi kuanzia mwaka ujao Mheshimiwa, Ofisi ya Katibu wa Baraza tumekubaliana Mhe. Spika, kwamba litaweza kulipwa na *Inshaallah* suala hili litamaliza, lakini kwa makubaliano na Mhe. Waziri wa Fedha ambaye ninamuamini sana kuwa ameahidi atatulia fedha hizi ili kuweza kulipwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa muda ulionipa, umenivumilia sana, lakini ni lazima nichukue muda mrefu ili niweze kuhakikisha kwamba ninawatosheleza Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, na ninaamini kwamba nimejitahidi kwa kadri inavyowezekana kuona kwamba ninajibu hoja zao.

Ninashukuru tena kwa michango ambao wamenipa, ninawatakia kila heri katika safari ambayo tuliyonayo; mwezi wa Ramadhani unaoanza kesho au keshokutwa kwa wengine. Kama alivyosema Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, tunawatakia kila heri tunawatakia kila la heri mwezi unaokuja *Inshaallah* uwe mwezi wa faraja na mafanikio. (*Makofi*)

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sasa, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majumuisho hayo. Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2015/2016 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kukubaliwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizra yangu.

KAMATI YA MATUMIZI
FUNGU J01-WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 05 Idara ya Habari, Maelezo	Shs.38,000,000/=
Kifungu 07 Tume ya Utangazaji Zanzibar	Shs.65,000,000/=
Kifungu 10 Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	Shs.230,000,000/=
Kifungu 11 Baraza la Kiswahili Zanzibar	Shs. 40,000,000/=
Kifungu 12 Baraza la Sanaa, Sensa, Filamu na	

Utamaduni Zanzibar	Shs.20,812,000/=
Jumla Kuu	**Shs.393,812,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU J01 - WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu P01 Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Nilipokuwa nikichangia katika eneo hili la Idara ya Magazeti nilimuomba Mhe. Waziri kwamba wakati umefika sasa Zanzibar na sisi tutoe gazeti lenye lugha ya Kiingereza, lakini Mhe. Waziri alipokuja kujibu baadhi ya hoja hapa hili sijalisikia. Sasa Serikali au Wizara yake ina mpango gani katika hili. Naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ukweli kwamba Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, alitupa ushauri huo. Kimsingi tunakubaliana naye na kwamba Bodi ya Shirika la Magazeti wameshalizungumza hili na wameshaliwekea utaratibu wa kulitekeleza. Kwa hivyo, ni bahari mbaya kama sikumjibu kwa sababu ya muda na baada ya kuniambia niharakishe. Lakini kimsingi tumeshaanza kulifanyia kazi na Bodi imeshaeleza utaratibu wa kwenda nalo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ni sawa kwamba Bodi imeshalizugumza hili na kwa uzoefu tulionao Bodi mara nyingi huwa inakaa mara nne katika mwaka. Sasa sijui ni muda gani hasa litachukua hadi kuona kwamba na sisi Zanzibar labda katika mwaka wa fedha mwishoni kwenye mwezi wa Oktoba au mwanzoni mwa mwaka unaokuja tuweze kupata mwelekeo wa kuweza kupata hili gazeti la Kiingereza. Ni lini hasa hili gazeti litakuwa tayari. Namuomba Mhe. Waziri, atusaidie katika hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, lini hasa, siku na mwezi itakuwa vigumu sana kumpa jibu. Lakini maelekezo ya Bodi ni kwamba kwa vile utafiti umeshafanywa na Shirika na imeshaonekana umuhimu wa kuwepo na wasomaji wapo. Kwa hivyo, nimeelekeza kwamba katika mwaka huu wa 2015/2016 iangaliwe uwezekano na hasa baada ya kupata fununu kwamba Zanzibar kupitia Kiwanda cha Uchapaji patakuwa na Kiwanda cha Ofisi ya Magazeti.

Kwa hivyo, hili nimeelekeza kwamba hali hiyo ikiwezekana basi mapema katika mwaka huu wa 2015/2016 liweze kutekelezwa. Hayo ndiyo maelekezo ya Bodi na tutayasimamia kuona kwamba yanatekelezwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na majibu yake, naomba tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante lakini kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, alivyokuwa akijibu hoja baada ya hoja kwa umakini. Lakini hoja yangu kwa sauti ya chini kabisa ni ile ile Mhe. Waziri, kaijibu mwisho kwa kweli, lakini bado wanasema Waswahili "Dalili ya mvua mawingi", au "Nyota njema huonekana alfajiri".

Hawa wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira magumu; wafanyakazi wa *ZBC* na kwa milioni kumi na tano kwa vipindi vitano, bado Shirika linaingiza pesa, lakini inaonekana hakuna harufu hata ya kuweza kulipwa pesa. Haiwezekani vipindi vitano basi hata kupunguziwa hizi pesa.

Mimi nimuombe Mhe. Waziri, angalau anayebwebwa naye hujikaza kwa hichi kidogo nacho kinachotumika katika kipindi hichi kabla hujaondoka zipunguzwe hili deni. Hiyo ni hoja ya kwanza.

Hoja ya pili, kuhusu mazingira ya Gazeti la Zanzibar Leo, mazingira ya wafanyakazi wa Gazeti la Zanzibar Leo hayaridhishi kiafya.
Na hoja ya tatu kuhusu kile kifaa cha *link* bado sijapata ufafanuzi tokea asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema suala la malipo haya kuwa wafanyakazi hawa wanajua kwa namna ambavyo nimekuwa nikifuatilia suala hili, wafanyakazi yenyewe wanafahamu hivyo. Nimekuwa nikizungumza nao na uongozi wao mara kwa mara.

Ukweli ni kwamba Shirika la *ZBC* linakusanya lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Shirika hili lina matumizi mengi. Nikikwambia kuna wakati hufika *ZECO* wakataka kukata umeme. Sasa uone kwamba kile kinachokusanywa chote kinatumika vizuri kwa kuendesha Shirika lenyewe ili angalau watu waone.

Mashirika mengine ya habari Mhe. Mwenyekiti, katika nchi nyengine yanapata ruzuku kubwa sana kutoka nchi zao. Sisi tunashukuru na kama nilivyosema kwamba Serikali imetupa ruzuku, katika hili tumekubaliana na Mhe. Waziri wa Fedha yule pale si leo wala jana, ni kipindi kwamba ameshaelekeza karatasi anayo,

barua yangu anayo na yeye ameshaelekeza kwa watendaji wake kwamba watilieni fedha wale vijana. Mimi nitahakikisha Mheshimiwa, kwamba mwezi huu wa Ramadhani haumalizi pesa zao watazipata.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri na huu ndiyo umakini wa Waziri, anasema mwezi huu wa Ramadhani panapomajaaliwa haumalizi. Ninataka kujua kuwa pesa zote hizi watapewa au watapewa nusu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, katika mtu ambaye ninayemuamini kwenye miongoni mwa Mawaziri ni Waziri wa Fedha. Mgumu wa kukubali jambo lakini akishakukubali na akishalifahamu anatekeleza na yeye ni *very sympathetic* na hawa vijana.

Ananiambia Mhe. Waziri, hili mimi na wewe. Sasa mimi ninamuamini sana Mhe. Omar Yussuf Mzee. Sasa ameshaniahidi hili Mhe. Mwenyekiti, tutalipata. Kwa hivyo, sina wasi wasi naye hata kidogo.

Suala la gazeti, Wizara, Bodi na *Management* ya Shirika tumekubaliana kwamba pale pahali sasa wahame na tushapata majengo mawili, tunayaangalia na baada ya muda tutahapa pale kwenda katika maeneo ambayo tumeyaona ni mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *microwave link* iliopo hapo juu na iliopo *ZBC* hazina matatizo, *technically* hazina matatizo, mimi ni fundi kidogo. Kwa hivyo, baada ya kuuliza mimi nilikwenda *ZBC* leo mchana, zile zikishaonana baina ya *link* na *link communication* inakwenda. Kwa hivyo, sijui maelezo aliyoyapata ni yapi, lakini mimi kama waziri, mimi kama fundi bado nahisi kwamba *technically very thing is ok* hapo juu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakubaliana na majibu ya Mhe. Waziri, lakini mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, hiyo bajeti ya kuwalipa wale inatoka wapi. Mhe. Waziri wa Fedha, yupo hapa uzuri wenyewe, tupe ufafanuzi Mhe. Waziri wa Fedha. Inuka Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, nataka nitowe ufafanuzi juu ya suala ambalo Mhe. Jaku Hashim, ameniuliza. Nimepata maombi kutoka kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na hili shirika lina ruzuku kutoka serikalini, na katika hiyo ruzuku yao Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ameniomba basi sehemu ya ruzuku nimpatie aweze kuitumia ili aweze kuwalipa vijana hao. Kwa hivyo, na mimi nimemuahidi kwa kushirikiana na watendaji wangu, tutahakikisha kwamba hiyo ruzuku inapatikana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Namalizia Mhe. Mwenyekiti. Hiyo ruzuku ni lini itapatikana.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Jaku Hashim, kwamba mwaka huu utamaliza tarehe 30 Juni, na ruzuku yao iko ndani ya mwaka huu, itapatikana katika mwezi huu wa Juni. *(Makofi)*

KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA MAENDELEO YA HABARI NA UTANGAZAJI

Programu Ndogo S01 Upatikanaji na usambazaji wa habari	Shs. 3,601,853,000
Programu Ndogo S02 Usimamizi wa vyombo vya habari na utangazaji	Shs. 240,000,000
Jumla ya Kifungu	**Shs. 3,841,853,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA MAENDELEO UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuzunguka sana. Niko katika kesi ambayo iko Mahakamani, Mhe. Waziri, huo ni muda mrefu ingawa Kanuni hazitaki uzungumze, lakini mpira unazidi kuporomoka na kiwango cha mpira. Sijui kesi hii imefuatiliwa vipi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mjumbe: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni zetu hazituruhusu kuzungumzia mwenendo wa kezi iliyoko Mahakamani. Kwa hivyo, namshauri Mhe. Mjumbe, kwa sababu tunaongozwa na Kanuni za Baraza lako tukufu, suala hili bora kuzingatia, kwa sababu tusije tuka-*influence* maamuzi ya Jaji.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tuendelee.

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA MAENDELEO UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Programu Ndogo S01 Uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria	Shs.1,585,349,000
Programu Ndogo S02 Uendelezaji wa utalii na ukuzaji wa michezo	Shs. 1,369,720,000
Jumla Kifungu	**Shs.2,955,069,000**

KIFUNGU P03 - PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Programu Ndogo S01Kuratibu na kusimamia mipango
mikuu ya wizara Shs.2,620,305,000
Programu Ndogo S02

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kabla ya kutoa hoja yangu hapa, niombe tu mawaziri wasikimbilie kila hoja Wizara ya Fedha, kwa sababu Wizara ya Fedha ina bajeti yake, wazingatie *reallocation* ya wizara husika. Kwa hivyo, kila jambo wakipelekea Wizara ya Fedha, itabidi aseme mambo ambayo kwenye bajeti hayapo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kifungu S02 H01, ujenga uwezo na mazingira mazuri ya wafanyakazi kwenye wizara. Mhe. Mwenyekiti, nilihoji hapa kwamba utaratibu mzima wa wizara yake, wanapoamua kuwahamisha au kuwaondosha wafanyakazi kwa hoja mbali mbali, nilipongeza kwamba hoja moja waliyofanya Bwawani ya kuwaondosha wafanyakazi kwa kisingizio kwamba walikuwa na vyeti *fake* vya kughushi 150. Lakini nikahoji kwamba *ZBC* ikiwa hii mipango na sera yote iko chini ya wizara, maamuzi yoyote ya *ZBC* kama shirika ni lazima yaidhinishwe na bodi. Nikahoji kwamba kuna wafanyakazi wanapata *harassment* mbali mbali kwa sababu ya utendaji wa *ZBC*. Hata bodi haina baraka zake. Sasa Idara hii ya sera na mipango, kifungu cha S02 H01 ni kifungu ambacho lazima kifuate maslahi ya wafanyakazi na mazingira mazuri.

Mhe. Waziri, naomba anieleze orodha ambayo nimempa ya wafanyakazi 22, waliotakiwa kuhamishwa hata bila ya idhini ya bodi ni idhini ya nani?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mjumbe: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza hiyo orodha Mhe. Mjumbe hajanipa. Pili, *ZBC* ina sheria yake, sasa kama kuna mjumbe wa bodi amemlalamikia kwamba wao hawashirikishwi katika maamuzi. Mimi Mwenyekiti wa bodi ni mtu wangu wa karibu. Tatu, na wajumbe wangu wa bodi nimewateuwa mimi, sijapata malalamiko hayo. Kwa hivyo, ni vigumu kuyatolea maelezo hoja ambayo sina msingi nao madhubuti.

Sheria ya *ZBC* inaruhusu ama bodi kuitwa au bodi kupelekewa *secular*. Sasa sijui jambo ambalo analalamikia ni lipi hasa, mimi nilidhani ile barua atania, hakunipa nikaitizama. Nilikuwa na kikao na watendaji wangu niliwaeleza wakasema hawana kumbukumbu na hilo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, itakuwa tabu sana kulitolea jawabu jambo ambalo sina msingi madhubuti wa maelezo yake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika kidogo kwa sababu hii hoja niliitoa asubuhi na mimi sikai Kenya, nakaa hapa hapa Unguja, angeniita wakataka ufafanuzi, lakini ninahakika wizara wanajua, kwamba kuna wafanyakazi wamepata *harassment* mbali mbali za kuhamishwa hapa na pale, asubuhi nilisema hapa, kuwa kuna wafanayakazi zaidi ya 22 ambao walipata barua ya wizara kwamba wafanyakazi wa *ZBC* wahamishwe kule *ZBC* kwa sababu hawana kazi na nilisema mpaka barua yenyewe, natambua kuwa *ZBC* ina sheria yake, lakini msimamizi wa sera na sheria ni Idara ya Mipango.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ikiwa sheria ya *ZBC* inavunjwa chini ya Idara yako ya Mipango ambayo ndio msimamizi, leo unaniambia huna taarifa mpaka nikuletee waraka wangu, kwamba huu waraka ni wa kusadikika. Mhe. Mwenyekiti, nadhani nimuambie waziri kwamba wafanyakazi wanahofishwa, wanasumbuliwa kwa sababu ya nguvu fulani ya watu fulani. Sasa sera na mipango ndio idara yako inasimamia masuala ya wafanyakazi. Kifungu S01 H01 ni kifungu ambacho kinalinda mazingira mazuri ya wafanyakazi. Ndio maana kwa majibu haya Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, akatuonesha kwamba hata hawa wapiga kamera humu, kuwa haya malipo ni hidaya tu sio haki yao.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, bado nataka ufafanuzi ni kwa nini Idara ya Mipango na Sera ikashindwa kusimamia watoto wake, kulinda sera na mipango ya wizara.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mjumbe: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Mjumbe. Kama nilivyosema awali kwamba uhamisho kutoka idara moja kwenda idara nyenyengine ni suala la kawaida katika wizara na katika taasisi, sio unyanyasaji huu hata kidogo. Ingekuwa kasimamishwa kazi, kapewa likizo bila ya malipo, ndio ungesema huyu ameonewa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mwenyewe kwamba wafanyakazi wengine hawana kazi wamekaa tu, sasa kumuhamisha kutoka eneo moja kwenda eneo jengine huo sio unyanyasaji. Kama nilivyosema pale kwamba *ZBC* itakuwa na *reform* kubwa, itapunguza wafanyakazi wengi, wafanyakazi 325 ni wengi sana kwa shirika lile. Kwa hivyo, tunapanga hivyo tutakwenda nalo kwa awamu kadiri tutakavyoweza. Kwa hivyo, wafanyakazi kuhamishwa pale wasione kama labda wameonewa, ni jambo la kawaida. Watahamishwa kwa mujibu wa *reform* ambayo sisi wizara na kwa kushauriana na Shirika, tumeona kwamba ni lazima.

Mhe. Mwenyekiti, tumekubaliana na bodi. Mimi siku ambayo nilikwenda kuizindua bodi na niliwapa kazi hiyo ya kuhakikisha kwamba tunali-*reform* Shirika la *ZBC* na haliwezi kwenda vizuri lile kwa utitiri ule wa wafanyakazi abadani. Kwa

hivyo, Mheshimiwa, huo ndio mtazamo wa wizara na ndio mwelekezo wa wizara, kwamba tutawahamisha wale ambao tutawaona ni *redundants.*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na wafanyakazi kuhamishwa. Mfanyakazi madamu amejaza mkataba ni lazima afuate utaratibu wa wizara. Kwa hivyo, nia yangu kuhamishwa au kupewa chochote kile ni kwa utaratibu wa sheria na taratibu, hiyo ndio hoja yangu, kwamba kuhamishwa au kufukuzwa chochote kile ni utaratibu wa sheria na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi hao 22 ambao walikuwa wahamishwe *ZBC* nilishtuka ilikuwa haina habari, baada ya kumuona mtangazaji mahiri, na naomba nimtaje anaitwa Omar Said Ameir, huyu ni jembe *ZBC*, baada ya kufika huyu kuhamishwa ndio Mkurugenzi *ZBC* akashtuka alaa! kumbe kuna watu wanahamishwa, ndio akazuwia zoezi wakati huo tayari wengine wamesha athirika, nani mwenye mamlaka hayo ikiwa sio bodi, bodi inayo habari na kama bodi haina habari ithibitishe hapa kwamba haina habari. Kuna mtu anawa-*punch* wenziwe bila ya utaratibu, yeye anamjua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, una maelezo zaidi. Basi nadhani waziri akubali kuyasimamia haya, ili tuone kwamba yanakwenda kwa utaratibu uliopo na baada ya hapo tuendelee.

Programu Ndogo S02 Uwezeshaji na usimamizi katika sekta za

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri, alikuja akayatoa hapa, katika kuelezea juu ya kadhia hii ya hawa wafanyakazi ambao wamo humu ndani.

Sisi tunaelewa kwamba hii sio *reinstate* au watu wakawa wanalipwa malipo ambayo yalikuwa yanahitajika humu ndani. Tunachozungumzia ni kwamba Baraza la Kumi na Nane ndio walikuwa wamelipwa. Sasa hivi tuko katika Baraza la 20, hapa katikati hapa malipo yao hayajapatikana na maisha yanavyokwenda Mhe. Mwenyekiti, kama unavyoyaelewa.

Je, ni lini wafanyakazi hawa watapatiwa haki zao, hii ndio hoja yetu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza hii Baraza la 20 sio sahihi, hili ni Baraza la Nane, labda mkutano unazungumzia. Hebu tupe maelezo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mjumbe: Mhe. Mwenyekiti, kuna haja tena ya kutoa maelezo baada ya hoja ya Mhe. Jaku Hashim, kuhusu suala hili kuzungumzwa tena.

Mhe. Mwenyekiti: Kama yapo tupe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe.Waziri wa Fedha, tumeshashauriana, tumeshakubaliana na Mhe. Waziri wa Fedha, keshawaahidi kwamba kabla ya kumaliza mwezi huu wa Juni, siku ambayo bajeti ya serikali inakwisha, mimi nadai milioni 148, basi atahakikisha kwamba anatutilia pesa kwa ajili ya kuwalipa, ndio majibu hayo yamekwisha kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti: Haya, nafikiri tuendelee.

Programu Ndogo S02 Uwezeshaji na usimamizi katika sekta za Habari,
Utamaduni, Utalii na Michezo Shs.1,370,153,000

Programu Ndogo S03 Kuratibu na kusimamia uendeshaji na
mipango ya Ofis Kuu Pemba Shs.1,038,920,000
Jumla ya Kifungu **Shs.5,029,378,000**
Jumla Kuu **Shs.11,826,300,000**

FUNGU J02 - KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 03 Kamisheni Ya Utalii Shs.1,656,951,000
Jumla Kuu **Shs.1,656,951,000**

FUNGU J02 - KAMISHENI YA UTALII

KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII

Programu Ndogo S02 Utangazaji na uhamasishaji wa utalii Shs. 304,500,000
Jumla ya Kifungu **Shs. 304,500,000**

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII
Programu Ndogo S01Kuratibu na kusimamia maendeleo
ya Utalii Shs.921,400,000
Jumla ya Kifungu **Shs. 921,400,000**
Jumla Kuu **Shs. 1,225,900,000**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa, tukae. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mjumbe: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu, bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji. Wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuruni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya leo kama kawaida yenu na kwa mashirikiano makubwa mliyotupa, ambayo yamesaidia kuzifanya shughuli zetu ziende vizuri.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe, sasa nakiahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 17 Juni, 2015, saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:43 usiku kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 17/06/2015 saa 3:00 asubuhi)